# Nipashe

Ijumaa Mei 31, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579932

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US







## RC Makonda amuenzi Dk. Mengi kuwafuturisha watu wenye ulemavu

UKURASA 2




UKURASA 13



# Mifuko mbadala sasa changamoto

• **Leo** ni mwisho wa matumizi, huku bei ya mifuko mbadala na upatikanaji wake vikiibua maswali... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**WAZIRI MKUU AIAGIZA BODI UNUNUZI PAMBA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) kuchukua jukumu la utoaji leseni za ununuzi wa...

UKURASA WA 7

**WATU 2,830 WAUGUA DENGUE**

UGONJWA wa homa ya dengue, umeendelea kushika kasi nchini hasa katika Jiji la Dar es Salaam, ambako watu 2,831...

## Kipindu-pindu chaua watu 4 Dar

UKURASA 3



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakichangamkia fursa kwa kuuza vikapu, badala ya mifuko ya plastiki, katika eneo la Mbezi Mwisho, jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Bibi adaiwa kumchoma mjukuu kisa kisamvu

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YASAJILI MASHINE HATARI UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6




Rais John Magufuli akikagua gwaride la heshima katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Robert Mugabe, jijini Harare, Zimbabwe jana, kabla ya kupanda ndege ya Shirika la ATCL, kurejea nyumbani. Rais Magufuli alikuwa katika ziara rasmi katika nchi za Afrika Kusini, Namibia na Zimbabwe. **PICHA: IKULU**

## JPM arejea nchini

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alirejea nchini akitokea Zimbabwe ambako alifanya ziara ya kiserikali ya siku 3 kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo, Emmerson Mnangagwa.

Kabla ya kufanya ziara hiyo, Rais Magufuli alifanya ziara Afrika Kusini ambako pamoja na kuhudhuria sherehe za uapisho wa Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa, alifanya mazungumzo na kiongozi huyo, Ikulu jijini Pretoria.

Baadaye Rais Magufuli akaelekea Namibia ambako alifanya ziara ya kitaifa kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo, Dk. Hage Geingob, ambapo pamoja na kufanya naye mazungumzo, alifungua mtaa mkubwa uliopatiwa jina la Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, na pia alitembelea eneo walipozikwa mashujaa wa ukombozi wa Namibia na kiwanda cha nyama cha Meatco.

Alipowasili katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) Jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli alipokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo.

# Bibi adaiwa kumchoma mjukuu kisa kisamvu

**Na Consolata Evarist,** GEITA

MKAZI wa Kata ya Buhalahala mjini Geita, Magreth Digugulo, anadaiwa kumchoma moto na kisha kumkatakata na wembe mjukuu wake kwenye mkono wa kulia kwa madai ya kukomba mboga.

Mtoto huyo (jina linahifadhiwa) alizungumza na Nipashe jana nyumbani kwao alitaja sababu za kufanyiwa kitendo hicho kuwa ni kujipakulia mboga aina ya kisamvu.

Alisema siku ya tukio, hakuwa amekwenda shuleni ila hakuwapo nyumbani na baada ya kurudi alipakua mboga kidogo akala na baada ya bibi yake kurudi, alimwita na kumkaripia ndipo akamchoma moto na kumkatakata vidole na wembe.

"Sikuwa nimeenda shuleni siku hiyo. Baada ya kutoka kucheza nilikuja nyumbani kula, sikumkuta bibi hivyo nikajipakulia mboga kidogo nikala. Bibi aliporudi akasema nimekomba mboga ndiyo akanifanyia hiki kitendo," alisema.

Baadhi ya majirani ambao walishuhudia tukio hilo, akiwamo Ayoub Bwanamadi, ambaye ni Mratibu wa Mtandao wa Marafiki wa Elimu, alisema walipata taarifa za tukio hilo na baada ya kusogea eneo la tukio, walitafuta namna yakumsaidia mtoto huyo.

Kwanza, alisema walitaka kujua nini chanzo cha tatizo na walimuuliza bibi yake akawajibu mtoto amekomba mboga ndiyo maana amemchoma moto.

Alisema tabia hiyo inaonekana imezoeleka kwa bibi huyo kutokana na mtoto kuonekana na majeraha mengine makubwa kwenye mwili wake ambayo yamekwisha pona.

"Hali ilivyo kwa huyu mtoto ni kama matukio haya ni ya kujirudia. Ukitazama kwenye kiganja cha mkono wake kuna kovu moja na mtoto anavyodai bibi alishawahi kumchoma kwenye majivu kabla ya tukio hili," alisema Bwanamadi.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata hiyo, Neema Emmanuel, alisema alipokea taarifa ya tukio hilo na kumpeleka mtuhumiwa polisi kisha kumpeleka mtoto hosptalini kwa ajili ya matibabu.

"Mwezi huu wa tano (Mei) matukio kama haya yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara. Hili ni tukio la nne kutokea kwenye kata yangu, mengine tumeshayafikisha kwenye ngazi husika. Hata hivyo tunawashukuru wananchi wamekuwa wakitoa taarifa za matukio haya," alisema.

Babu mzazi wa mtoto huyo, Stephano Matata, alisema tukio hilo limemsikitisha kutokana na mtoto huyo kutokuwa na msaada wowote wa malezi ya wazazi wake kwa kuwa anaishi na bibi yake kwa sababu mama yake mzazi ameshatokomea kwenye machimbo huku baba akiwa hajulikani ni nani.

"Mimi huwa sikai hapa nyumbani, lakini nilivyopata taarifa hizi zilinisikitisha kwani huyu mtoto ni kama hana wazazi. Mimi nitamchukua nikae naye kwa sababu hana msaada mwingine," alisema Matata.

# Makonda aandaa futari kumuenzi Mengi

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kumuenzi aliyekuwa Mwenyekiti wa IPP, Dk. Reginald Mengi (marehemu), Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ameandaa futari kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Makonda ameandaa futari hiyo kwa zaidi ya watu 4,000 wenye ulemavu wa mkoa huo kwa lengo la kuonyesha upendo na kudumisha mshikamano katika mkoa huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Makonda alisema amealika walemavu kutoka Jiji la Dar es Salaam ambao watahudumiwa chakula na watu mashuhuri nchini, wakiwamo watangazaji, wasanii, wachezaji mpira, Jeshi la Polisi na watumishi wa benki.

"Wakati wa msiba wa Dk. Mengi, niliahidi kumuenzi kwa kuhakikisha naendelea kuwalisha walemavu kama sehemu ya jukumu kubwa alilokuwa akilifanya. Aliifanya kazi hii kwa upendo mkubwa na bila kutegemea kurudishiwa fadhila yoyote," alisema Makonda.

Aliongeza kuwa: "Dk. Mengi alikuwa akihakikisha watu wenye ulemavu wanakula pamoja, kufurahi na kubadilishana mawazo, hivyo jukumu hilo nitalifanya kama alivyofanya ili kuendelea kudumisha upendo huo.

"Ndio sababu ya kusema sijawahi kuona mtu kama Dk. Mengi ambaye hakujali utajiri wake, alijitoa kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Ingawa maandiko yanaelekeza hivyo hakuna watu walioweza kufikia upendo wake," alisema.

Alisema alichoamua kufanya ni kuungana na Waislamu katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa kuandaa futari kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kushiriki pamoja karamu hiyo.

"Hii haitakuwa tu futari bali nimewashirikisha watu mashuhuri kama watangazaji, wachekeshaji kama Masanja, wachezaji mpira, watumishi wa umma na sekta binafsi ambao watakuwa sehemu ya kuwahudumia watu wenye ulemavu," alisema Makonda.

Aliwataja miongoni mwa watu mashuhuri 500 wanaotarajiwa kuwahudumia watu wenye ulemavu katika futari hiyo ni Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/ Redio One, Joyce Mhavile; aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Tido Mhando,

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Kipindupindu chaua watatu Dar

**Na Mary Geofrey**

WATU watatu wamepoteza maisha jijini Dar es Salaam kutokana na ugonjwa wa kipindupindu, huku watu 40 wakiwa wamelazwa.

Kutokana na ugonjwa huo, tayari Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeandaa kambi tatu za kutibu wagonjwa katika hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala.

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Yudas Ndugile, aliliambia Nipashe jana kuwa wagonjwa wengi wanatoka katika wilaya ya Temeke na Ilala wachache.

Alitaja maeneo ambako wanatoka wagonjwa wengi ni Buza, Keko, Mtoni Kijichi, Tandika, Chamazi, Kivule na Mtaa wa Azimio katika wilaya ya Temeke.

Dk. Ndugile alitaja maeneo mengine kuwa ni Mchikichini, Kigogo, Kariakoo, Vingunguti na Ilala kwa upande wa Wilaya ya Ilala.

"Tayari katika mkoa wetu tuna wagonjwa takribani 40 na wengine watatu wameshapoteza maisha kutokana na kuugua ugonjwa wa kupindupindu," alisema Dk. Ndugile.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, alisema tayari wameshachukua tahadhari katika maeneo mbalimbali ya jiji ikiwamo maofisa wa afya kufanya ukaguzi wa mazingira katika kata na mitaa yote pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuepuka kuenea kwa ugonjwa huo.

Aliwata wakazi hao kuchukua tahadhari ya kutotiririsha majitaka, kuzingatia usafi wa mazingira, kunawa mikono, vyakula kupashwa moto, kuosha matunda na mbogamboga ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu.

Juzi, Waziri Ummy aliwataka wananchi wa Dar es salaam kujihadhari na janga hilo kwa kuacha kutiririsha majitaka mitaani hasa katika kipindi hiki cha mvua.

Aidha, alizitaka Manispaa za Dar es Salaam kuweka faini kubwa kwa wote wanaotiririsha maji machafu mitaani na kuwataka wananchi wawaripoti.

Ugonjwa huo, ulianza kuripotiwa wiki iliyopita katika maeneo kadhaa ya jiji hilo, huku chanzo kikitajwa ni kutiririsha maji ya chooni mtaani.



Mafundi wa Kampuni ya Estim, wakiendelea kazi ya awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19. **PICHA: JOHN BADI**

# Kesi ya vigogo TPDC yakwama

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imeshindwa kuendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri katika kesi ya matumizi mabaya ya madaraka dhidi ya vigogo watano wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), akiwamo Mkurugenzi Mtendaji, James Mataragio, kwa madai ya kuwa shahidi mgonjwa. Kesi hiyo ilipangwa kuendelea kusikilizwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Kevini Mhina. Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Aneth Mavika, alidai kuwa kesi hiyo ilikuja kwa ajili ya kusikilizwa lakini mashahidi waliowategemea ni wagonjwa. "Mheshimiwa mashahidi tuliowategemea leo hii ni wawili mmoja mgonjwa na mwingine amehamishiwa kikazi jijini Dodoma, naiomba mahakama yako ipange tarehe nyingine ya kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri," alidai Mavika.

Upande wa utetezi katika kesi hiyo walidai mahakamani hapo kuwa hawana pingamizi na maombi ya Jamhuri.

Hakimu Mhina alisema itaendelea kusikilizwa Juni 20, mwaka huu, upande wa Jamhuri uhakikishe unapeleka mashahidi wao.

Mbali na Mataragio, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni, Kaimu Meneja wa Uvumbuzi, George Seni, Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Utawala, Wellington Hudson, Mkurugenzi wa Mkondo wa Juu, Kelvin Komba na Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Edwin Riwa. Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa wametenda kosa hilo kati ya Aprili 8, 2015 na Juni 3, 2016. Inadaiwa wakiwa watumishi wa umma na waajiriwa wa TPDC kwa nafasi zao, wakati wakitimiza majukumu yao kwa makusudi walitumia madaraka vibaya. Inadaiwa walibadilisha na kupitisha bajeti na mpango wa mwaka wa manunuzi wa mwaka 2014/2015 na 2015/2016 kwa kuingiza ununuzi wa kifaa cha utafiti cha airborne gravity gradiometer survey ndani ya ziwa Tanganyika bila ya kupata kibali cha bodi ya wakurugenzi ya shirika.

Inadaiwa kitendo hicho kinakiuka kifungu cha 49(2) cha sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kwa lengo la kujipatia manufaa yasiyohalali ya Dola za Marekani 3,238,986.50 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 7.2 kwa Bell Geospace.

Washtakiwa waliposomewa mashtaka yao walikana kwa nyakati tofauti na wapo nje kwa dhamana.

# Sakata la korosho laibuka tena bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imeibua tena sakata la kutouzwa kwa korosho zilizokusanywa na serikali kutoka kwa wakulima hivi karibuni.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini Dodoma jana kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Esther Matiko, kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba (Chadema), alisema kambi hiyo inaitaka serikali kumwondoa madarakani Balozi wa Tanzania nchini Kenya kutokana na sakata hilo.

Alisema balozi huyo hakutimiza wajibu wake kuishauri vizuri serikali wakati wa kuingia mkataba na Kampuni ya Indo Power ya Kenya kununua korosho nchini.

Makamba alilieleza Bunge kuwa Januari 30, mwaka huu, serikali iliingia mkataba na kampuni hiyo ya Kenya kununua korosho zilizokusanywa na serikali hasa kutoka mikoa ya kusini na korosho hizo mpaka sasa zinaonekana kudoda kwa kukosa soko.

Alisema taarifa za baadaye za kiuchunguzi uliofanywa na gazeti la Daily Nation la Kenya zilibaini kuwa kampuni hiyo ni hewa na haina hata ofisi Kenya.

"Matokeo ya uzembe huo wa serikali wa kuingia mkataba na kampuni ya nje bila kuifanyia upekuzi, yaani 'due diligence' ni kwamba mpaka sasa hakuna korosho zozote zilizonunuliwa, jambo ambalo limeisababishia serikali hasara kubwa," alisema.

Alisema kitendo cha serikali kuingia mkataba na kampuni hiyo isiyo na uwezo wa kununua korosho kinadhihirisha kwamba balozi za Tanzania hazina kazi za kufanya hasa katika utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi na hazina weledi wala ufanisi kutokana na kutoelewa majukumu yao ipasavyo.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa ufafanuzi ni kwanini mpaka leo pamoja na hasara kubwa iliyotokea maofisa waliohusika katika mkataba huo wanaendelea na nyadhifa zao?

"Nini ilikuwa wajibu wa Ubalozi wa Tanzania Kenya katika mkataba wa Indo Power na Tanzania? Serikali ina mpango gani wa kuwachukulia hatua na kuwaburuza mahakamani wale wote waliohusika na mkataba feki wa Indo Power katika sakata la korosho nchini?

"Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha zao la korosho nchini linaendelea kubaki kwenye mzunguko wa kimataifa?" Makamba alihoji. Mbunge huyo pia alisema kambi yao inatambua kuwa balozi nyingi za Tanzania kwenye nchi mbalimbali zina changamoto ya uhaba wa rasilimali watu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 31/05/2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 03-06-2019** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.00 |
| Upana | - | mita | 2.84 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

3. Njia itakayotumika: SINGIDA hadi DAR ES SALAAM kupitia DODOMA.

Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215256202

# Mifuko mbadala changamoto

**Na Waandishi Wetu**

LEO ni mwisho wa kutumia na kuzalisha mifuko ya plastiki, hatua inayokuja wakati taifa likishuhudia maelfu ya tani za bidhaa hizo ikiwamo mifuko zikijazana baharini, kwenye maziwa, ndani ya mito na nyingine zikijishindilia, chini na juu ya ardhi.



Machinga akiuza mifuko mbadala ambayo haijatengezwa kwa plastiki katika makutano ya mitaa ya Mkunguni na Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

Wakati katazo la kuzalisha na kutumia mifuko ya plastiki litaanza kutekelezwa rasmi kesho baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wanaona kuwa upatikanaji wa mifuko mbadala ni tatizo kubwa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe maeneo ya Kariakoo kuangalia maandalizi ya kuachana na mifuko ya plastiki, ulibaini kuwa kilio ni uhaba na bei kubwa ya vifungashio rafiki wa mazingira.

Mfanyabiashara Hussen Omary, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema ukosefu wa mifuko mbadala ni changamoto kubwa ya zuio hilo na kutaka kutolewe elimu na mafunzo ya kuzalisha mifuko rafiki wa mazingira kwa kasi na haraka ili kampeni hiyo ifanikiwe.

"Mifuko mbadala michache iliyoko sasa ni ghali mno. Huuzwa kati ya Sh. 500 na 2,000 maeneo ya sokoni Kariakoo. Hizi ni pesa nyingi wananchi wasio na kipato kikubwa hawawezi kuinunua ," alisema.

Aidha, Omary aliishauri serikali ianishe mikakati ya kuzalisha mifuko mbadala ili itengenezwe kwa gharama nafuu na kuuzwa kwa bei ndogo ili kunufaisha wananchi wote badala ya kuacha kama hali ilivyo sasa. Lakini Omary, alieleza wasiwasi kuwa huenda baadhi ya bidhaa kama 'ice-cream,' zikakosekana sokoni kwani vifungashio vyake si rafiki wa mazingira.

Ili kufikia hatua hiyo, baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, waliiomba serikali kuwekeza zaidi kwenye kutoa elimu kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo ili kutumia fursa hiyo kuzalisha mifuko mbadala na kutimiza lengo.

James Kinabo, mfanyabiashara wa nafaka aliishauri serikali badala ya kuanza kutoza faini kuanzia kesho, ianze kutoa elimu kwanza kuhusu athari za matumizi ya plastiki na kuwekeza kwenye kuzalisha mifuko rafiki wa mazingira.

**UKUSANYAJI WA MIFUKO**

Changamoto nyingine iliyobainika ni wananchi wengi kutokuelezwa mahali pa kusalimisha mifuko ya plastiki, licha ya serikali kutoa maelekezo kadhaa.

Pamoja na kuwa inatakiwa kupelekewa ofisi za serikali za mitaa, lakini mkazi wa Tegeta, Yusuf Mugabo, anasema hajui pa kuipeleka.

Mugabo ana maoni sawa na ya baadhi ya wajasiriamali eneo la Mwenge, ambao wanasema hawana taarifa kuhusiana na wapo wanapaswa kuisalimisha.

Licha ya baadhi ya changamoto hatua ya kupiga marufuku hiyo inapongezwa na wengi kama wanamazingira, wateja na wazalishaji, wengine wakiona kuwa zuio hilo lilichelewa kwa kuwa plastiki imechafua mno mazingira.

Uamuzi wa kupiga marufuku plastiki umekuja baada ya kuzirekebisha kanuni za sheria ya usimamizi wa mazingira sura ya 191, na kutunga kanuni nyingine zenye vipengele vinavyopiga marufuku mifuko ya plastiki za mwaka 2019.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika hotuba ya bajeti ya ofisi yake aliyoitoa Aprili mwaka huu, aliwapa mwezi mmoja wenye viwanda, wanunuzi na watumiaji wengine kumaliza shehena za mifuko hiyo kabla ya kesho Juni Mosi, kwani itakuwa ni mafuruku kutumika nchini.

**FURSA KIUWEKEZAJI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (Leat), Dk. Rugemeleza Nshala, akizungumzia katazo hilo aliipongeza uamuzi huo, aliouita wa kuokoa mazingira na viumbe.

Alisema zuio la mifuko hiyo ni kilio cha muda mrefu cha wanamazingira kilichochelewa kusikika.

Dk. Nshala, aliongeza: "Ni changamoto kwa wazalishaji, lakini ni fursa mpya kwani wataanza kutengeneza mifuko mbadala rafiki wa mazingira. Tukumbuke kabla ya plastiki kulikuwa na mifuko ya karatasi na katani iliyotunza mazingira."

**JET: TUIGE MAURITIUS**

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wanahabari za Mazingira Tanzania (JET), Ellen Otaru, aliishukuru serikali kupiga marufuku plastiki, akisema walianza kupiga kelele kuhusu suala hilo miongo kadhaa iliyopita.

"Kila Siku ya Mazingira Duniani sauti za wadau zilisikika. Plastiki ilichafua mno mazingira, uamuzi huu ulikuwa hauepukiki japo tulichelewa Zanzibar walishafanya maamuzi haya siku nyingi," alisema.

Alionya kuwa plastiki inachangia kutoweka viumbe bahari pia inachochea mabadiliko ya tabianchi.

"Mabadiliko ya tabianchi yakitokea yanaathiri wote, lakini samaki wakitoweka chakula kinapungua na kuathiri uchumi. Zuio litaokoa viumbe wa bahari, binadamu na mazingira," alisema Otaru.

Alisema inachukuza zaidi ya miaka 100 plastiki kuoza na kwamba taka hizo zimejaa kwenye fukwe za Tanzania na kufanya watalii kuzikimbia.

"Watalii wanatembelea fukwe safi za Unguja na visiwa vya Mauritius zisizo na plastiki," aliongeza Otaru na kusema kuwa Mauritius wako mbele kwani wanatumia mifuko ya plastiki inayoyeyuka baada ya miezi sita ili kutunza mazingira.

Aliitaka Tanzania kuiga kutoka kwa taifa hilo ambalo limemudu kufanya kile kinachoanza kufanyika kesho.

**KUPUNGUZA KANSA**

Mtafiti wa Mazingira na Afya wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (Muhas), Hussein Mohamed, alipongeza hatua hiyo akisema plastiki inaweza kuwa chanzo cha saratani, magonjwa ya mfumo wa uzazi na ini.

"Kuna ongezeko kubwa la matatizo hayo, tunashindwa kutaja plastiki moja kwa moja, lakini matumizi ya plastiki ni mengi na kuna ushahidi wa kisayansi kwamba vitu vilivyoko ndani ya plastiki vinaleta madhara, kuna imani matumizi ya plastiki yanahusika," alisema Mohamed.

Mkufunzi huyo wa Muhas, alisema plastiki zina madhara mengi mwilini ambayo huchukua hata miaka 20 kabla ya kujulikana na kwamba katazo hilo ni muhimu kiafya.

**KILIO VIWANDANI**

Katazo hilo la uzalishaji na matumizi ya plastiki limeacha kilio kwa baadhi ya viwanda, kwa mujibu wa Meneja wa moja ya viwanda vinavyozalisha plastiki nchini, Mohamed Ally, anasema tangazo la serikali liliwafukuzia wateja.

Akizungumzia hatua hiyo alisema wamepata hasara na wamelazimika kufukuza wafanyakazi ambao sasa hawana ajira.

"Baada ya tangazo la serikali hakuna aliyekuwa anataka kununua mifuko yetu tena, matokeo yake tumejikuta mzigo umebaki bila mnunuzi, kwa sasa tumefunga biashara na wafanyakazi zaidi ya 100 wako nyumbani," alisema.

Aidha, walifunga kiwanda hicho na wanajipanga kwa ajili ya mambo mengine, ikiwamo kuzalisha mifuko mbadala. "Tunakubaliana na serikali kwa kuwa ni uamuzi wa kutunza na kuyaokoa mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho. Mifuko tuliyokuwa tunazalisha ilikuwa ni kwa mujibu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), ambayo ni macrons 50," alisema.

Aidha, alikumbusha kuwa mifuko laini ambayo haina ubora ilikuwa inatoka nchi jirani na ndiyo iliyolijaza soko la ndani.

**KUKIUKA KATAZO**

Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), lilieleza kuwa kanuni za usimamizi wa mazingira za kupiga marufuku mifuko hiyo za mwaka 2019 limetaja faini na adhabu ya kifungo kwa watakaokiuka katazo.

Mwanasheria wa NEMC, Manchare Heche, alifafanua kuwa kuzalisha au kuingiza nchini mifuko hiyo faini yake haitapungua Sh. milioni 20 na kuzidi Sh. bilioni moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

"Kusafirisha nje mifuko ya plastiki, kunabeba faini isiyopungua Sh. 5,000,000 na isiyozidi Sh. milioni 20 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja."

Alikumbusha kuwa kuhifadhi au kusambaza mifuko hiyo, adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. milioni tano na isiyozidi Sh. milioni 50 au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Kwa wauzaji wa mifuko hiyo alisema adhabu yake ni faini ya Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 500,000 au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja, anasema Heche.

"Wamiliki au watumia mifuko hiyo, adhabu yao ni faini isiyopungua Sh. 30,000 na isiyozidi Sh. 200,000 au kifungo kisichozidi siku saba au vyote kwa pamoja," alionya

Aidha, alisema wanaoingiza nchini, kusafirisha nje au wanaozalisha vifungashio vya plastiki ambavyo havijazuiliwa wahakikishe vinakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na TBS.

**KUTUPA PLASTIKI OVYO**

Heche aliwaonya wanaokula au kutupa vifungashio vya plastiki ovyo kuwa watakabiliwa na adhabu kali.

"Tunatoa tahadhari kwa abiria wanaotumia usafiri wa umma, wamiliki wa mabasi, meli, bajaji na bodaboda waelewe kwamba adhabu ni kuanzia Sh. 200,000. Ukimaliza kula karanga, kunywa maziwa, au bidhaa iliyo katika kifungashio ambacho hakijakatazwa na unatupa ovyo sheria itachukua mkondo wake kuweni makini sana," alionya Heche.

**Imeandikwa na Salome Kitomari, Mary Geofrey na Elizabeth Zaya**

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Utoaji wa Elimu ya Demokrasia, Utawala Bora, Uraia na Upigaji Kura Tanzania (Tafeyoco), Elvice Makumbo (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuanza kutoa elimu hiyo nchi nzima kuanzia Julai mwaka huu. Kulia ni Mkuu wa Miradi wa shirika hilo, Emmanuel Kanumba na Mratibu wa Vijana, Mchungaji Steven Mtiro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Upinzani wataja mambo manne yanayoiangusha nchi kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imeliambia Bunge kuwa kwa sasa kuna mambo manne yanayoiangusha Tanzania kimataifa.

Akiwasilisha hotuba bungeni jana kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Esther Matiko, kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba (Chadema), alisema mambo hayo yamekuwa na madhara makubwa kwa taifa.

Huku hotuba yake ikilazimika kufutwa katika baadhi ya maeneo kutokana na kupingwa na wabunge kadhaa wa Chama Cha Mpainduzi (CCM), Makamba aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na matukio ya kutekwa kwa watu mbalimbali hasa wanaoonekana kuikosoa serikali.

Alisema mambo mengine matatu yanayoichafua Tanzania kimataifa ni kupotezwa kwa watu pasi na hatua madhubuti kuchukuliwa na vyombo vya dola, majaribio ya kuuawa kwa viongozi wa kisiasa na kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari.

"Tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano mwaka 2015, kumekuwapo na ongezeko la ukiukwaji wa haki za binadamu, uminywaji wa demokrasia na uvunjwaji wa sheria mbalimbali tulizojiwekea wenyewe kama taifa," alisema.

Makamba aliongeza: "Taarifa ya Haki za Binadamu ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ya mwaka 2018, ilionyesha hali ya hatari kwa Tanzania kwa kubainisha matukio ya mauaji, kutekwa na kupotezwa kwa watu, uvunjifu mkubwa wa sheria na katiba ya nchi pamoja na ukandamizwaji mkubwa wa vyama vya upinzani.

"Hali hii pia inajishajihishwa na ripoti ya Freedom House kwa Tanzania kwa mwaka 2018. Mambo haya si tu yameichafua na yanaendelea kuichafua Tanzania, bali yana athari za moja kwa moja kama vile kudorora kwa shughuli za uchumi na kudorora kwa uhusiano baina ya Tanzania na jumuiya ya kimataifa."

Makamba pia alisema kambi yao inaitaka serikali kuhakikisha kunakuwa na kanzidata inayoonyesha idadi kamili ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi na taarifa za wanachokifanya huko. Alisema kambi hiyo pia inaitaka serikali iweke wazi msimamo wake kuhusu uhusiano wa kidiplomasia baina yake na Umoja wa Ulaya (EU) na hasa sababu zilizopelekea kuondolewa kwa balozi za umoja huo nchini mwishoni mwa mwaka jana.

# DECI hatimaye yakata rufani

**Na Hellen Mwango**

KAMPUNI ya Development Entrepreneurship for Community Initiative (DECI) imewasilisha kisudio la kukata rafani kupinga hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam ya kutaifisha magari, mali zisizohamishika (nyumba) na Sh. bilioni 14.3 kuwa mali ya serikali.

DECI kupitia wakili Majura Magafu, imewasilisha kusudio la kukata rufani Mahakama ya Rufani Tanzania, kupinga hukumu ya mahakama hiyo iliyotolewa Mei 7, mwaka huu chini ya Jaji Stephen Magoiga.

Kampuni hiyo chini ya wakurugenzi Jackson Mtares, Dominick Kigendi, Timotheo Saiguran Ole Loitg'nye na Samwel Mtares wamewasilisha kusudio kupinga kutaifishwa mabilioni yao na mali zake.

Mapema Jaji Magioga katika hukumu yake alisema bila kuacha shaka walalamikiwa wameshindwa kuthibitisha kwamba mali na fedha taslimu zimepatikana na chanzo tofauti za kampuni hiyo.

Hukumu hiyo ilitolewa baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kufungua maombi ya kutaka kufilisi fedha na mali zote za kampuni hiyo zilizopatikana kwa upatu.

Jaji aliagiza Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kubadilisha umiliki wa magari kutoka DECI kuwa ya serikali, DPP kuwasilisha maombi mahakamani ili madalali wakawahamishe wananchi wanaoishi

INAENDELEA UK. 8

# Majaliwa aiagiza TCB leseni ununuzi pamba

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) kuchukua jukumu la utoaji leseni za ununuzi wa pamba.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana katika mkutano wa dharura wa baadhi ya wadau wa sekta ya pamba uliofanyika jijini Mwanza, na kusema suala la utoaji leseni za ununuzi wa pamba kutolewa na wilaya ilikuwa umechelewesha jukumu hilo kuanza.

Alisema wanunuzi wanapopata leseni leo, kesho wanaruhusiwa kwenda kununua pamba, hivyo viongozi wa wilaya wawaruhusu wasiweke vikwazo katika kutekeleza jukumu hilo.

Pia, alisema katika ununuzi wa pamba, mkulima anapaswa kufungua akaunti benki ili iwe rahisi katika malipo sambamba na kuwataka viongozi kuwaelimisha wakulima na wananchi juu ya uzalishaji pamba bora bila kuchanganya na maji na mchanga.

Aidha, Waziri Mkuu alisisitiza kuwa bei ya pamba itabaki kuwa shilingi 1,200 kwa kilo ili kulinda maslahi ya mkulima.

Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, alisema changamoto iliyokuwapo awali ni suala la upangaji wa bei, lakini katika kikao kilichofanyika Mei 2, wadau walikubaliana na bei elekezi ya serikali, na sasa wapo tayari kuingia sokoni kwa ajili ya kununua pamba.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanunuzi Binafsi wa Pamba (TCA), Christopher Gachuma, alisema wanunuzi wa pamba wapewe leseni kabla msimu kuanza, angalau mwezi moja au miwili kabla ili kuondoa mkanganyiko. Pia alisisitiza kuwa kila mmoja kwa nafasi aliyonayo kumsaidia mkulima kuzalisha pamba kutoka kilo 300 hadi 1,500 kwa kuwatumia maofisa ugani kumwelimisha namna ya kufuata kanuni za kilimo ili kupata tija.

"Hata tukipandisha bei na kufikia shilingi 2,000 kwa kilo, huku uzalishaji ukiwa mdogo, tutakuwa hatujamkomboa huyu mkulima," alisema Gachuma.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Diaspora, mabalozi wamuige Rais Magufuli

**RAIS** John Magufuli, ametangaza habari njema kwa wakulima wa mahindi ambao wamepata soko la kuuza nafaka hiyo, nchini Zimbabwe, ambayo kuanzia sasa itanunua tani 700,000 za zao hilo kutoka nchini.

Jitihada hizo za Rais ni wazi zitawanufaisha wakulima wengi ambao walikuwa na kilio cha kukosa soko la kuuzia mahindi yao, ambayo yalikuwa hayana mnunuzi katika soko la ndani.

Alichofanya Rais pamoja na kudumisha ushirikiano wa nchi za Afrika Kusini kinaongeza pia hamasa kwa wakulima wa mahindi ambao wamepata fursa ya kuzalisha na kuwekeza zaidi kwani kuna uhakika wa soko.

Ni wazi kuwa pamoja na Zimbabwe mataifa kama Kenya, Ethiopia, Uganda, Malawi, Msumbiji na Rwanda ni miongoni mwa nchi zilizoathiriwa na mafuriko ambayo huenda yakasababisha njaa na kuhitaji chakula kutoka Tanzania.

Tunaona kuwa hii nayo ni fursa ya kuuza mazao yanayozalishwa kwa wingi nchini ukiwamo muhogo, maharage na jamii nyingine za nafaka.

Tukizungumzia mihogo ni zao ambalo limezalishwa kwa wingi kwa miaka ya hivi karibuni, lakini halijapata soko la uhakika hasa kutokana na ukosefu wa viwanda vya kutosha vya kusindika na kuchakata bidhaa nyingine zinazotokana na mihogo.

Ni wazi kuwa kama walivyo wakulima wa mahindi, wanaozalisha mihogo nao wangependa juhudi zao kupata fursa ya kuwezeshwa kuuza nje ya mipaka.

Kwa hiyo tunaona ni vyema mabalozi na wana diaspora walioko katika nchi mbalimbali kusaidia juhudi za wakulima kupata masoko ya mazao ya chakula yanayozalishwa kwa wingi kama ambavyo Rais amefanya kwa muda mfupi alipoitembelea Zimbabwe.

Ni wazi kuwa mataifa mengi ya Afrika yanatumia unga wa mahindi au muhogo kama chakula kikuu na Tanzania ni moja ya mataifa wazalishaji wakubwa wa muhogo na mahindi.

Kwa wakulima hii ni fursa kuzalisha unga ulioongezewa thamani ukiwamo wa muhogo na mahindi ambao unaweza kuuzwa kwenye mataifa ya Kusini na Mashariki mwa Afrika ambayo yamekumbwa na mafuriko, ukame na njaa.

Ni jukumu la wawakilishi wakiwamo mabalozi na wana diaspora kutafuta masoko hayo, ili kukuza uzalishaji na uchumi wa raia taifa hili.

Aidha, mazao kama maharage huzalishwa kwa wingi nchini na ni chakula kinachotumiwa na nchi nyingi duniani kuanzia Afrika, Asia, Uarabuni na Uchina.

Tanzania imebarikiwa kuwa na aina mbalimbali tena bora za maharage yakiwamo soya inayozalishwa Mbeya.

Tunaona ni wakati wa kusaka masoko ya mazao hayo na kuwanufaisha wakulima wetu. Japo zama hizi kinachosisitizwa ni kujenga viwanda ili kuyaongezea thamani, vyote hivyo vinaweza kufanyika ili kukuza uchumi wa taifa na kuongeza wigo wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

Chakula ni mojawapo ya mahitaji makubwa barani Afrika mathalani uwapo wa soko kubwa linalopatikana Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na hata Sudan Kusini.

Tunashauri kufunguliwa magulio na masoko ya nafaka hasa mahindi, mtama na muhogo ambayo yatawaalika wafanyabiashara kutoka nchi hizo na nyinginezo kuja kununua mazao hayo hapa nyumbani.

Kama yalivyo magulio na masoko ya dhahabu ni vyema pia kuwa na magulio ya mazao ya chakula ili kuwapa nafasi wafanyabiashara wa nje kuja nchini kununua bidhaa hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tutumie Siku ya Tumbaku leo kutathmini pumzi zetu

**LEO** ni Siku ya Kimataifa Duniani ya Kutovuta Tumbaku, ikiwa na ujumbe mbalimbali kwa jamii wenye lengo la kuacha uvutaji wa kilevi hicho.

Maadhimisho ya mwaka huu yana ujumbe 'usikubali tumbaku ichukue pumzi yako.' Hiyo inabeba maana kwamba, uvutaji wa sigara au tumbaku una madhara, hivyo mtu asikubali matumizi ya kilevi hicho yaondoe uhai wake.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema madhara ya matumizi ya tumbaku kwa mapafu ya binadamu kuwa zaidi ya asilimia 40 ya vifo vikihusiana na matumizi hayo.

Ni vifo vivyohusiana na magonjwa kama saratani, magonjwa sugu ya njia ya hewa na kifua kikuu.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus, anakaririwa kwamba kila mwaka kuna watu milioni nane wanaofariki kutokana na tumbaku, huku mamilioni wengine wanaishi na magonjwa sugu.

Anataja baadhi ya magonjwa hayo kuwa saratani, kifua kikuu, pumu au magonjwa sugu ya njia ya hewa, ambayo yamekuwa yakisababishwa na matumizi ya tumbaku.

WHO inasema, zaidi ya watoto 60,000 wenye umri wa chini ya miaka mitano wanafariki dunia kwa kuvuta moshi. Watu wanaoishi hadi utu uzima wakiwa katika nafasi kubwa zaidi ya kupata magonjwa sugu ya njia ya hewa mara wanapofikia umri wa utu uzima.

Dk. Ghebreyesus anasema mvuto mmoja wa moshi wa tumbaku una mamia ya kemikali za sumu, ambazo huanza kuharibu mapafu, mifumo ya kusafisha makohozi na uchafu kutoka kwenye mapafu inadhoofishwa. Ni jambo linaloruhusu sumu iliyomo katika tumbaku kuingia kwenye mapafu kirahisi.

Anasema, kuna haja ya kujiepusha matumizi ya tumbaku kulinda afya zao, kwa kuzingatia mapafu yenye afya ni muhimu, ili mtu anaweze kuishi maisha yenye afya.

Rai yake ni kwamba, serikali zipunguze matumizi ya bidhaa za tumbaku, kwa kuongeza kodi, kutenga maeneo ya uvutaji, ili kuwasaidia wanataka kuondokana nayo.

"Wazazi, walezi na viongozi wa kijamii wanatakiwa kuchukua hatua kulinda afya za familia kwa kuwaeleza wazi madhara ya matumizi ya tumbaku na mbinu za kujiepusha na matumizi yake," anasema.

Anasisitiza kuwa, udbibiti wa tumbaku utasaidia kufanikisha kupunguza idadi ya wanaofariki dunia kabla ya muda, kutokana na uvutaji tumbaku ifikapo mwaka 2030.

Malalamiko yake ni kwamba, bado dunia haiko kwenye mwelekeo wa kutimiza lengo, hivyo kila mtu anapaswa kulinda mapafu yake, ya rafiki zake na familia, kwa kukataa kutumia tumbaku.

**KILIO CHA TTCF**

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF), Lutgard Kagaruki, anataka sheria inayoendana na matakwa ya Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Tumbaku WHO itekelezwe.

Anasema tumbaku ni kisababishi namba moja cha magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo saratani, moyo, magonjwa sugu ya kifua, kisukari na mengine mengi na pia asilimia 90 ya saratani ya mapafu husababishwa na tumbaku.

"Tanzania ni nchi pekee ndani ya Afrika Mashariki isiyokuwa na sheria madhubuti ya kudhibiti tumbaku; Zanzibar inayo sheria bora na hata Ethiopia juzi juzi imetoa sheria bora kuliko zote Afrika," anasema.

Kagaruki anasema ni wakati sasa kwa serikali kutunga sheria bora, ili kulinda afya, mazingira, uchumi na ustawi wa jamii ya Watanzania.

Tumbaku ni miongoni mwa mazao matano ya kimkakati, ambayo katika mwaka wa fedha 2018/2019, serikali ikilenga kuimarisha masoko yake na mazao hayo kwa kuhamasisha mfumo wa stakabadhi ghalani, huku yakizalishwa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika kwa njia ya minada.

Mwelekeo wa kazi za serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019, wana mtazamo wa katika mkakati huo, lengo kuongeza mapato ya wakulima utokanao na chanzo cha kuaminika cha malighafi katika uchumi wa viwanda na kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira na fedha za kigeni.

Inaelezwa uamuzi wa kuongeza usimamizi katika uzalishaji wa mazao hayo makuu ya biashara unatokana na ukweli kwamba, kwa kipindi kirefu uzalishaji ulishuka kutokana na changamoto kadhaa.

Miongoni mwa sababu hizo ni vyama vya ushirika kutotekeleza vyema wajibu wao, wizi, dhuluma na pia ushiriki mdogo wa maofisa kilimo katika kusimamia kilimo cha kitaalamu.

# Serikali yahimiza uendelezaji uhifadhi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewahakikishia wenyeviti wa Muungano wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA) kuwa itaendelea kuwapa ushirikiano kwa lengo la kuendeleza dhana halisi ya uhifadhi wa wanyamapori shirikishi katika jamii.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alipokuwa akizungumza na wenyeviti hao kwenye mkutano wa siku moja uliolenga kuimarisha ushirikiano kati ya wizara na wadau wa uhifadhi nchini.

Alisema wizara itaendelea kutatua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwa kuwa inatambua mchango mkubwa wanaoutoa katika shughuli za uhifadhi wa wanyamapori nchini.

Aidha, Kanyasu aliziagiza WMA zinazotegemea kufanya uchaguzi hivi karibuni ziendelee na utaratibu wa zamani wa kutumia kigezo cha elimu ya kuanzia darasa la saba na kuendelea.

Kanyasu alisema lengo la kuruhusu kutumika kwa kigezo hicho cha elimu ya darasa la saba na kuendelea ni kutoa fursa kwa wagombea wengi wenye uwezo kujitokeza.

Alizitaka WMA hizo kuchagua viongozi watakaokuwa na uwezo wa kutekeleza mipango mbalimbali kwa ufanisi.

Hata hivyo, alisema yako baadhi ya mambo ya msingi ambayo wizara imeanza kuyaboresha kwenye kanuni za WMA likiwamo suala la kiwango cha elimu kwa viongozi wa jumuiya hizo, ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima inayojitokeza mara kwa mara.

Naye Mwenyekiti wa Muungano huo, Christopher Mademula, alimweleza Naibu Waziri kuwa suala la kigezo cha elimu liangaliwe kwa mapana yake kwa kigezo kuwa ikiwa wagombea wa darasa la saba hawataruhusiwa kugombea nafasi za uongozi kwenye WMA, kitendo hicho kitachochea ujangili kwa kuwa wao wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa taarifa za kiintelijensia za ujangili kwenye maeneo yao.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa (kulia), akikagua mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), unaotekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), eneo la Njedegwa, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ujenzi ya TBA, Humphrey Killo. Habari Uk. 22. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kabudi aweka msimamo nchi kujiamulia mambo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesisitiza kuendeleza msimamo wa kutetea misingi ya taifa kwa kulinda uhuru wa kujiamulia mambo yake bila kuingiliwa na kutofungamana na upande wowote katika uhusiano wa nchi nyingine na jumuiya za kimataifa.

Amesema Tanzania kamwe haitaipigia magoti nchi yoyote kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka misingi iliyowekwa na waasisi wa taifa, akibainisha kuwa nchi ina akiba ya kutosha ya fedha na haijawahi kushindwa vita.

Vile vile, imesema itahakikisha taswira ya nchi inalindwa na haitosita kutoa ufafanuzi pindi shutuma ovu zinapotolewa dhidi ya nchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alipowasilisha hotuba kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Prof. Kabudi alilieleza Bunge kuwa Tanzania iliiarifu jumuiya ya kimataifa namna serikali inavyotimiza misingi ya haki za binaadamu kama ilivyobainishwa kwenye katiba na mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania ni mwanachama.

Alisema serikali itaendelea kuhakikisha taswira ya nchi inalindwa kila mahali pale shutuma dhidi ya nchi inapotolewa.

"Niendelee kuzisihi jumuiya za kimataifa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kushauriana na serikali pale ambapo wanahisi kuna tatizo kabla ya kutoa shutuma dhidi ya serikali," Prof. Kabudi alisema.

Aliongeza kuwa Tanzania inaongozwa kwa misingi ya kikatiba na kisheria ambayo lengo kuu ni kudumisha amani, ulinzi, usalama na mshikamano wa wananchi kama ilivyowekwa na waasisi wa taifa baada ya uhuru.

Waziri huyo alisema Tanzania inashirikiana na nchi wanachama wa nchi zisizofungamana na upande wowote (NAM), hususan nchi zinazoendelea kulinda na kutetea maslahi ya pamoja katika mijadala ya kimataifa.

Alisema katika kutekeleza azma hiyo, Tanzania ilishiriki kwenye Mkutano wa Mawaziri wa NAM mwaka 2018, uliofanyika Baku, Azerbaijan.

Prof. Kabudi pia alisema Tanzania inaheshimika kimataifa kutokana na juhudi zake za kupambana na rushwa, dawa za kulevya, utakatishaji fedha, kutetea masuala ya haki za binadamu na kuunga mkono misingi ya demokrasia na utawala bora.

Alibainisha kuwa msimamo wa Tanzania kuhusu mgogoro Israel na Palestina ni kuendelea kuzingatia msingi uliowekwa na waasisi wa taifa ambayo ndiyo nguzo ya sera ya mambo ya nje kupigania haki ya kujitawala, kuheshimu mipaka na kuunga mkono maazimio ya jumuiya ya kimataifa.

Alibainisha Tanzania inaunga mkono maazimio ya UN na Umoja wa Afrika (AU) kuhusu mgogoro huo na itaendelea kushauri pande husika kuheshimu makubaliano yaliyofikiwa. "Tanzania inaamini kwamba suluhisho la kudumu katika mgogoro huu ni kuwa na nchi mbili ambazo zitaishi kwa pamoja ikiwa ni Palestina huru na Israel salama," alisema.

Kuhusu mgogoro kati ya Morocco na Sahrawi katika eneo la Sahara Magharibi, alisema Tanzania inaunga mkono juhudi za UN na AU kwa pande zote kushiriki mazungumzo ya namna bora ya kutatua mgogoro huo.

Alisema katika mijadala hiyo, Tanzania imeendelea kuzisihi pande zote kukaa meza moja kupata suluhu ya kudumu.

"Tunapongeza mazungumzo yaliyofanyika Desemba mwaka jana Geneva nchini Uswisi kati ya pande mbili. Ni matumaini yetu kuwa suluhu ya mgogoro huo itapatikana mapema," alisema.

Waziri huyo pia alisema urejeshaji wa wakimbizi wa Burundi nchini mwao kwa hiari unafanyika kwa uweledi kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa na sheria za nchi.

Hata hivyo, alisema kuna watu wachache wenye nia ovu husussan watu wanaodai kuwa ni Warundi waishio kweye baadhi ya nchi za Ulaya, walianzisha kampeni chafu dhidi ya Tanzania kuwa inawalazimisha wakimbizi hao kurejea kwa nguvu. "Tuhuma hizo si za kweli na zinalenga kulichafua taifa letu kimataifa. Wizara kwa kutumia majukwaa ya kimataifa ilitoa ufafanuzi wa namna zoezi hilo linavyofanyika kwa hiari," alisema.

Ili kutelekeza majukumu yake, Prof. Kabudi aliliomba Bunge liidhinishe Sh. bilioni 166.9 kwa ajili ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

# Watu 2,830 waugua dengue

**Na Mary Geofrey**

UGONJWA wa homa ya dengue, umeendelea kushika kasi nchini hasa katika Jiji la Dar es Salaam, ambako watu 2,831 wamebainika kuugua katika kipindi cha miezi mitano.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akielezea hali ya ugonjwa huo juzi jijini Dar es Salaam, alisema idadi inazidi kuongezeka.

Alisema mbali na wagonjwa wa Dar es Salaam, wengine 118 wanatoka mkoa wa Tanga, 19 mkoani Pwani na mmoja Morogoro.

"Tunaendelea kutoa tahadhari kuhusiana na ugonjwa wa homa ya dengue, tayari wagonjwa 2,831 wamepatikana katika Jiji la Dar es Salaam na wawili wameshapoteza maisha nchi nzima," alisema Waziri Ummy.

Alisema idadi hiyo ni kubwa kulinganisha na wagonjwa ambao wamewahi kuugua homa hiyo nchini. "Mwaka huu idadi ya wagonjwa wenye homa ya dengue ni kubwa zaidi kuliko miaka mingine ya nyuma. Mwaka 2014 waliugua watu 400 tukadhani ni watu wengi zaidi, lakini idadi ya sasa ni kubwa zaidi," alisema Ummy.

Kutokana na kukithiri kwa wagonjwa wa homa hiyo, idadi ya vituo vinavyopima ugonjwa huo viliongezwa hadi kufikia 19 tofauti na vituo saba vilivyokuwapo awali ili kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma.

Vituo vinavyopima homa hiyo kwa gharama ya Sh. 15,00 ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Maabara Kuu Muhimbili, Amana, Temeke, Mwananyamala, Sinza, Vijibweni, Mnazi Mmoja, Lugalo, Mbagala na FFU Ukonga jijini Dar es Salaam.

DENGUE NI NINI?

Homa ya dengue ni ugonjwa wa kitropiki unaosababishwa na virusi vya dengue maarufu kama dengue.

Homa ya dengue pia hujulikana kama, homa ya kuvunja mifupa kwa sababu inaweza kuwafanya watu wawe na maumivu makali hadi wahisi kama mifupa yao inavunjika.

Dalili za ugonjwa huu huanza siku tatu hadi kumi na nne baada ya kuambukizwa.

Baadhi ya dalili ni homa kali, kuumwa na kichwa, kuota vipele kwenye ngozi na maumivu kwenye misuli na maungio.

Kwa watu wachache, homa ya dengue inaweza kubadilika na kuwa aina zinazohatarisha maisha.

Dalili kubwa ni ile ya kuvuja damu, ambayo huifanya mishipa ya damu inayobeba damu.

Kwa kawaida matibabu huchukua siku tatu hadi saba hadi mgonjwa kupona na hakuna dawa ya chanjo inayofanya kazi kuwakinga watu dhidi ya virusi vya dengue.

# Elimu ya mpigakura kuanza Julai

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalotoa elimu ya demokrasia, utawala bora, uraia na upigaji kura kwa vijana na wanawake Tanzania (Tafeyoco), linatarajia kuanza kutoa elimu hiyo nchi nzima kuanzia Julai mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Elvice Makumbo, alisema hayo alipokuwa akizungumza katika ofisi za gazeti hili Mikocheni, jijini Dar es Salaam, jana na kufafanua kuwa kazi itaendelea hadi 2020.

"Sisi ni miongoni mwa mashirika 24 yaliyochaguliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutoa elimu hiyo kwa ajili ya kuandaa Watanzania kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020," alisema Makumbo. Makumbo alisema wataanzia elimu hiyo katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam na wataendelea kwenye maeneo mengine ili kuhakikisha wanafikia katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

"Elimu hii ni msingi sana kwa kila Mtanzania na hasa vijana na wanawake, ambao kimsingi, ndio wapigakura wakubwa, hivyo tunapojiandaa kuwafikia, basi wawe tayari kutoa ushirikiano ili kufanikisha kazi hii," alisema.

Alisema shirika hilo linaendelea na mchakato wa kusajili vijana 300 watakaopewa semina kisha watashiriki katika utoaji wa elimu ya mpigakura kwenye maeneo watakayopangiwa.

Aidha, Makumbo alisema, mbali na kutoa elimu, wao ni waangalizi huru wa ndani kupitia NEC na wamekuwa wakishiriki kikamilifu kwenye jukumu hilo ili kuhakikisha kila uchaguzi unafanyika kwa uhuru na haki. "Watanzania bado wanahitaji elimu ya uraia, ili waweze kutambua haki zao, ndio maana tunawajulisha ili wajiandae kujitokeza kwa wingi tutakapoanza kazi ya kutoa elimu," alisema.



Balozi wa Kenya nchini, Dan Kazungu, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uandikishaji wa wapigakura kwa lengo la kuhakikisha raia wa Kenya wanaoishi nchi za nje wanapiga kura kupitia balozi zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makonda aandaa futari kumuenzi Mengi

**INATOKA UK. 2**

Mtangazaji wa Clouds na Mmiliki wa Blog ya Millard Ayo, Millard Ayo na mchekeshaji Emmanuel Mgaya, maarufu kama Masanja Mkandamizaji.

Makonda alisema watu hao mashuhuru wataketi kila meza ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuwahudumia, lakini pia kubadilishana nao mawazo.

Alisema wageni hao waalikwa pia watafika na zawadi ambazo wamewaandalia watu wenye ulemavu na kuwapatia.

"Lengo ni kuona ule upendo, umoja na moyo aliotuonyesha marehemu Dk. Mengi wa kupendana bila kubaguana, tuuonyeshe kwao tena bila kutegemea fadhila kutoka kwao hii ni kama sehemu ya kumuenzi Dk. Mengi," alisema Makonda.

Makonda alisema pia maandalizi yanaenda vizuri na futari itakayotolewa ni ya viwango vya juu pamoja na vinywaji vya baridi vya aina mbalimbali vitatolewa.

Makonda alisema pamoja na kumuenzi Dk. Mengi, anatarajia kuona baada ya futari hiyo upendo na mshikamano utaendelea kudumu katika mkoa huo.

Alisema wakazi wa jiji hilo wanapaswa kujitoa na kusaidia wengine bila kutarajia kupata fadhila kutoka kwa waliowasaidia. Pia aliwataka wenye viwanda na kampuni zinazotoa ajira nchini kutoa ajira kwa watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria.

Alisema kama sheria ya ajira itafuatwa, watu wenye ulemavu wengi watapata ajira na hivyo kupunguza utegemezi hasa kwa wale wenye elimu.

Kila mwaka Dk. Reginald Mengi alijiwekea utaratibu kuandaa chakula cha mchana na kula na watu wenye ulemavu nchini.

Dk. Mengi ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Dk. Reginald Mengi Persons with Disabilities Foundation , Februari mwaka huu, alishiriki chakula cha mchana na kutoa tuzo za I Can, kwa watu wenye ulemavu.

Dk. Mengi alifariki dunia Mei 2, mwaka huu, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuzikwa Machame, Kilimanjaro.

# DECI hatimaye yakata rufani

**INATOKA UK. 5**

kwenye nyumba hizo kuwa za serikali.

Alisema mali zisizohamishika ikiwamo nyumba zibadilishwe majina ya umiliki kutoka DECI kuwa kwa jina la Msajili wa Hazina.

Akifafanua hukumu hiyo jaji, alisema akaunti za kampuni hiyo zilizoko Benki ya NMB tawi la Msasani, DCB tawi la Uhuru na KCB tawi la Samora wahamishe Sh. bilioni 14.3 kutoka kwenye matawi yao kwenda serikalini mara watakapopokea amri ya mahakama yake.

"DPP katika maombi yake amewasilisha vielelezo kuthibisha kwamba mali zote zilipatikana kwa fedha za upatu, zilizopatikana kwa njia isiyo halali, lakini walalamikiwa hawajawasilisha majibu yoyote yanayopinga maombi hayo au kufafanua upatikanaji wa mali hizo tofauti na vielelezo vya mlalamikaji, mahakama yangu inaamuru mali zote zitaifishwe kuwa mali za serikali," alisema Jaji Magoiga.

Alisema DPP aliwasilisha maombi akitaka kutaifisha mali hizo kuwa za serikali baada ya kubainika kuwa zimepatikana isivyo halali na kwamba ni fedha chafu.

Hata hivyo, walalamikiwa hawajawasilisha utetezi kuonyesha kwamba walikuwa na biashara nyingine zaidi ya upatu.

Jaji aliendelea kuichambua hukumu kwamba walalamikaji wameshindwa kujitetea kwamba fedha na mali zote hazihusiani na upatu uliotokana na makusanyo kutoka kwa wananchi bila kuwa na leseni ya kufanya hivyo.

Alisema lengo la DPP si kuitajirisha serikali bali ni kuwataka watu wafuate taratibu na sheria kuendesha shughuli zao.

Maombi hayo namba 42/2019 yalifunguliwa na DPP Biswalo Mganga dhidi ya wakurugenzi wa DECI.

Hata hivyo, DECI haijaridhishwa na uamuzi huo, hivyo imewasilisha kusudio la kukata rufani Mahakama ya Rufani kupitia wakili wao Magafu.

Mapema, mahakamani hapo Magafu akijibu hoja za mlalamikaji alidai kuwa akaunti zilizowasilishwa na DPP, kati ya hizo moja inamilikiwa na kanisa na ya pili inamilikiwa na mlalamikiwa wa kwanza.

Hata hivyo, hati ya kiapo iliyowasilishwa na DPP hakuna mahali inaonyesha ushahidi kwamba mali zote zimetokana na fedha za ujanjaujanja.

Jopo la mlalamikaji liliongozwa na DPP Biswalo Mganga akisaidiana na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, Mawakili wa Serikali Waandamizi, Theophil Mutakyawa na Shadrack Kimaro.

Akijibu hoja za walalamikiwa, DPP alidai kuwa walalamikaji walikuwa wanaendesha mchezo wa upatu kinyume cha sheria na kwamba mali zote ni mali za DECI zinafaa kutaifishwa.

## HABARI KITAIFA

# Afungwa miaka 120 kuhujumu miundombinu

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma mkoani hapa, imemhukumu mkazi wa Kitongoji cha Kilelema A katika Kijiji cha Kazuramimba Wilaya ya Uvinza, Tazani Sadiki (52), kutumikia kifungo cha miaka 120 kwa makosa sita ya uharibifu wa miundombinu ya huduma kwa jamii.

Makosa hayo ni pamoja na kuwaunganishia umeme watu watano kinyume cha taratibu pamoja na kukutwa na vifaa ambavyo ni mali ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco). Vifaa hivyo ni kofia ngumu moja, waya na fomu za maombi ya umeme Tanesco 42, nyumbani kwake kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kenneth Mutembei, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo bila ya kuacha shaka.

Hakimu Mutembei alisema Mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi 11 na vielelezo 3 ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo.

Aidha, hakimu huyo alisema mshtakiwa huyo alijifanya wakala wa Tanesco na kuanza kuwaunganishia umeme watu watano ambao ni Hatibu Hamis, Gerald Silivery, Exaver Lucas, Ramadhani Iddi na Maulidi Zuberi na wakati akijua si mfanyakazi wa Tanesco.

Alisema mshtakiwa alijipatia fedha kutoka kwa watu hao, huku akijua kabisa si mfanyakazi wa Tanesco.

Alisema Mahakama imeangalia kwa makini na kugundua kuwa aliwafungia umeme watu watano. Pia askari polisi walipomfanyia upekuzi nyumbani kwake walikuta kofia ngumu moja, waya za umeme na fomu za maombi ya kuomba umeme Tanesco.

Alisema mshtakiwa alishindwa kukanusha ushahidi wa watu watano aliowaunganishia umeme, hivyo kumtia hatiani kwa makosa yote sita.

Mshtakiwa huyo alijitetea kuwa anaomba mahakama impunguzie adhabu kwa sababu ana familia kubwa kisha kuangua kilio.

Hakimu Mtembei alitupilia mbali utetezi huo na kusema makosa yako ni ya uhujumu uchumi na kuamuru aende jela miaka 120, lakini atatumikia miaka 20 kwa sababu kila kosa kifungo chake ni miaka 20.

Awali akisoma hati ya Mashtaka Wakili wa Serikali, Benedict Kivuma, alidai kuwa tarehe isiyofahamika Desemba mwaka 2017, katika Kitongoji cha Kilelema A katika Kijiji cha Kazuramimba Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma, mshtakiwa alijifanya fundi wa Tanesco kwa kushirikiana na wenzake aliwaunganishia umeme kinyume cha taratibu watu watano pamoja na kukutwa na vifaa vya Tanesco kinyume cha sheria.



Spika wa Bunge Job Ndugai (wa pili kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, katika hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo, kwa ajilli ya wateja na wadau wake, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Katibu wa Bunge, Steven Kagaigai na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Ally Laay. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Shule Dar yasaidiwa kuepuka kipindupindu

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu yanayotokana na kunywa maji yasiyo salama, Klabu ya Rotary Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, imetoa msaada wa vichujio (water filters) kwa Shule ya Msingi Mbezi Beach.

Rais wa Rotary Club Mbezi Beach, Guru Sykes, akikabidhi msaada huo jijini Dar es Salaam, alisema vichujio hivyo vitasaidia wanafunzi wote kunywa majisafi na salama na kuepuka hatari ya kupata magonjwa.

Alisema msaada huo ni sehemu ya jitihada za kuendeleza elimu nchini kwa kuwa elimu ni eneo mojawapo wanalolifanyia kazi.

"Tumeamua kushirikisha baraka zetu kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mbezi Beach ili kuwasaidia kufanya vizuri kwenye masomo yao na kuwa na afya bora," alisema Sykes.

Alisema malengo yao ni kuboresha uwanja wa michezo pamoja na kutoa vifaa vya michezo shuleni kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kuwa na muda wa michezo ili kujenga afya zao na kuwa bora kwenye masomo yao.

"Pia tunajipanga kuanzisha kambi ya kupima malaria bure kwa kushirikiana na shule na wadau wengine pia," alisema Sykes.

Awali akielezea vifaa hivyo, Meneja wa Rotary, Fatma Mahsen, alisema vifaa hivyo vina uwezo wa kuchuja na kuondoa bakteria wote kwa asilimia 100 kwenye maji.

"Kifaa hiki pia kina uwezo wa kudumu kuchuja maji lita 100,000 na kinadumu kwa miaka mitatu, baada ya hapo kinaisha uwezo wake wa kuchuja na kutoa maji masafi," alisema Mahsen.

Aidha, alisema kifaa hicho kimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ubora na ufanisi wake.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Prisca Haule, aliishukuru Rotary na kwamba itasaidia wanafunzi wote kupata majisafi na salama na kuepuka hatari ya magonjwa.

# Mzee wa Upako aeleza mazito uchaguzi wa mitaa

**Na Mary Geofrey**

ASKOFU wa Kanisa la Maombezi la Gospel Revival Center (GRC), Ubungo - Kibangu, Antony Lusekelo, maarufu Mzee wa Upako, amesema serikali haina haja ya kufanya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na kudai ni matumizi mabaya ya muda na fedha.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu maendeleo ya nchini na juhudi zinazofanywa na Rais John Magufuli.

"Tungeacha nchi itulie, tufanye kazi, ningekuwa mimi, kama ambavyo Bwana mkubwa (Rais Magufuli) amekuwa akifuta sherehe mbalimbali za serikali, uchaguzi huu ningeufuta na ninaomba waufute, hauna tija kwa nchi yetu," alisema.

Alipendekeza kuwa uchaguzi ungefanyika kwa wakati mmoja badala ya kuanza kufanya uchaguzi kwa miaka miwili mfululizo, kunasababisha shughuli za maendeleo kukwama. Alisema angepata fursa ya kumshauri Rais Magufuli, angemshauri kufuta uchaguzi huo na viongozi waliopo waendelee na shughuli zao hadi hapo utakapotangazwa uchaguzi mkuu ujao.

"Uchaguzi ufanyike mara moja, ikifika mwakani uanze uchaguzi wa serikali za mitaa, madiwani, wabunge na Rais ili tuache shughuli za maendeleo zifanyike," alisema Askofu Lusekelo.

Alimshauri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaan (Tamisemi), Selemani Jafo, kumshauri Rais Magufuli afute uchaguzi huo na badala yake ufanyike mwakani na viongozi waliopo madarakani waendelee kutekeleza majukumu yao.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kumuunga mkono Rais Magufuli katika utekelezaji wa majukumu yake hasa kukuza uchumi wa taifa.

Alisema amefanya kazi nyingi, hivyo anapaswa kupewa muda wa kuendelea kuzifanikisha katika kipindi chake za uongozi.

"Sisemi haya kwa sababu najipendekeza... sina shida na ukuu wa wilaya wala kitu kingine, ninayoyasema mtakuja kuyakumbuka miaka ijayo," alisema Askofu Lusekelo.

Alisema anayoyafanya yataonekana yana manufaa kwa taifa miaka ijayo. "Mimi leo na wengine tukipata nafasi tuseme asante Mungu kwa kupata kiongozi, kwa kumpata kiongozi ambaye anajali wananchi wake. Msipotambua anayoyafanya Magufuli leo, mtakuja kuyatambua miaka mingi ijayo," alisema.

Alisema kwa tathmini yake, miongoni mwa nchi zitakazokuwa na maisha mazuri miaka mingi ijayo, Tanzania ni miongoni.

Askofu Lusekelo, alisema haungi mkono wanasiasa wanaohama vyama kwa sababu yoyote ile kwa sababu ni kuwapotezea muda Watanzania.

Alisema watu wa aina hiyo, hawana misimamo na wanadhihirisha uongo wao kwa madai ya kuhama vyama.

"Mimi nina kawaida ya kutopenda mtu muongo, kiongozi anayehama chama anakuwa ni muongo, aliahidi kukitumikia chama fulani ghafla anatangaza kuhama, watu wa namna hii siwaungi mkono hata kidogo," alisema Askofu huyo.

Kuhusu matukio ya ulawiti, ubakaji, Lusekelo alisema kushamiri kwa matukio hayo kunatokana na wingi wa vyombo vya habari ambavyo vinaripoti tofauti na miaka ya nyuma.

Alisema miaka ya nyuma vyombo vya habari vilikuwa vichache na kwamba pia sababu ni misingi mibovu ya malezi kuanzia ngazi za familia.

"Nachukizwa sana na mwanaume ambao anatoboa masikio, anavaa heleni, anasuka nywele, eti hawezi kuwa msanii bila kufanya hivyo. Nani kakwambia, enzi zetu wazazi na familia zilikuwa haziruhusu kufanya mambo hayo na mzazi wa mtoto alikuwa anatengwa na mtaa," alisema kiongozi hiyo wa kanisa.

Kadhalika, Askofu Lusekelo alisema anasikitishwa na watu ambao wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii kuchafua watu na serikali ikiendelea kuwafumbia macho.

# Maeneo ya mabondeni kutorasimiwa

BUNGE limeelezwa kuwa serikali hairuhusu na haitarasimisha makazi yaliyojengwa maeneo hatarishi ikiwamo mabondeni.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Zainab Amiri.

Katika swali lake, Mbunge alisema kuna baadhi ya watu wanajenga kwenye mabonde, wengine jirani na hifadhi ya barabara na reli, lakini serikali hukusanya kodi za maeneo na majengo katika maeneo hayo.

"Je, serikali inaeleza nini kuhusu kadhia hii? Ili mwananchi ajenge mahali husika lazima apate kibali, je, nini adhabu ambayo wanapewa wanaotoa vibali kwenye maeneo hatarishi?" Alihoji.

Lukuvi alisema utoaji wa leseni za makazi hautafanyika kwa watu waliojenga maeneo hatarishi.

"Ni kweli kuna watu wanajenga kwenye hifadhi za barabara na hifadhi za miundombinu mingine na mabondeni, lakini wamefanya hivyo kinyume cha sheria, serikali hairuhusu na hata zoezi la urasimishaji na utoaji wa leseni za makazi," alisema.

Alisema wapo watu ambao wamejenga kwenye maeneo hayo, hivyo sheria itachukua mkondo wake.

"Ni kweli kodi inakusanywa kwa sababu bado wanatumia rasilimali zilizopo lazima wachangie, lakini ujenzi katika maeneo hayo hauruhusiwi," alisema.

Alisema kodi za majengo zitatozwa na kodi wanazotozwa raia wengine zitatozwa, lakini haitahalalisha wao kuwa wamekaa kwenye maeneo hayo kihalali.

"Lolote linaweza kutokea kama wapangaji na halmashauri husika wakiamua kuchukua hatua. Vibali vya ujenzi vinatolewa na timu ya wataalamu ya ujenzi na havichukui zaidi ya siku tatu na vinatolewa kwa kasi," alieleza.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kuwapatia wananchi wa Tanznaia elimu stahiki, ili waepukane na ujenzi ambao hauzingatii mipango miji.

Lukuvi alisema serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuwaelimisha wananchi kuhusu ujenzi unaozingatia mipango miji, ili kuepuka madhara mbalimbali ikiwamo kubomolewa nyumba zao bila kulipwa fidia.

Alitaja mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa njia ya vyombo vya habari kama vile redio, runinga, magazeti, vipeperushi, machapisho mbalimbali, mitandao ya kijamii pamoja na tovuti ya wizara.

"Serikali inaendelea kusisitiza kuwa wananchi wazingatie sheria na taratibu za uendelezaji miji ili kujiepusha na ujenzi holela," alisisitiza.

Aidha, aliwataka wananchi waepuke kujenga mijini bila kuwa na vibali vya ujenzi ili kuepuka kubomolewa nyumba zao bila kulipwa fidia.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Laikala wilayani Kogwa, mKoa wa Dodoma walipotembelea Bunge jana, kwa lengo la kujifunza. **PICHA: BUNGE**

## Nape ahoji safari ATCL

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imekiri kuwa kwa siku za hivi karibuni kumetokea ucheleweaji wa ndege za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutokana na sababu mbalimbali za kiufundi ambazo zimesharekebishwa.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Atashasta Nditiye, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, ambaye alisema pamoja na mipango ya serikali ya kuboresha Shirika la Ndege, sasa kumeanza kujitokeza tabia ya ucheleweshaji wa ndege jambo ambalo linakera sana.

"Chanzo cha tatizo hili ni nini na serikali mmechukua hatua gani kurekebisha?" Alihoji.

Nditiye alisema serikali ilishatoa maelekezo kwa ATCL kwamba kama kutakuwa na ucheleweshaji wa nusu saa basi itolewe taarifa ya maandishi ya sababu zilizosababisha ndege kuchelewa.

"Hilo limeanza kufanyika na tumeanza kupata taarifa, tunawasisitiza ATCL kuwa wateja ndio watu wa thamani sana kwa hiyo delay ambazo hazina sababu za msingi ziepushwe sana," alisema.

Nditiye alisema marekebisho yalishafanyika na ATCL inaenda vizuri na ucheleweshaji pamoja na kusitisha safari bila sababu za msingi hazijitokezi tena. Katika swali la msingi, Mbunge wa Shaurimoyo (CCM), Mattar Ali Salum, alisema kampuni ya Azam Marine ambayo inafanya biashara ya kusafirisha abiria kwa kutumia boti kupitia baharini, huuza tiketi kwa abiria kwa ajili ya safari, lakini abiria anapochelewa safari tiketi hiyo huwa haitumiki, hivyo kusababisha hasara kwa abiria pamoja na usumbufu.

Alihoji serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hilo.

Nditiye alisema serikali ina taarifa ya jambo hilo kwa kuwa limekuwa likijitokeza mara kwa mara, na ufuatiliaji uliofanywa na wizara yake kupitia Tasac umebaini kampuni iliyotajwa ina utaratibu wa namna abiria anavyoweza kuahirisha safari na namna nauli itakavyorejeshwa.

# Waziri afafanua mradi maji wa Mto Ruvuma

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amehoji kuhusu marekebisho ya mchoro wa mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma hadi Mtwara, ili vijiji vya Halmashauri ya Nanyamba viweze kupata maji.

Akiuliza swali, Mbunge huyo alihoji ni vijiji vingapi vya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba vitanufaika na mradi huo na lini utaanza kutekelezwa.

"Kwa kuwa marekebisho yatafanyika mara baada ya mtaalamu mshauri kupatikana, serikali ipo tayari kutoa maelekezo kwa mtaalamu mshauri ili kuingiza vijiji 20 kwenye mradi huu?" Alihoji.

Alihoji pia serikali haioni kuwa ni wakati wa kutekeleza mradi huo kwa kutumia fedha za ndani.

Akijibu, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alikiri kuwa serikali ilikubali kufanya marekebisho ya mchoro wa mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwenye Manispaa ya Mtwara, ili kuongeza idadi ya vijiji zaidi vikiwamo vya Halmashauri ya Nanyamba.

Aidha, alisema usanifu wa mradi huo ulishakamilika, hivyo mabadiliko ya mchoro yatafanyika wakati wa utekelezaji wa mradi huo kabla ya kuanza ujenzi.

"Idadi ya vijiji vitakavyoongezeka vitajulikana baada ya mabadiliko ya mchoro yatakayofanywa na mtaalamu mshauri atakayesimamia utekelezaji wa mradi," alisema.

Alisema ujenzi wa mradi huo unakadiriwa kugharimu kiasi cha Dola za Marekani milioni 189.9 na serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo unategemea upatikanaji wa fedha hizo.


Alifafanua kuwa wizara imewekwa mwongozo kuwa vijiji vyote vilivyopo kwenye vyanzo vya maji ndio vya kwanza kupata huduma ya maji na vijiji vitakavyokuwa pembeni mwa bomba la maji kwa umbali wa kilomita 12 vitapatiwa huduma hiyo.

"Vijiji alivyosema mbunge tuna mpango wa kupeleka maji vijiji kama Maembe Chini na Juu, Kirombo Juu na Chini, Mchanje na Mji Mwema pamoja na vingine 14 vitapata huduma ya majisafi na salama," alisema.

Kuhusu kutumia fedha za ndani, Mbarawa alisema mradi huo unagharimu takribani Sh. bilioni 400 na bajeti ya wizara ni Sh. bilioni 673, hivyo kama ikitumia fedha hizo kutekeleza mradi huo miradi mingine ya maji haitatekelezwa.

Alisema wizara hiyo itahakikisha inatafuta fedha nyingine kwa ajili ya kazi ya kutekeleza mradi huo wa Mto Ruvuma na ukamilike kwa wakati.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia, alisema ilionekana mradi huo haupo kwenye mipango ya wizara. Prof. Mbarawa alisema mradi huo ulipangwa na serikali na utatekelezwa.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA



Walimu wa mafunzo kwa vitendo wanaotoka Chuo Kikuu cha Fachakademien nchini Ujerumani, wakiwa katika ziara ya kutembelea Shule ya Tarangire Pre & Primary English Medium ya mjini Babati, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wafanyabiashara wa maziwa waomba kupunguziwa kodi

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

BAADHI ya wafanyabiashara wa maziwa wameiomba serikali kupunguza kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa katika bidhaa hizo, ili kuwezesha wananchi wa kawaida kufungua viwanda vya kusindika maziwa katika maeneo mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini Arusha katika Maadhimisho ya Wiki ya Unywaji Maziwa Duniani ambayo kitaifa inafanyika mkoani hapa, Meneja wa Mauzo wa Kampuni ya Cowbell, Vitus Mpanda, alisema utitiri wa kodi ni kikwazo.

Aliongeza kuwa kodi nyingi zilizopo kwenye uwekezaji wa maziwa nchini zinawanyima wafanyabiashara wengi fursa ya kufungua viwanda vya maziwa.

Alieleza kuwa gharama za uendeshaji zimekuwa kubwa katika biashara hiyo, kwani tozo ni nyingi sana hali inayosababisha baadhi ya viwanda vya maziwa kufungwa.

Aidha, aliomba serikali kuunganisha kodi ya Shirika la Viwango (TBS) pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), kwani vitengo hivyo vinafanana na tozo zake ni kubwa pia mpaka upate vibali vyake ni mchakato unaokatisha tamaa.

"Gharama za kusindika maziwa nchini ni kubwa mno kuliko majirani zetu, wanasindika kwa bei ya chini, hivyo mtu anaona bora akasindike nje aje kuuza huku," alisema Isaya Mbindi mmoja wa wafugaji.

Isaya alisema kuwa mbali na hapo wafugaji wengi wanapenda kufuga, lakini kutokana na gharama za ufugaji zilivyo juu wanashindwa kuendeleza ufugaji.

Alisema kuwa mbali na gharama kubwa pia aliomba serikali kuwapatia elimu zaidi wafugaji, ili waweze kufuga kisasa na kufanya ufugaji bora na kupata mazao bora.

# Wanasheria wa Afrika kuzibana serikali zao

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA cha Wanasheria wa Afrika (Palu) kwa kushirikiana na taasisi ya kusimamia matumizi ya Kidijitali Duniani, kinakusudia kuziandikia nchi zao na kuziomba kurekebisha upungufu mwingi ulio kwenye sheria za kidijitali.

Palu imeeleza kuwa kuna upungufu katika sheria hizo, hivyo wameamua kujadiliana na kuandaa mapendekezo watakayopeleka katika serikali za nchi zao zikiwamo za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Palu pamoja na wadau wengine wanakutana Arusha kujadili na kuweka mikakati ya kusimamia haki za watumiaji wa mitandao ya teknolojia ya kidijitali, ili kuwezesha wananchi kupata huduma.

Akizungumza jana jijiji Arusha wakati wa kongamano la wiki moja linalohusu haki za mawasiliano ya kidijitali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Palu, Donald Deya, alisema kuwa, binadamu wana haki ya kupata mawasiliano ya kidijitali ili kuendesha shughuli zao.

Akitaja baadhi ya upungufu uliopo katika nchi hizo alisema ni baadhi ya kampuni zilizopewa leseni za kutoa mawasiliano kupuuza sheria ikiwa ni pamoja na kutofikisha mawasiliano vijijini.

"Mawasiliano ni muhimu kwa wakati kama huu wa sasa kwa sababu mitandao inatumika katika kufanya biashara, kutoa elimu na kutibu, lakini bado baadhi ya kampuni hazitoi huduma stahili ya internet na simu kama inavyotakiwa," alisema Deya.

Alisema lakini pamoja na haki hizo bado zipo baadhi ya serikali katika nchi hizo zinakiuka haki za binadamu za uhuru wa kupata huduma hiyo kwa kufunga mitandao ya kijamii wakihofia kukashifiwa jambo ambalo si sahihi na ukiukwaji wa haki hizo.

Deya alishauri badala ya serikali kukimbilia kufunga mitandao hiyo, wangeachia bunge lipitishe sheria nzuri za kusimamaia suala hilo na huku mahakama zikihakikisha zinapewa nafasi za kuhakikisha sheria hizo zinasimamiwa na anayekiuka anaadhibiwa. "Kwani kweli hata serikali inatumia mitandao hii kufanikisha kukamata wahalifu wa makosa mbalimbali, hivyo vema kila upande ukaheshimu haki ya wengine na sio kukimbilia kuzuia wngine wasipate haki ya huduma hiyo," alisema.

Alisema katika kongamano hilo wanakutana wanasheria na wanaharakati kutoka nchi za EAC, maofisa wa haki za binadamu na Tume ya Umoja wa Afrika ya Kupambana na Rushwa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Kijamii.

Ofisa Mipango wa Kidijitali wa Taasisi Inayosimamia Matumizi ya Kidijitali Duniani ijulikanayo kama Article 19 Ephraim Kenyanito, alishauri ziwepo sheria zitakazosimamia mawasiliano kwa haraka, "Hadi sasa hatuwezi kuzifikia nchi zilizoendelea katika matumizi ya kidijitali ni vema EAC tukafanya jitihada kuweka mipango madhubuti ya kusimamia hili na kusambaza huduma kwa wote hasa vijijini," alisema.

# Wapewa somo kuepuka kubambikiwa bili za maji

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati (Bawasa), imewataka wateja kutumia mfumo mpya wa malipo kuepuka bili feki.

Wameshauriwa kutumia mfumo huo wa ulipaji wa bili maarufu kama GEPG, ili kuwaepusha na usumbufu ukiwamo kubambikiwa malipo.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Kaimu Meneja Biashara na Mkuu wa Kitengo cha Tehama wa Bawasa Rashid Charahani, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mfumo mpya wa ulipaji Ankara za maji.

Charahani aliiambia Nipashe iliyotaka kujua namna mfumo mpya wa GEPG unavyofanya kazi. Alisema Bawasa imeanza kuutumia tangu Mei 20, 2019 na kwamba unaungwa na benki na mitandao ya simu.

Alisema wameamua kutumia mfumo wa GEPG kukusanyia fedha zote za umma kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya fedha ya mwaka 2001 kupitia marekebisho ya mwaka 2017.

"Waraka wa Hazina namba 3 wa Septemba 4, 2017 pamoja na maelekezo ya serikali ni kwamba taasisi zote za umma zinatakiwa kujiunga katika mfumo huu ifikapo Juni 30, 2019," alisema.

Aidha, alisema taasisi iliyounganishwa na mfumo wa GEPG ni lazima ihakikishe kuwa Ankara inayotoka kwenye mfumo huo na kwenda kwa mteja au mlipaji inakuwa na taarifa za kile kilichopo ndani ya bili.

Aidha, iwe na kumbukumbu ya malipo (control number) rejea ya malipo, namba ya taasisi inayotoa huduma, jina la mlipaji, namba ya simu ya mlipaji na maelezo ya bili.

Taarifa nyingine ni aina ya huduma zinazolipiwa, kiasi kinachodaiwa kwa tarakimu, kiasi kinachodaiwa kwa maneno, tarehe ya Ankara kuchapishwa, ya Ankara kumalizika muda wake, jina la mtoa ankara na saini ya mtoaji.

Mtaalamu huyo wa Tehama wa Bawasa aliwataka wateja wao wanapolipa bili za maji kwa njia ya simu kutumia namba ya usajili kwenye mfumo wa malipo ya serikali, ambapo namba za usajili zinakuwa 12 ila tarakimu tano za kwanza zinaelezea mfumo pamoja na taasisi husika.

Kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo kwenye mfumo huo alisema, wakati wa utengenezaji wa bili inawalazimu kutumia muda mrefu kutengeneza namba ya malipo na fedha ikwisha kusanywa ina mzunguko mpaka kurudi kwa ajili ya matumizi.

Charahani aliongeza kuwa kuanzishwa kwa mfumo huu kumeongeza mwitikio wa kulipa bili, huku akisema ndani ya wiki moja ya kwanza baada ya kutoa bili kwa mfumo wa zamani walikuwa wanakusanya asilimia 40, lakini kwa mfumo huo wanaweza kukusanya kwa kipindi kama hicho hadi asilimia 60.





# Tanesco yanasa waliolihujumu shirika milioni 374/-

**Na Paul William,** MOSHI

SHIRIKA la Umeme - Tanesco mkoani Kilimanjaro, limekamata wateja zaidi ya 226 wanaodaiwa kuhujumu shirika hilo kwa madai ya kuliibia umeme.

Kufuatia hatua hilo Tanesco imeokoa zaidi ya Sh. milioni 374.59 baada ya kuwanasa wateja wasio waaminifu waliokuwa wakichakachua nishati hiyo na kuwatoza faini na kuwalipisha gharama walizotumia bila kulipia.

Taarifa ya mhandisi mdhibiti upotevu wa mapato wa Tanesco, Mussa Ngombole, ilieeleza kuwa kundi hilo linahusisha wateja wakubwa wa umeme.

Kwa mujibu wa Ngombole operesheni iliyofanyika kati ya kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, jumla ya wateja 226 walikamatwa kwa makosa ya kulihujumu shirika hilo. Alisema kuwa katika wateja hao waliokamatwa, sita ni wakubwa ambao ni watumiaji wa viwandani, hoteli na nyumba za kulala wageni, huku wateja 220 wakiwa ni wateja wa majumbani.

"Tumekuwa tukifanya operesheni za mara kwa mara kuwatembelea wateja wetu kwa kushtukiza, ambapo zoezi hilo lilizaa matunda baada ya kuwakamata wateja wasio wazalendo na nchi yao ambao wamekuwa wakitumia umeme wa wizi," alisema Mhandisi Ngombole.

Alisema kutokana na wateja hao kukamatwa kiasi cha Sh. milioni 374.59 kimeokolewa, ambapo ni fedha zinazotakiwa kulipwa na wateja hao pamoja na faini, huku akieleza kuwa hadi kufikia Aprili 30 mwaka huu jumla ya Sh. milioni 167.25 zimeshalipwa.

Mhandisi huyo alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo wakati wa kufanya operesheni hiyo ni baadhi ya wateja kutoa vitisho kwao wanaokwenda kufanya ukaguzi nyakati za usiku.

Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, Mhawa Mkaka, alisema kazi ya kuwatembelea wateja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ni endelevu na kuwataka wateja wote kuwa wazalendo na shirika lao.

Mhandisi Mkaka alizitaja wilaya zinazoongozwa kwa matukio ya wizi wa umeme kuwa ni Moshi na Same, huku pia akitaja madhara yanayoweza kutokea kutokana na wizi huo kiusalama ni mdogo kwa kuwa inaweza kupelekea nyumba kuungua na moto au kusababisha vifo vya watu. "Nitoe wito kwa wateja wote kutumia umeme kihalali na kuacha kulihujumu shirika na wezi wote watakaokamatwa watatozwa faini pamoja na gharama za matumizi ya umeme walioutumia pasipo kulipia," alisema Mkaka.

Meneja huyo alitoa wito kwa wasamaria wema mkoani Kilimanjaro kuendelea kutoa taarifa za kuwafichua wale wote wanaolihujumu shirika hilo na kwamba taarifa hizo zitaendelea kuwa siri, pia zawadi zitatolewa kwa watoa taarifa sahihi.



Meneja wa Benki ya NMB tawi la Kilindi, Godwin Manimo, akitoa elimu kwa wateja waliotembelea banda la NMB wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya "Muhogo kwa Maisha" iliyofanyika wilayani Kilindi Mkoa wa Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mghwira ataka kuwakumbuka wenye ulemavu wa ubongo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mgwhira, amesema anaumizwa kuona kundi la watoto wenye matatizo ya mtindio wa ubongo, wanasahaulika.

Aidha, alieleza kuwa kinachomsikitisha ni kwamba hawakumbukwi na huachwa kwa makusudi na makundi mengine ya walemavu, wakati wa utoaji wa misaada ya kibinadamu.

Matatizo ya mtindio wa ubongo yanatokana na au kusababishwa na vinasaba au jeni (genetic), au huletwa na dawa alizotumia mama wakati wa ujauzito, matumizi ya mihadarati, pombe, hali ya hewa, mionzi au ajali, kwa mujibu wa taarifa za kiafya kwenye mitandao.

Dk. Mghwira alieleza masikitiko yake hayo mbele ya wadau mbalimbali na viongozi wa serikali, wakati alipowaita wenye ulemavu huo kushiriki futari jana mjini hapa.

Alisema kutoonekana kundi hilo na kutotambuliwa mara kwa mara na wadau wanaotoa misaada ya kibinadamu kwa walemavu, kumemsukuma kuwataka wenye uwezo wa kifedha kuwatazama wahitaji hao ambao wanaishi katika mazingira magumu.

"Nimekuwa nikitazama mara nyingi wanaopelekewa misaada ni walemavu wa aina nyingine, yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, lakini ni nadra kusikia wenye mtindio wa ubongo au usonji wanakumbukwa. Nifuteni machozi kwa kuhakikisha mnawapa faraja na kuwasaidia," alieleza Dk. Mghwira. Alisema katika Mkoa wa Kilimanjaro wapo watoto wengi katika makundi mbalimbali wenye mahitaji maalumu na wanaishi kwenye mazingira magumu, hivyo ni vyema ikiwa wadau wote wakashirikiana kuhakikisha wanamaliza changamoto zao.

"Baadhi ya maeneo watoto wanapata tabu kutokana na migogoro ya kifamilia, talaka na mengine mengi. Wakati mwingine ajira za utotoni na mimba za utotoni zinatokana na kutengwa kwa baadhi ya makundi ama kusahaulika."

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Shirika la Connects Autism Tanzania (CAT), Graceanna Lyimo, alieeleza kuwa pombe ina athari kubwa na mbaya kwa wajawazito, kwa kuwa kuna tatizo kitaalamu linaitwa Fetal Alcoholic Syndrome (FAS) ambalo huwapata watoto mama zao waliokuwa wakitumia kilevi kupindukia.

Katika halfla hiyo, Dk. Mghwira alialika pia mashirika ya kiraia yanayojihusisha na kulea makundi mbalimbali ya watoto wenye changamoto yakiwamo ya Gabriela Rehabilitation Center, Msamaria Center For Street Children na Faraja Farijika Foundation.

Akitoa salamu zake, Kaimu Shekhe Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Mkoa wa Kilimanjaro (Bakwata), Shaban Mlewa, alisema watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ni wa kila mtu na wanaishi kwenye jamii, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuwasaidia.

"Ukizitazama kesi nyingi katika mahakama mbalimbali hapa nchini ni kwa sababu ya kugombania mali na hata wengine kuwadhulumu yatima, tuache hayo.

"Na kuwekeza katika watu wenye uhitaji maalumu katika kuwalipia ada za shule, kuwekeza kwenye afya na kuwasaidia chakula," alisem

# Masauni awaonya polisi wala rushwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Yusuph Masauni, amesema wizara hiyo inafuatilia nyendo na taarifa za askari wanaolichafua Jeshi la Polisi kwa kuendeleza vitendo vya rushwa.

"Jeshi letu la Polisi lina miiko yake katika utendaji wa kazi, lakini wapo askari wachache wanaoendelea na matukio ya rushwa, hali hiyo haikubaliki na atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu za jeshi," alisema Masauni.

Akizungumza jana katika mji mdogo wa Sanya Juu uliopo katika Wilaya ya Siha, Masauni aliwaonya askari dhidi ya vitendo hivyo.

Alitoa onyo hilo, baada ya kupokea malalamiko kuwa baadhi ya askari wa wilaya hiyo wanakiuka taratibu kwa kuwakimbiza ovyo madereva wa bodoboda na baadaye kutaka fedha.

"Nyie askari fanyeni kazi zenu kwa weledi na acheni kuwafukuza ovyo madereva pikipiki, nadhani jambo jema na ambalo lina afya ni kuandika namba za pikipiki kama hawakutii sheria za usalama barabarani. Kumfukuza mwendesha pikipiki ni hatari zaidi," alionya Masauni.

Aidha, alisema ili kazi ya polisi iwe nyepesi pia, ni lazima wananchi nao wawe na ushirikiano na Jeshi la Polisi.

Awali, Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel, akizungumza katika mkutano huo alisema kuna baadhi ya polisi wasio waaminifu wanawakamata watu ovyo na kuwapa kesi, huku pia likiwacheleweshea kesi na wengine kuomba rushwa katika Kituo cha Polisi Sanya Juu.

Kwa upande wake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Hamisi Issaha, alisema kuwapo kwa ushirikiano mzuri kati ya jeshi hilo na wananchi kumekuwa kukiwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Alisema wananchi hawawezi kuwapa ushirikiano polisi kama polisi wenyewe wanaondoa picha ya heshima kwa jamii.



Ukurasa 20

Marufuku za RC Makonda, biashara mifuko ya 'Kariakoo'




Ukurasa 19

Ulipo wajibu wa sekta fedha kufikia uchumi wa viwanda

BUFE

Ijumaa Mei 31, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Mikakati ilivyopenya na kusomba maelfu ya watalii China

Ukurasa 14



# Zambi alivyowaingiza darasa la saa moja magwiji wa korosho

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, akizungumza katika mkutano wa Runali. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango na Mwenyeki wa Runali, Hassan Mpako. **PICHA: SABATO KASIKA.**

**Na Sabato Kasika,** aliyekuwa Nachingwea

IJUMAA iliyopita, majira ya jioni mji wa Nachingwea mkoani Lindi ulipokea kundi kubwa la watu waliofurika katika nyumba mbalimbali za kulala wageni na kuzifanya nyumba hizo kujaa mapema.

Watu walikuwa ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Pili wa Chama Kikuu cha Ushirika Runali, waliofika hapo kwa ajili ya kuhudhuria mkutano huo uliofanyika Mei 25 katika ukumbi wa mikutano wa chama hicho.

Runali ni chama cha ushirika, kinachohusisha wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale, ambazo ndizo magwiji wa uzalishaji korosho, mkoani Lindi.

Wajumbe hao walitoka katika wilaya hizo tatu waliohudhuria mkutano wa chama hicho, wengi walilazimika kulala katika nyumba za wageni ili asubuhi wawahi mkutano huo.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Neno la serikali kwa watalii Wachina Ukurasa 20

BIASHARA

# Mikakati ilivyopenya na kuso ya watalii China, Israeli walio

• Hadi Desemba idadi kufikia 10,000 • Wajitolea kuna soko bure kwao • Wajuzi wa urembo nao 'ofa' yao

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

TANZANIA imebarikiwa kuwa na vivutio vya aina tofauti vya kitaalii, kama vile wanyama mbalimbali na mchanga unaohama.

Kila mwaka katika Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, marashi ya karafuu Visiwani Zanzibar, miti, mimea, mito, maziwa na maporomoko ya maji yanayopendeza kuangalia na Mlima Kilimanjaro.

**WATALII MAELFU**

Ni vivutio vinavyowafanya wageni kimataifa, wanatembelea nchi kujionea rasilimali zilizopo. Hivi karibuni, kulikuwapo kundi kubwa la watalii 1,000 kutoka nchini Israel, waliofika nchini na kukaa wiki moja, kuangalia vivutio vilivyopo.

Siku chache baadaye, kulikuwapo na kundi lingine la watalii kutoka China zaidi ya 330, waliofika kushuhudia rasilimali zilizopo.

Ni mafanikio yanayotajwa, ikiwa sehemu ya jitihada za serikali kwa kushirikiana na wadau wa Shirika la Hifadhi la Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Wengine katika chanzo cha jitihada hizo zenye mafanikio, ni Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA), Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na wadau wengine kutoka sekta binafsi.

Mkurugenzi wa TTB, Devotha Mdachi, anasema ujio wa watalii wa Kichina, waliofika nchini Mei 12, mwaka huu, waliletwa kupitia kampuni ya Touchroard International Holdings Groups ya China, ikiwa ni matunda ya makubaliano na bodi, waliyoingia na kampuni Novemba mwaka jana.

"Sisi tulikuwa ziara ya kutangaza utalii katika miji ya Beijing, Shanghai, Chengdu, Guangzhou na Hong Kong. Tukiwa huko, tukaingia makubaliano ya kutuletea watalii 10,000 na kampuni hii ya Touchroard, ambayo leo wametuletea watalii hawa, kama kundi la kwanza na tunasubiri lingine la watu 500 Juni mwaka huu," anaeleza Devotha.

Katika kundi la Wachina zaidi ya 330, inayojumuisha watu maarufu, wawekezaji kutoka kampuni 27 za China, waandishi wa habari 40 wa vyombo kutoka China, maofisa ngazi za juu serikalini na wakala wa kampuni kubwa za utalii za China.

Devotha anasema, watalii hao walitumia siku tano nchini, kuangalia vivutio vya wanyama katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, wakaona makundi makubwa ya nyumbu, simba, twiga, pundamilia, nyati, swala na fisi.

Ni ugeni ambao ulikuwa dha-




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimfunga vazi la asili mtalii kutoka Israeli, baada ya kuwasili nchini. Kulia kwake ni Waziri wa Maliasili na Dk. Hamis Kigwangwala. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Sisi tulikuwa ziara ya kutangaza utalii katika miji ya Beijing, Shanghai, Chengdu, Guangzhou na Hong Kong.**




Watalii wa Kichina wakivalishana nguo za Kimasai.

# omba maelfu tua nchini

di



Utalii,



hiri wengi wao walifurahia kupiga picha na mimea mbalimbali waliyoiona na magogo yake, katika hifadhi walizotembelea.

Pia, mkurugenzi huyo anasema walipata fursa kutembelea kreta katika hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro, Olduvai Gorge, maboma ya Wamasai na duka kubwa la vinyago, madini ya tanzanite na nguo za asili lililopo wilayani Karatu, ambako walifurahia fahari za rasilimali zilizopo.

Aidha, Devotha anasema katika makubaliano hayo waliyoingia na kampuni hiyo ya kutangaza utalii Bara la Afrika, ilichagua nchi tatu za Djibout, Zimbabwe na Tanzania, ambako walianza kutembelea Djibouti kwa siku moja, Tanzania siku tano na kumalizia Zimbabwe siku mbili.

Devotha anasema katika ujio huo, licha ya mafanikio waliyopata kutangaza vivutio na wageni kununua bidhaa nchini, kuna changamoto zilizojitokeza kuhudumia makundi makubwa ya watalii yanapofika na anazitaja kuwa ni uandaaji ugeni wa watalii zaidi ya 300 akisema 'si kazi rahisi.'

Anafafanua kuwa watalii hao wamefurahi sana sababu kila walichoelezwa nchini kwao kuwa wakija Tanzania watakiona na wamekishuhudia, hivyo kupitia kiongozi wao wameahidi mwezi huueta kundi la watalii 500.

Katika hilo, Mkurugenzi wa TTB, hivyo sio jambo la kubeza bali kila mwenye mapenzi mema na nchi hii anapaswa kufurahia.

"Naomba wadau wote wa utalii kila mmoja kwa nafasi yake afanye maboresho ya kasoro zilizojitokeza, kama vitanda vichache viongezwe, kama vyoo pia viongezewe, ili linapofika kundi la pili tuwe tumejitahidi kuondoa kasoro chache zilizojitokeza," anasema.

Devotha anasema licha ya kuhamasisha utalii nchini China, pia wamejipanga kuhamisha utalii nchini Urusi, India na nchi nyingine za mashariki ya mbali, ili waje kwa wingi kuona vivutio.

Aidha, anatumia fursa hiyo kuwataka vijana waliosoma nchini China ambao hawajapata ajira pamoja na vijana ambao wanajua lugha ya Kichina kuomba ajira kwa kampuni ya utalii hapa nchini, ili kuweka urahisi wa mawasiliano wageni hao wanapokuja nchini.

Anasema kupitia wageni hao wanaozidi kuongezeka kutembelea hifadhi zetu ni fursa kwa kila mmoja kwa nafasi yake kufanya anachoweza kufanya ili mwisho wa siku wote waje Tanzania na kupeleka sifa ilio sahihi kwa nchi hizo wanazofika kwetu.



Watalii kutoka China, wakinunua bidhaa za nchini.

**WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anasema watalii wengi wanapofika nchini ni lazima waondoke na historia, kwani wanapata fursa kuona wanyama wengi na Mlima Kilimanjaro, ambao ni mlima mrefu kuliko yote barani Afrika.

Majaliwa, anavitaja baadhi ya vivutio ni: mbuga za Selous, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro yenye shimo kubwa linalojaza wanyama wa aina mbalimbali, pia

Hifadhi za Taifa za Gombe, Katavi, Rubondo, Ruaha, Mkomazi, Mikumi na Serengeti.

Pia, katika eneo jingine ni Zanzibar kwenye fukwe zenye mchanga mweupe na harufu nzuri zenye marashi ya karafuu pamoja na zingine.

Anasema, vivutio vilivyopo katika hifadhi hizo na zingine nchini, mtalii yeyote atakayefika nchini atafurahia, kwa sababu hatoweza kuviona kwingineko vivutio hivyo popote duniani, isipokuwa Tanzania.

"Watanzania tunapaswa kufurahia matunda tuliyoanza kuyaona, kwani kufika kwa makundi makubwa ya watalii nchini ni neema kwa sekta ya utalii na tunaongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, kwani hawataondoka bila ya kununua bidhaa za kitamaduni na vingine," anasema.

Majaliwa anatoa wito kwa China kuendelea kufanya kazi na Tanzania na wao watadumisha ushirikiano uliopo na urafiki wao uliojengwa na waasisi wa nchi hizo mbili.

**DK. KIGWANGWALA**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, anasema Tanzania imeweka nchi kadhaa katika mkakati wake wa utalii, zikiwamo Australia, Israel, Oman, Russia, Cuba na China, ikiwapa kipaumbele cha uwekezaji katika eneo hilo.

"Tunajua nchi hizi tukishika soko lao, tutaongeza idadi kubwa ya watalii wanaokuja kutembelea vivutio vyetu na kuongeza pato la taifa na wawekezaji wa sekta ya utalii," anasema.

**WAZIRI KABUDI**

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashari-

INAENDELEA UK.18

## Neno la serikali kwa watalii Wachina




Msanii wa muziki kutoka China, Di, akipokea zawadi kutoka kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI watalii kutoka China 336 walipotembelea nchini, hivi karibuni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipata fursa ya kuongea nao.

Alisema, Tanzania kwa miaka mingi imekuwa ikipokea watalii, hata hivyo kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na kuboreshwa mbinu za kuvutia watalii kutoka nje pamoja na kuweka msisitizo kwenye diplomasia ya uchumi kupitia balozi nje ya nchi, imeanza kupokea watalii kwa makundi kutoka sehemu mbalimbali.

Majaliwa anataja vivutio vya utalii vya asili kama vile hifadhi za wanyama, fukwe za bahari, milima mirefu, vyakula na mavazi ya asili visivyopatikana kwingine duniani.

"Wageni wetu mmefika kwenye nchi salama kabisa, nawaomba mwendelee kufurahia vivutio vilivyopo. Ni matumaini yangu kuwa, mtapofika Ngorongoro kwenye bonde lililosheheni wanyama badala ya maji kama yalivyo mabonde mengi.

"Eneo hili ni maarufu kama Ngorongoro Crater huwezi kulipata kokote duniani isipokuwa Tanzania pekee," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo, kuuelezea Mlima Kilimanjaro kwa Watalii kwamba ndio mrefu zaidi barani Afrika na hakuna anayeweza kuuona, kuuzunguuka wala kuupanda bila kuja Tanzania.

Waziri Mkuu alitumia nafasi hiyo kuwashukuru na kuwapongeza wote waliofanikisha ziara ya watalii hao akiwamo Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na kuwaomba watalii hao kuwa mabalozi wazuri wa vivutio vya utalii vya Tanzania wanaporudi kwao.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa. Palamagamba Kabudi, alisema kuwa ziara ya watalii hao imedhihirisha namna wizara kupitia balozi zake na kwa kushirikiana na wadau wengine inavyotekeleza diplomasia ya uchumi ambayo imejikita katika kuvutia watalii na wawekezaji pamoja na kukuza biashara nchini.

Vilevile aliongeza kuwa serikali kwa sasa ina mpango mkubwa wa kutangaza utalii kwenye nchi mbalimbali kupitia mpango uliopewa jina la "New Horizon, Tour Africa" na kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa hii ya watalii wanaoendelea kuja nchini makundi kwa makundi ili wanufaike na uwepo wao.

Waziri wa Maliasilia na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, alieleza kwamba sekta ya utalii nchini imepiga hatua kubwa katika kipindi kifupi cha Serikali ya Awamu ya Tano na anafafanua:

"Hii ni hatua kubwa kwenye sekta ya utalii nchini kuona makundi ya watalii yakija nchini mfululizo. Tumeamua kuwekeza katika nchi tano za kipaumbele cha pili kwa maana ya China kama mdau wetu namba moja, Israel, Oman na nchi zingine za mashariki ya kati, Australia na Urusi."

Mwenyekiti wa Kampuni ya TouchRoad International Holding Group ya China, Liehui He ambayo iliratibu ziara hiyo, alikiri kufurahishwa na mapokezi makubwa na kwamba kampuni yake itaendelea kushirikiana na serikali kwenye sekta ya utalii kama walivyoahidi kwenye makubaliano waliyosaini kati yao na TTB.

Wakiwa nchini, watalii hao watatembelea maeneo mbalimbali ya utalii; Hifadhi ya Wanyama ya Manyara, Ngorongoro, Serengeti, Olduvai Gorge pamoja na kutembelea maboma ya Wamaasai.

Aidha, sehemu ya watalii hao ambao ni wawekezaji 57 kutoka kampuni 26 za China wanatarajiwa kushiriki kongamano la uwekezaji litakalofanyika jijini Arusha tarehe 13 Mei 2019.

**Ni kwa mujibu wa Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.**

BIASHARA

# RC Zambi alivyowaingiza darasa la saa moja magwiji wa korosho

## • Awa 'mbogo' ubabaishaji uliojaa ushirika • Wajumbe Runali kimya kufuatilia darasa • Mwenyekiti 'amkubali' watazingatia somo

INATOKA UK.13

Inawezekana siyo hiyo wamiliki wa nyumba hizo walivuna pesa, kutokana na ukweli kwamba kwa wale ambao jioni walikuwa wakitafuta vyumba vya kulala walihangaika sana kwani baadhi ya nyumba zilikuwa tayari zimejaa.

Mei 25 saa mbili asubuhi, wajumbe hao zaidi ya 100 walikuwa wameshafika nje ya ukumbi wa mkutano na kisha majira ya saa waliingia ndani kumsubiri mgeni rasmi ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi.

Baada ya mkuu wa mkoa kuwasili ukumbini saa nne na nusu, ulianza utaratibu wa utambulisho na kisha ikifuata risala ya chama hicho iliyosomwa na mtumishi wa Runali, Caroline Mnunduma.

Ni risala yenye maudhui yaliyojikita katika maeneo matatu, ambayo ni historia ya Runali, mafanikio na changamoto zake, huku hadhira yote na mgeni rasmi Mkuu wa Mkoa, wakifuatilia kwa umakini, kasha kipaza sauti kikakabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, kwa ajili ya kutoa salamu na kumkaribisha mgeni rasmi.




Mwenyekiti wa Runali, Hassan Mpako akizungumza kwenye mkutano wa Runali.

#### MKUU WA MKOA

Baada ya kukaribishwa, Zambi aliyewahi, aliyewahi kuwa Mbunge wa Mbozi Mashariki, alitumia saa moja kujikita zaidi katika kutoa elimu ya jinsi ambavyo ushirika unaweza kuwa imara na pia sababu zinazoweza kuusambaratisha.

Zambi akiwapatia maneno makali wajumbe hao, anasema katika vyama vya ushirika kuna changamoto nyingi zinazosababishwa na viongozi wasio waaminifu, ambao wanaifanya serikali ilaumiwe, kutokana na makosa yao.

"Kwa mfano msimu wa korosho uliopita, kulikuwapo na baadhi ya viongozi wa vyama waliokuwa wakisafirisha korosho kwenda katika ghala kuu, huku wakizipunguza njiani ili kuichonganisha serikali na wakulima.

"Ninasema (viongozi) kuichonganisha serikali kwa sababu mwisho wa siku wanadai korosho zimeibiwa katika ghala kuu na kumbe wamepunguzia njiani," anasema.

Zambi anawatahadharisha viongozi wa ushirika, kwamba wasipokuwa waaminifu kuna hatari wataua ushirika, huku akiwakumbusha kwamba na ushirika unajengwa na dhana ya uaminifu na uadilifu.

Msisitizo wake ni kwamba, wajumbe wa vyama hivyo vya ushirika wanapaswa kujiwekea utaratibu wa kuchagua viongozi wanaotanguliza maslahi ya vyama na kamwe isiwe ya kwao binafsi.

> "Ninasema (viongozi) kuichonganisha serikali kwa sababu mwisho wa siku wanadai korosho zimeibiwa katika ghala kuu na kumbe wamepunguzia njiani.



Baadhi ya wajumbe wa mkutano wakimsikiliza kwa umakini mkuu wa mkoa. **PICHA: SABATO KASIKA**

Katika eneo hilo, Mkuu wa Mkoa anatoa agizo akisema: "Kuanzia sasa, kila kiongozi wa chama cha ushirika lazima ajue idadi ya wanachama wake, majina yao na ukubwa wa mashamba yao iwe rahisi kuhakiki," anasema.

Anafafanua kuwa kuna chama alikwenda kukitembelea akakuta viongozi hawajui idadi ya wanachama wao, majina wala ukubwa wa mashamba yao na kwamba hilo ni tatizo kubwa, pia viongozi wa aina hiyo hawatakiwi.

Mkuu huyo wa mkoa, huku ikionyesha kuchukia tabia za baadhi ya viongozi wanaochangia kuvuruga vyama vya ushirika, anatoa tahadhari kwamba ushirika siyo mahali pa kuchuma, bali kutumikia wakulima.

Hayo yaliendelea huku wajumbe waliotekwa na ujumbe mzito wa RC, wakimsikiliza kwa makini, anahamishia 'dongo' pia kwa makarani na makatibu wa vyama vya ushirika, akiwaambia nao baadhi yao ni tatizo, kwa vile ni sehemu ya mtandao wa wizi na udanganyifu.

"Ikiwezekana, Mrajisi wa Mkoa jaribu kupunguza idadi ya vyama vya ushirika ili kubaki na vile ambavyo vinafanya kazi kwa kuzingatia dhana ya ushirika, ambayo imejengwa katika uaminifu na uadilifu," anasema.

Mwisho akawaachia 'ushauri wa bure' kwamba Runali iwe na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyama vya ushirika, kwa vile ndivyo inavyotakiwa katika kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha ushirika unaendelea kuimarika.

#### MWENYEKITI

Hassan Mpako ni Mwenyekiti wa Runali, anayeelekeza kukipokea chama kitazingatia somo na kuhakikisha vyama vya ushirika vya msingi, ambavyo ni wanachama wa Runali vinakuwa na viongozi bora.

"Tunatambua sisi ni binadamu tulioletwa hapa duniani na kuwekewa utaratibu wa kuishi, ambao kila mmoja wetu anapaswa kufuata, ndio maana akaweka serikali za binadamu na madili ya kiroho ili haki itendeke," anasema Mpako.

Anafafanua kuwa, hata mikusayiko yao ni sehemu ya utekelezaji wa waliowekewa na serikali, kwa lengo la kufanya kazi.

Anawakumbusha wajumbe wenzake wa mkutano, kuzingatia fursa, maadili na imani, jambo litakalowafanya wana - ushirika kuwa na ufanisi na kuondoa anayoyaita 'makondokando' ndani ya ushirika.

Katika kuthubutu kuzingatia ufanyaji kazi kwa weledi, anasema Rinali imeajiri wataalamu wenye sifa, akiwataja baadhi kwa vyeo; Meneja Mkuu, Mhasibu Mkuu na Meneja Masoko.

"Baada ya kuajiri watu hao wenye sifa, tunaamini kwamba changamoto mbalimbali za kitaalamu ambazo hazitajitokeza tena, kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma wakati Runali inaanzishwa," anasema.

Anafafanua kuwa, katika utaratibu huo wa kuajiri wataalamu, kulingana na nafasi wanazoomba, wanavihimiza vyama vyote vya ushirika vya msingi kuitumia, ili viweze kuwa na mafanikio ya uendeshaji.

#### HISTORIA YAKE

Mwenyekiti huyo anasema, Runali inayoundwa na wilaya tatu za Ruangwa, Nachingwea na Liwale, ilianzishwa mwaka 2013 ikiwa na wanachama 52, lakini hadi sasa wameongezeka kufikia 104, huku kukiwapo maombi mengi ya kujiunga.

Sababu ya Runali kuanzishwa baada ya wilaya hizo zinazolima korosho kwa wingi, kujivua uanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Lindi (Ilulu). Kilipata usajili rasmi, Februari mwaka jana.

"Tangu Runali ianzishwe, imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi mbalimbali, kama ujenzi wa ofisi ya chama, ghala dogo la kuhifadhi pembejeo na magunia, ambalo ujenzi wake unaendelea," anasema.

Mpako anasema, Runali inaendelea kujenga vituo vya maandalizi ya malipo ya wakulima wilayani Nachingwea, wanavyotarajia itagharimu Sh. milioni 280, na wameshaanza ujenzi wa ghala kuu wilayani Ruangwa.

"Ghala hilo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za mazao ya wakulima wetu kwa wakati mmoja. Hadi kukamilika kwake litagharimu zaidi ya Sh.bilioni moja," anasema.

#### MALENGO YAO

Anasema wakati ujenzi wa ghala kuu ukiendelea wilayani Ruangwa, Runali pia ina mpango wa kujenga mengine katika wilaya za Nachingwea na Liwale yenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za mazao kila moja.

"Lengo lingine ni kujenga majengo ya kuandalia malipo katika wilaya za Ruangwa na Liwale, kwa sababu tayari Nachingwea lipo. Pia, tumepanga kununua eneo la ekari 500 kwa ajili ya shamba la mikorosho," anasema.

Anafafanua kuwa hilo litakuwa ni shamba darasa kwa ajili ya wanachama wa Runali, ili wajifunze kilimo bora cha korosho na wanufaike zaidi na kilimo cha zao hilo kuu la biashara, kwenye mikoa ya kusini.

Runali pia, imepanga kujenga kiwanda cha kubangua korosho na kuchakata mbaazi, pia kuendelea kuhamasisha kilimo cha zao la alizeti, ili liweze kuwa maarufu mkoani Lindi.

"Wakulima wetu wanategemea kilimo cha korosho na ufuta kama mazao ya biashara, hivyo ipo haja ya kuwahamasisha waanze kujikita kwenye kilimo cha alizeti kwani zao hilo halitegemei soko la nje ya nchi," anasema.

Anaongeza kuwa, iwapo watakuwa na mapato ya ziada watanunua mbegu za alizeti na kuzigawa kwenye shule za msingi, sekondari na serikali za vijiji katika wilaya zinazounda Runali ili kuwa na mashamba darasa na wakulima watajifunza.

# Biashara katika picha



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa pili kushoto), akibadilishana hati za makubaliano ya ushirikiano wa miaka mitano na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS), Nicomed Bohay, makabaliano yatakayoiwezesha NBC kusaidia mnyororo wa thamani wa sekta ya kilimo biashara nchini. NBC pia ilipokea mfano wa hundi ya Dola 1,000,000 kutoka PASS zitakazotumika kama dhamana katika mikopo ya kilimo itakayotolewa na benki hiyo. Hafla ilifanyika jijini Arusha jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru na Ofisa Mtendaji Mkuu wa PASS, Anna Shenalingigwa. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa vyombo akipanga bidhaa zake, kando ya barabara, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa waenda kwa miguu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Kinamama wachuuzi wa vitafunwa wakisubiri wateja wao katika eneo la Feri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BIASHARA

# Mikakati ilivyopenya na kusomba maelfu ya watalii China, Israeli



Kundi la watalii kutoka Israeli wakifuatilia hotuba ya kuwakaribisha nchini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.15**

ki, Profesa Palamagamba Kabudi, anasema ongezeko la watalii nchini katika siku za karibuni na hasa Wachina, hususan kutoka miji mikubwa miwili ya Zhejiang na Shanghai.

Profesa Kabudi, anafafanua kwamba ni matokeo ya jitihada kubwa za Rais Dk. John Magufuli, TTB, Wizara ya Maliasili na Utalii na ubalozi wa China nchini na wadau wote wa utalii.

**TTB YANENA**

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, anasema watalii hao wa Israel na China wameguswa na vivutio vilivyopo nchini na wameahidi kuvitangaza katika maeneo mablimbali nchini kwao.

Jaji Mihayo anasema, katika kundi la watalii wa China la hivi karibu lililoondoka, wameahidi kuwaleta wataalamu wa kutengeneza bustani maalum zenye ukubwa wa ekari sita, kila moja zenye maua mbalimbali ya asili, kama ilivyo bustani za nchini kwao, ambazo zinawaingizia pato kubwa kutoka kwa watalii wanaopenda mimea ya asili.

Pia anasema watalii hao wameitaka TTB kupeleka mabango mbalimbali bila ya gharama nchini kwao China, yatakayowekwa kwenye bustani hiyo ya maua, kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii nchini.

"Katika hili la kuandaa mabango yenye vivutio vyetu mbalimbali, tumeanza kulifanyia kazi na hivi karibuni tutakapoenda tena China tutaenda nayo, ili yakawekwe maeneo yao mbalimbali, kwa ajili ya kuvutia watalii wengi zaidi kutoka nchi hiyo waje Tanzania kuona rasilimali zetu," anasema.

> **"Una lengo la kuhakikisha Tanzania haipotezi watalii walioanza kutembelea vivutio, wanajitahidi kuboresha miundombinu ya kitalii, ili kuhakikisha idadi yao inaongezeka badala ya kupungua.**



Mwinuko maarufu kama 'Mlima wa Simba' uliopo katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, ukiwa na kundi la Simba kileleni.

Jaji Mihayo anasema, baada ya kuondoka kwa kundi hilo la kwanza na timu yote ya maandalizi, watajipanga kuweka sawa kuondoa dosari mahali zilipojitokeza, ili makundi mengine yatakapokuja wasiweze kuona.

Ofisa Uhusiano Mkuu wa TTB, Geofrey Tengeneza, anasema licha ya kuanza kupokea makundi makubwa ya watalii kwa siku za karibuni, Tanzania imejipanga kutekeleza mpango mkakati wa awamu ya pili, wa kuingia katika masoko ya China, India, Israel, Australia na Oman walikojiwekea malengo.

Anasema, mkakati wao wa kwanza ulilenga kufikia masoko ya mwanzo ya Marekani, Uingereza Italia na Ujerumani, ambao nchi ya Israel wameshaleta watalii 1,000 na Wachina wanatarajia kuleta watalii 10,000 kutembelea vivutio hivyo na anaahidi kabla ya Desemba mwaka huu, wote watakuwa wameshafika nchini.

Anasema katika kampeni hiyo, Tanzania itaendelea kuzuru katika nchi hizo na zingine, ili kuhamasisha utalii na wanatarajia kushirikisha makundi mbalimbali kama vile wasanii maarufu, wanahabari na wanamichezo, ili watumike kutangaza vivutio hivyo.

Pia, Tengeneza anasema kuna lengo la kuhakikisha Tanzania haipotezi watalii walioanza kutembelea vivutio, wanajitahidi kuboresha miundombinu ya kitalii, ili kuhakikisha idadi yao inaongezeka badala ya kupungua.

"Katika kuhamasisha watalii hawa wa nje ya nchi tunapenda kuhimiza watalii wa ndani kutembelea vivutio vyetu na tuache kutegemea watalii wa nje ya nchi, sababu kuna madhara yake wakati yanapotokea magonjwa ya mlipuko au vita nchi jirani huwa wanaogopa kutembelea," anafafanua.

**WAFANYABIASHARA**

Mfanyabiashara kutoka duka la vinyago, vito vya tanzanite na nguo za asili wilayani Karatu, Sisca Dodhia, anaipongeza serikali na TTB, kwa jitihada za kuleta kundi kubwa la watalii toka China.

"Kweli nimeona matunda kwani wengi wao wamenunua kahawa ya Tanzania, vinyago vya Makonde na madini ya tanzanite, ambayo waliyanunua kwa wingi, sababu wanasema wanayapenda sana na wanatamani wawe na soko kule kwao waweze kuuza," anasema.

Meneja wa Benki ya NMB tawi la Karatu, Willium Nkuna, anasema wao kama wadau wa fedha, waliposikia ujio wa watalii wanatembelea duka la vinyago, waliamua kutumia fursa hiyo kuhamishia huduma zao dukani hapo.

"Kweli tumewarahisishia huduma, wengi wao walikuwa wakitoka kwanza kwetu kubadilisha fedha za kigeni na kuingia 'duniani' kununua bidhaa za vinyago na tanzanite, lengo kuonyesha Tanzania hatupo nyuma katika kila nyanja," anasema.

Anasema, anaomba wadu wengine kutumia fursa kama hizo pale wanaposikia wageni wanakuja nchini kuwasogezea huduma walipo, ili kuwapa urahisi wa kununua bidhaa mbalimbali wanazotaka.

UCHUMI

# Ulipo wajibu wa sekta ya fedha kufika uliko uchumi wa viwanda

• Imekamata 'mikono' ya wakulima • Wasisitiziwa umuhimu wa bima

**Na Reubeni Lumbagala,**

DODOMA

MSIMAMO na mikakati ya serikali hivi sasa, umejipambanua kuelekea katika Tanzania yenye uchumi wa kati, unaoegemea viwanda ifikapo mwaka 2025.

Viwanda ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja, katika maendeleo ya nchi na ukuaji wake unajielekeza katika sura kuu mbili.

Hapo msingi wake unahusisha sekta nyinginezo, kama vile kilimo, usafirishaji, elimu, ardhi, mawasiliano, maji, afya na nishati

Mtiririko na muungano huo kiuchumi una msamiati wake unaojulikana kama 'backward and forward linkage' kwa maana ya kila kinachonfayika katika ngazi moja, uwezekano wa kupiga hatua, umeshikiliwa na shughuli nyingine kiuchumi katika ngazi tofauti.

Mathalan, katika kuufanya mfumo wa uzalishaji viwandani, ili ufanye kazi na mfumo tegemezi kutoka sekta ya kilimo, kunakopatika malighafi.




Maofisa kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Benki ya Posta (TPB), wakionyesha nyaraka kuhusu Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo nchini (SCGS), inay0lenga kuwawezesha wakulima kukopa katika taasisi za fedha, ikiwamo benki za biashara. **PICHA: MTANDAO.**

Dira ya viwanda na ya uchumi wa kati nchini, inasimamiwa na serikali kwa kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi, ili kutimiza ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi ( Public and Private Partenership - PPP). Ni mfumo unaofanyiwa kazi na serikali, tayari ukitumika chini ya sheria maalum.

Serikali kwa upande wake, inawajibika katika kutunga sera nzuri za kukuza viwanda, kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara, kujenga miundombinu bora.

Pamoja na hayo, ipo sekta ya fedha ambayo ni mdau mkubwa wa kusimamia, kutekeleza na kufanikisha utekelezaji wa maendeleo ya viwanda.

Hicho ndicho kinafungua msukumo kwa wakulima, wafanyabiashara na wawekezaji wanaopaswa kuzitumia taasisi za fedha, ambazo zipo kwa ajili ya kuwawezesha wote wanaohitaji huduma za kifedha, ili kufanikisha uwekezaji wa viwanda.

### NAFASI YA FEDHA

Katika mabalishano yakiwamo ya 'Forwad and backward' linkage, kuna jambo linalotakiwa kuwezeshwa ni nafasi ya fedha. Jukumu lake kuu ni kuwezesha dira na malengo yaliyopo katika uzalishaji, hadi katika soko lake.

Tafsiri fupi ni kwamba, dira na uzalishaji mara zote unafanikishwa na mtaji, unaowezeshwa na fedha, lakini kwa bahati mbaya, upatikanaji wake ni tatizo kuu, ambayo huhitimishwa kwa njia nyingi kama vile kukaribisha wawekezaji wenye mitaji na uwezo wa kuendesha miradi husika, pia mikopo ni njia ya pili.

Hapo ndipo taasisi za fedha huchukua nafasi yake katika utoaji mikopo. Zinaelezwa kuwa na mchango mkubwa wa kufanikisha maendeleo ya viwanda nchini kwa njia mbalimbali.

Utakumbukwa katika kuimarisha ombwe hilo, ilipitishwa Sheria ya Fedha na Benki nchini, iliyofungua mlango wa kuanzishwa benki nyingi binafsi nchini, pia utitiri wa asasi binafsi za fedha, huku vikundi vya ushirika wa kifedha (Saccos) kupitia sheria tofauti, vilianzishwa.

Pia, mtazamo huo wa maboresho, hivi karbuni katika hilo, serikali iliimarisha Benki ya Rasilimali nchini (TIB) kwa kuongezea mitaji ya kuinua uwekezaji mkubwa kama wa viwanda nchini, hali kadhalika uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Kwa ujumla taasisi zote za fedha nchini, zina wajibu wa kisheria wa kutoa elimu ya uwekezaji kwa wananchi. Taasisi hizo zinaajiri watumishi weledi katioka masuala ya uchumi, biashara, fedha na masoko kutoa huduma kwa wateja.

Hivyo basi, wanawajibika kuzitumia elimu zao kuwajuza wananchi ujasiriamali na uwekezaji, wapate uelewa wa usahihi katika kuwekeza mitaji ya ngazi zote za viwanda; vidogo, kati na vikubwa, kwa maendeleo ya nchi.

Pia, taasisi hizo za fedha zinawajibika kuwajengea uwezo wananchi na wawekezaji hasa wawekezaji wadogo na wazawa ili kuwa na maarifa ya kutosha ya uwekezaji.

Hiyo inafanyika kupitia semina na mikutano wanayoendesha, kuwafikia wananchi washiriki katika uchumi wa viwanda.

Pili, wanatakiwa kutoa mikopo yenye masharti na riba ya nafuu, kwani wananchi wengi hawana mitaji ya kutosha kufanikisha uanzishwaji wa viwanda na miradi mingine.

Uwepo wa riba kubwa na masharti magumu katika taasisi za fedha, inatajwa kuwa kikwazo kikubwa kwa uwekezaji wa sekta ya viwanda.

Kwa kutambua umuhimu wa taasisi za fedha na nafasi ya mikopo katika uchumi wa viwanda, uongozi wa benki na washirika wao, wanaelezwa jukumu la kufanya marekebisho, ili kufanikisha utoaji mikopo yenye masharti nafuu.

Ni hivi karibuni, serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT), iliingilia kati kwa kuchukua hatua kadhaa kama vile kupunguza riba kwa fedha inayozipatia benki na wakati huohuo, kuzitaka benki nyingi kupunguza riba hizo, hatua zilizokwishaanza kuchukuliwa.

Tatu, asasi hizo zina wajibu wa kutoa huduma ya bima kwa viwanda na mazao ya wakulima. Mashirika na kampuni ya bima, ni miongoni mwa wenye wajibu huo.

Viwanda vinaelezwa kuwa ni majengo, yanaweza kupata majanga kama kuungua moto, kubomoka kwa sababu ya matetemeko ya ardhi.

Wawekezaji wa viwanda wanapaswa kupewa elimu ya bima, ili waweze kujiunga na huduma ya bima kulinda viwanda vyao dhidi ya majanga yanayoweza kuwaletea hasara katika uwekezaji wao.

> **"Tathmini zinaonyesha, taasisi nyingi za kibenki hadi sasa zimejikita katika utoaji huduma mijini, kuliko vijijini ambao inaaminika wakipewa elimu sahihi, wataweza kujiwekea akiba taratibu.**

Pia, hata mazao ya wakulima yanaelezwa ni muhimu kuwekewa bima, kutokana na kuwapo changamoto kama vile ukame, magonjwa, mafuriko na wadudu waharibifu wa mazao.

Mkurugenzi wa Leseni na Mwenendo wa Soko kutoka Mamlaka ya Bima Tanzania, Samweli Mwiru, ana ufafanuzi: "Bima itasaidia endapo patatokea majanga yeyote katika kilimo na mazao, kampuni ya bima itaweza kuwalipa hizo gharama kumfanya mkulima asifilisike."

Nne, inaelezwa kuwa wananchi wengi wa vijijini hawajafikiwa na huduma za kibenki. Ni hali inayoelezwa kusababisha wananchi husika washindwe kufungua akaunti za benki, ni muhimu kiusalama na utunzaji fedha.

Tathmini zinaonyesha, taasisi nyingi za kibenki hadi sasa zimejikita katika utoaji huduma mijini, kuliko vijijini ambao inaaminika wakipewa elimu sahihi, wataweza kujiwekea akiba taratibu.

Ni kupitia mtazamo huo, wananchi wanaelezwa kukifaidika kwa kuweka akiba taratibu, wanahamia katika kujiunga vya kuweka na kukopa (SACCOS), pia vikoba ambako wanapataa mitaji ya kuwaingiza katika kilimo na viwanda.

Pia, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ina jukumu la kufikisha huduma zake katika maeneo ya vijijini, ambako wakulima wanapatikana. Hapi ndiko mlango wa Tanzania kuingia katika uchumi wa kati, ifikapo mwaka 2025, kwa wananchi kuzitumia taasisi za fedha.

BIASHARA

# Marufuku za RC Makonda, biashara mifuko ya 'Kariakoo' zinapogongana

## • Maji ya Kandoro kubaki ni simulizi • Machinga kupendeza kwa vitambulisho

**Na Sabato Kasika**

MWANZONI mwa Aprili mwaka huu, serikali ilitangaza kuwa Juni Mosi ambayo ni kesho, itakuwa marufuku kutengeneza, kuingiza, kuuza na kutumia mifuko ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa na matumizi yake yatakoma Mei 31.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ndiye aliyetoa kauli hiyo Jumanne, bungeni Dodoma, alipohitimisha hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2019/2020.

"Kuanzia sasa tunatoa fursa ya viwanda kubadilisha teknolojia, wauzaji kuondoa mzigo uliopo. Ofisi ya Waziri wa Nchi, Makamu wa Rais, itajiandaa kutumia kanuni chini ya Sheria ya Mazingira, ili kulifanya katazo hili kuwa na nguvu ya kisheria," Waziri Mkuu ndivyo alivyosema.

Waziri Mkuu aliendelea: "Tunachukua hatua hii ili kulinda afya ya jamii, wanyama, mazingira na miundombinu dhidi ya athari kubwa zinazotokana na taka za plastiki."

Tangu wakati huo, kumekuwapo matangazo mengi ya kukataza, ikiwakumbusha Watanzania kuwa uamuzi wa kupiga marufuku mifuko hiyo jijini Dar es Salaam kama 'Kariakoo' haitobadilika.

Serikali katika uamuzi wake inalenga kudbibiti madhara yake kimazingira, ikihusisha vifo vya mifugo wanaokula plastiki, kuziba mifereji, kuchafua mazingira kwa kushindikana kuoza.

Ni siku chache zimepita, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema ufungaji wa maji ya kunywa katika mifuko ya plastiki maarufu kama 'Kandoro' ni maarufu na kwamba biashara hiyo haina nafasi kuanzia kesho.

Anasema, serikali imeshatoa matangazo mengi kuhusu marufuku athari ya mifuko hiyo na serikali inaweza kutumia fedha nyingi kutangaza, lakini utekelezaji wa watumiaji ni dhaifu.

### KIFUNGO NA FAINI

Iijulikane kuna Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuna kanuni zilizokwishatungwa za mwaka 2019, kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.

Kuna kifungu kinachoorodhesha makosa matano ambayo ni; kuzalisha na kuagiza mifuko ya plastiki, kusafirisha nje ya nchi mifuko ya plastiki, kuhifadhi na kusambaza mifuko ya plastiki, kuuza na kumiliki na kutumia mifuko hiyo.

Na katika hilo, kila kosa lina adhabu yake kwa mujibu wa kanuni hizo, kulingana na uzito wa kosa lenyewe. Kwa mfano, uzalishaji na uagizaji, adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tano na haizidi shilingi milioni 20; kifungo kisichozidi miaka miwili jela, au adhabu zote kwa pamoja.



Shughuli za umachinga zikiendelea jijini Dar es Salaam. Picha nyingine, uhalisia wa biashara na kutapakaa mifuko ya plastiki. **PICHA ZOTE: MKTANDAO**

> **"Serikali imeshatoa matangazo mengi kuhusu marufuku athari ya mifuko hiyo na serikali inaweza kutumia fedha nyingi kutangaza, lakini utekelezaji wa watumiaji ni dhaifu.**





### MACHINGA DAR

Wakati sakata la mifuko ya plastiki linapokwisha, wajasiriamali wadogo wanaohamahama, maraufu kama machinga, waliopo jijini Dar es Salaam wasio na vitambulisho vya ujasiriamali, nao wanakabiliwa na agizo la Mkuu wa Mkoa Paul Makonda, ambaye ana msako wake kuanzia Jumatatu, anapambana na machinga wasio na vitambulisho.

Makonda anasema ni uamuzi unaotokana na ukweli kwamba, amewapa muda wa kutosha kujisajili na kupatiwa vitambulisho hivyo.

Itakumbukwa, katika utoaji wa vitambulisho hivyo, Rais Dk. John Magufuli, aliwahimiza viongozi wa mikoa na wilaya wahakikishe zinawafikia wananchi waliko na amekuwa akiendelea kuhimiza katika ziara zake mikoani.

Katika baadhi ya maeneo alifikia hatua ya kuwanyooshea kidole kuwapo urasimu katika utoaji vitambulisho hivyo, jambo aliloliweka wazi hajapendezwa nalo.

Makonda anasema, ameibaini kuwapo wafanyabiashara wanaoendesha shughuli za umachinga bila ya vitambulisho na hiyo ni baada ya kufanya ziara katika mitaa tisa jijini.

Kwa maana hiyo ni kwamba wakati sakata la mifuko likifikia mwisho, hili la vitambulisho linaweza kuwakumba wengi, kutokana na hicho alichobaini mkuu wa mkoa, wengi wa machinga hawana.

Baada ya Dar es Salaam kuanzisha msako huo, kuna uwezekano mkubwa ukapanuka hadi katika mikoa mingine nchini, kwani wanaangukia katika agizo moja kutoka kwa Rais la kutaka vitambulisho hivyo vinavyopatikana kwa gharama ya shilingi 20,000 na hakuna tozo nyingine tena ya kodi, kwa kila atakayekuwa nacho.

Kigezo ni kinatolewa kwao wajasiriamali wote wenye mitaji ya mapato chini ya shilingi milioni nne kwa mwaka.



## HABARI MBEYA

# Jafo awakumbusha ma-DED mikopo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, amewataka wakurugenzi kusimamia kikamilifu utoaji wa fedha za asilimia nne kwa vijana ili ziwasaidia katika shughuli zao za kujiingizia kipato.

Jafo alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa kukabidhi Sh. bilioni 1.7 kwa taasisi tisa ambazo zinasaidia utengenezaji wa ajira, ujasiriamali, uongozi na maisha bora kwa vijana kupitia mradi wa Inua Vijana wa 'Feed The Future' unaofadhiliwa na serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (Usaid).

Alisema serikali imetoa mwongozo rasmi wa kusimamia asilimia 10 ya fedha za mapato ndani ya halmashauri kuwa lazima kutolewa kwa makundi maalumu ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Waziri Jafo alisisitiza kuwa wakurugenzi wanapaswa kusimamia na kugawa fedha hizo bila upendeleo kwenye makundi ambayo yamekidhi vigezo vya kupata mikopo hiyo.

"Serikali imejitahidi kutengeneza mazingira rafiki ili walengwa wanufaikea na mikopo iliyotolewa na halmashauri kupitia vyanzo vyake. Ninasisitiza fedha hizo zikawanufaishe walengwa na si vinginevyo na jukumu la kusimamia utoaji wa mikopo ni la wakurugenzi, hivyo mtende haki," alisema Jafo.

Mkurugenzi Mkazi wa Usaid, Andrew Karas, alisema mradi wa Inua Vijana wa 'Feed The Future' unaofadhiliwa na shirika hilo una lengo la kuwawezesha vijana kujinufaisha na fursa mbalimbali za kiuchumi.

Alisema kupitia mradi huo, vijana wanapewa elimu ya ujasiriamali, wanahamasishwa kujiunga kwenye vikundi, ili kukopesheka, lakini pia kunufaika na fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye mradi huo ikiwamo nyenzo za kufanyia shughuli zao.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo alilitaka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) kutoa elimu ya kuongeza thamani ya mazao na bidhaa wanazozalisha wakulima na wajasiriamali ili zimudu soko la ushindani. Alisema elimu hiyo itawasaidia hasa vijana kupata uhakika wa soko na kujiongezea kipato sambamba na kuzalisha ajira kwa vijana wengine.



Kamishna Msaidizi wa Polisi, Deborah Magiligimba, akiwa amebeba nyoka mkubwa aina ya chatu wa kikundi cha utamaduni cha Mango Star, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Walinda Amani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# CCM yaonya wanaonunua uongozi

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasole, amewatahadharisha wanachama wenye nia ya kugombea uongozi kutotumia mianya ya rushwa kupata nafasi hizo kwa kuwa wakibainika watakatwa.

Mwakasole alitoa kauli hiyo juzi, wakati wa kikao kilichohusisha makada na wanachama wa chama hicho kilichofanyika wilayani Rungwe kikiwa na lengo la kuweka mikakati kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema endapo kuna mwanachama yeyote ambaye amejiandaa kupata uongozi kwa kuhonga aendelee na shughuli zake kwa kuwa chama hakiwezi kumpa nafasi yoyote ya uongozi.

"Chama chetu ni kisafi kinahitaji viongozi wasafi. Hatutaruhusu mianya yoyote ya rushwa kwenye uchaguzi ujao. Kiongozi mzuri atapatikana kwa matendo yake na dhamira ya dhati ya kuwatumikia wananchi na chama alisema," Mwakasole.

Alisisitiza wanachama kutokubali kurubuniwa kwa visenti badala yake wachague kiongozi mwadilifu na mwenye kiu ya kuwatumikia na kuwaletea maendeleo badala ya kumchagua kiongozi anayetaka kujinufaisha.

Aidha, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, aliwataka wanachama wa chama hicho kuwakataa wale wanaowarubuni kwa kuwapa zawadi ili kuwachagua.

Alisema haki hainunuliwi na kwamba wanachama hawana budi kumchagua kiongozi ambaye atazishughulikia changamoto zinazowakabili.

# RC awataka walimu kuongeza ubunifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewashauri walimu kuanzisha shughuli mbalimbali za ujasirimali ili ziwasaidie kujiingizia kipato na kumudu gharama za maisha badala ya kutegemea mishahara pekee ambayo wakati mwingine huchelewa.

Chamila alitoa ushauri huo juzi wakati wa sherehe za kuwapongeza na kutoa zawadi kwa walimu na shule za Jiji la Mbeya zilizofanya vizuri kwenye matokeo ya mitahani ya kitaifa.

Alisema kazi ya ualimu inahitaji ubunifu kwa sababu ya mazingira yake na kwamba ili kumudu gharama za maisha kwa sasa, mwalimu hana budi kufanya shughuli zingine ambazo zitamwingizia kipato.


Alisema baadhi ya walimu hulalamikia serikali kuwa mishahara ni midogo, hivyo waache kufanya hivyo na badala yake wawe wabunifu kwa kuanzisha miradi ambayo itawasaidia kuendesha maisha yao.

Hata hivyo, alisema kauli yake haitoi nafasi kwa walimu kuacha majukumu ya kufundisha badala yake watenge muda wa ziada na kufundisha kufanya shughuli zao. "Maisha sasa yamebadilika si wakati wa kulalamika, lazima ujiongeze kwa kuanzisha miradi mingine ya kujiingizia kipato badala ya kuishia kulalamika. Msitegemee mishahara pekee kwani haiwezi kutatua matatizo yenu," alisema Chalamila.

Aidha, aliwaonya maofisa ambao hutumia madaraka yao kuwakandamiza walimu na kuwataka kimapenzi walimu wa kike bali watumie nafasi zao kutenda haki.

Baadhi ya walimu waliohudhuria sherehe hizo walisema wamewasilisha changamoto ikiwamo maslahi duni na mazingira magumu ya kufundishia na kwamba wanaamini mkuu wa mkoa ataziwasilisha maeneo husika.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, aliwashauri walimu kuungana kuwa kitu kimoja ili waweze kupaza sauti zao. Alisema kupitia umoja wao wataweza kuwasilisha changamoto kwenye mamlaka husika na wataweza kusaidiwa badala ya kila mmoja kupeleka changamoto yake, alisisitiza vyama vya walimu vilivyopo vitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.





# Mchakato waanza ujenzi bandari uvuvi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SEKTA ya uvuvi nchini ipo katika mchakato wa kujenga bandari za uvuvi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa samaki, uchakataji na uuzaji katika masoko ya uhakika ya mazao yake ndani na nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, baada ya kufanya mazungumzo na wafadhili wa mradi wa ujenzi wa bandari ya uvuvi kutoka Korea Kusini, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), Dk. Rashid

Tamatama, alisema kinachosubiriwa ni taarifa ya mkandarasi ambayo ataiwasilisha mwezi ujao.

Dk .Tamatama alisema taarifa hiyo ikiwasilishwa itakuwa imebainisha ni wapi bandari hizo zitajengwa katika mwambao wa Tanga, Mtwara na Zanzibar ikiwamo gharama halisi za ujenzi wake.

Alifafanua zaidi ya kuwa wizara hiyo imeelekezwa kupanua wigo wa uvuvi kwa kujenga bandari za uvuvi na mkakati huo upo ndani ya Mpango wa Maendeleo wa Serikali wa miaka mitano 2016/17-2020/21 na katika Ilani ya CCM ya 2015-2020.

Aliongeza katika kutekeleza mradi huo sekta hiyo imewaalika wafadhili kufika nchini na wamefika na kufanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango baadaye watafanya na wizara husika na watatembelea maeneo ya Pwani na hata Zanzibar.

Alisema sekta hiyo inataka kujenga bandari za uvuvi kwa lengo la kuongeza thamani katika mnyororo mzima wa uzalishaji, uchakataji na usambazaji wa mazao ya samaki katika soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

Alisema nchi hii imejaliwa kuwa na maeneo makubwa ya maji, yakiwamo maji baridi ya maziwa matatu makubwa ambapo inamiliki asilimia 51 ya Ziwa Victoria, asilimia 41 Ziwa Tanganyika na asilimia 18 ya Ziwa Nyasa.

Dk. Tamatama alisema pamoja na kuwa na rasilimali kubwa ya maji, sekta ya uvuvi inatoa mchango mdogo katika pato la taifa, hivyo mkakati wa ujenzi wa bandari za uvuvi utachangia katika kuongeza pato la taifa.

Alisema mwaka 2017 serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, na taarifa itakamilika mwezi ujao, na kuongeza kuwa kwa sasa wizara inatafuta fedha ndiyo maana imewaalika wafadhili kutoka Korea Kusini.

Mkurugenzi wa Sekta ya Uvuvi, Magesa Bulayi, alisema wizara hiyo kupitia sekta ya uvuvi, imejipanga kusonga mbele na kuhakikisha nchi inapata faida kutokana na kuwapo kwa samaki katika maziwa na bahari nchini.

Ili kufanikisha azma hiyo, wizara inaandaa miundombinu ya bandari ambazo zitakuwa chanzo cha uhakika wa upatikanaji wa mazao ya samaki, masoko, kupunguza uvuvi haramu na kuongeza thamani ya mazao ya samaki katika mnyororo mzima wa uchakataji mazao hayo.

Kuanzishwa kwa bandari hiyo, ni fursa muhimu ya kuchakata samaki ambayo kwa sasa imekuwa baadhi ya viungo vinatupwa, na hakuna kitu kitakachotupwa kuanzia ngozi, minofu, mifugo, vichwa, mafuta na bidhaa nyingine.



Meneja Uhusiano Kiongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Eunice Chiume, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akitoa taarifa za utendaji za mfuko huo. Kushoto kwake ni Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa mfuko huo, Rehema Mkamba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Naibu Spika ahimiza misaada kwa makundi yasiyojiweza

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

NAIBU Spika, Dk. Tulia Ackson, amezishauri taasisi mbalimbali za watu binafsi zikiwamo zile za dini ya kiislamu katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuelekeza misaada ya chakula kwa watu wasio na uwezo, vituo vya watoto yatima na wazee.

Ushauri aliutoa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya futari iliyoandaliwa na benki ya NBC tawi la Dodoma jijini hapa.

Pia alizitaka taasisi zinazofuturisha kukaa karibu na jamii isiyo na uwezo katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na wao kutokuwa na uwezo wa kushiriki kwa pamoja kula futari.

Alisema ni vema kwa watu binafsi na taasisi zinazoweza kufanya hivyo zikafikia jamii hiyo ya wasiojiweza kwa kuwapelekea chakula kama vile kwenye makambi ya wasiojiweza.

"Naomba nitumie fursa hii kwa taasisi na watu binafsi wakaelekeza kwenye vituo, hivyo ili waweze na wao washiriki kwa pamoja na jamii hiyo isiyojiweza katika kipindi hiki cha Ramadhani wafuturu kwa kuwa watakuwa wamewakumbuka na wao ambao hawana kipato," alisema.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, alisema suala la kufuturisha ni la imani ya dini ya kiislamu na linastahili kushirikisha na jamii yote ile wakiwamo wenye uwezo na wasio na kipato.

"Ni imani yangu taasisi zingine zitakuwa na utaratibu huu wa kufuturisha kinachotakiwa wasiangalie nani mwenye uwezo na nani asiye kuwa na uwezo, ili kama ikiwezekana basi watu

# TBA yaagizwa ofisi za NEC

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

NAIBU Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Elias Kwandikwa, amewaagiza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kukamilisha mradi wa ujenzi majengo ya ofisi za Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC) kwa wakati ili matokeo ya uchaguzi mkuu ujao yatangaziwe hapo.

Kwandikwa alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa majengo hayo yaliyopo eneo la Njedengwa jijini hapa.

Aliwaagiza TBA kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa majengo hayo kwa wakati, ili tume hiyo iweze kuyatumia majengo hayo kwenye kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu ujao hapo. "Nimetembelea majengo haya yote nimeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wake, hivyo ninawataka kutekeleza makubaliano mliyowekeana na tume ili waweze kuhamia kwenye majengo yao kabla ya uchaguzi mkuu ujao," alisema.

Alisema lengo la serikali ni kuwa tume hiyo iweze kuyatumia kwenye kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu ujao pamoja na uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Hata hivyo alishauri kama kuna changamoto zilizopo kati ya mtekelezaji wa ujenzi wa mradi huo ambao ni TBA wakae na tume ili kasi ya ujenzi iongezeke.


Kaimu Mkurungezi wa Idara ya Ujenzi ya TBA, Humphrey Killo, alisema ujenzi wa majengo hayo unatarajiwa kukamilika Oktoba, mwaka huu na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 13.

Killo alisema ujenzi wa mradi huo unatekelezwa na wakala huyo kwa kujenga majengo yenye sehemu tatu za ofisi za NEC.

Aliitaja sehemu ya kwanza mradi huo ni ya kuhifadhi vifaa vya uchaguzi pamoja na kufunga mifumo ya vyombo vya uchaguzi ambalo limekaribia kuisha na litaanza kutumika muda si mrefu baada ya kukamilika.

Sehemu ya pili ni jengo litakalotumika kutangaza matokeo ya uchaguzi ambalo litajitegemea kwa miundombinu yake.

Sehemu nyingine ni ya jengo la utawala ambalo litatumika kwa wafanyakazi wa ofisi hiyo.



## BARAZA LA WAWAKILISHI



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (kulia), akisalimiana na baadhi ya wakurugenzi wa wizara yake, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. Katikati ni Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake, Suleiman Sarahan Said. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uhaba wataalamu wazorotesha kilimo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imesema kitendo cha kushindwa kupata wataalamu katika sekta ya kilimo kimezorotesha kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa mazao ya matunda na chakula.

Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Makame Ussi, alisema wizara yake ina wataalamu 92 Unguja na Pemba wakati mahitaji halisi ni 172.

Aliyasema hayo wakati akitoa ufafanuzi wa hali halisi ya mahitaji ya mabwana shamba na mabibi shamba waliopo katika wizara hiyo kutoa huduma za wakulima mashambani.

Dk. Ussi alisema mabwana shamba na mabibi shamba waliopo hawatoshi, huku wakulima wakishindwa kufikiwa na wasaidizi hao wa kilimo.

Alisema katika kisiwa cha Pemba yako malalamiko makubwa ya wakulima kushindwa kufikiwa na wataalamu hao wa kilimo kwa ajili ya kupata ushauri na utaalamu juu ya mbinu bora za kilimo.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tunakabiliwa na uhaba wa mabwana shamba na mabibi shamba katika sekta ya kilimo.

Hali hiyo kwa kiasi kikubwa imezorotesha uzalishaji wa kilimo cha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula," alisema.

Alisema upungufu wa mabwana shamba na mabibi shamba 80 ni idadi kubwa na tayari wizara imewasiliana na serikali kuu kwa ajili ya kutoa ajira.

Kwa sasa, alisema suala hilo linashughulikiwa na serikali za mitaa na halmashauri za wilaya kutokana na kugatuliwa kwa sekta ya kilimo.

"Tumewasiliana na Wizara ya Utumishi kwa ajili ya kuajiri mabwana shamba na mabibi wa ziada kukabiliana na pengo kubwa lililopo ili kuleta ufanisi wa sekta ya kilimo," alisema.

# Shule binafsi zaonywa kuhusu mitaala

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema shule za binafsi ambazo zitashindwa kufuata mitaala ya serikali zitachukuliwa hatua za kisheria.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2019/20.

Alisema shule binafsi zinatakiwa kufuata mitaala ya serikali ikiwa ni matakwa ya kisheria kwa mujibu wa sheria za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Alisema mitaala ya wizara inatakiwa ifuatwe na shule zote kwa sababu tayari imekubalika kisheria kwa ajili ya kutumika kwa wanafunzi wa shule zote.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wamiliki wa shule binafsi wote kwamba wanatakiwa kufuata mitaala ya Wizara ya Elimu kwa mujibu wa sheria ambayo tayari imepitiwa na kukubalika kutumikwa kwa wanafunzi wote," alisema.

Aidha, alisema tayari wizara imekamilisha mpango wa kupeleka huduma za elimu ya msingi kwa serikali za mitaa katika mpango wa ugatuzi.

Alisema kwa mujibu wa sheria elimu ya msingi na maandalizi iko katika ugatuzi na kutekelezwa na halmashauri za wilaya.

Naibu Waziri alisema makabidhiano ya ugatuzi kwa upande wa elimu yamekamilika na maslahi ya walimu wote waliokuwa wakifanya kazi katika shule ya msingi na maandalizi yapo katika Halmashauri za Wilaya.

"Mheshimiwa Spika Wizara ya Elimu imekamilisha mambo yote ya maslahi kwa walimu wa msingi katika utekelezaji wa mpango wa ugatuzi kufikisha huduma muhimu za elimu kwenda kwa halmashauri za wilaya," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2019/20. Katika makadirio hayo, Sh. 178,917,149,000 zitatumika kwa kazi za kawaida na maendeleo.

# Wawakilishi wapigia debe wataalamu wa Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuandaa wataalamu wa lugha ya Kiswahili ili kufundisha ndani na nje ya nchi.

Waliyasema hayo katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi wakati wakichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa wizara hiyo kwa mwaka 2019/20.

Walisema kufanya hiyo kutasaidia vijana kupata fursa ya ajira na kuitangaza Zanzibar kupitia lugha hiyo ambayo inasifa katika nchi mbalimbali.

Mwakilishi wa Magomeni, Rashid Makame Shamsi, alisema iwapo vyuo vikuu vitatoa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kutapunguza matumizi mabaya ya lugha hiyo ambayo kwa sasa ndiyo lugha mama ya taifa.

Wakizungumzia kuhusu vyoo vinavyotumiwa na wanafunzi, walisema baadhi ya shule hasa za zamani vyoo vyake viko katika hali mbaya, hivyo kuna umuhimu wa kujenga vyoo vya kisasa ambavyo vitatumika pia na watu wenye mahitaji maalumu.

Mwakilishi wa Viti Maalum, Viwe Khamis Abdalla, alisema pamoja na kuwa shule nyingi zinazojengwa na serikali kunakuwapo na vyoo, bado havijazingatia uwapo wa watu wenye mahitaji maalum.

Naye, Mwakilishi wa Chaani, Nadir Abdul-latif Yussuf, aliiomba serikali inapotoa ajira katika wizara hiyo kuangalia walimu waliojitolea kwa muda mrefu kuwaajiri ambao wameshapata uzoefu katika kada ya ualimu.

Hata hivyo, aliishauri wizara kuweka miundombinu ya usafiri kwa walimu wanaosomesha mashamba ili kuondosha changamoto hiyo hasa wanaofundisha maeneo ya mbali hasa mashambani.

# Serikali yawashukuru wadau wa maendeleo

**Na Mwandishi Maalum**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, amewashukuru wadau wa maendeleo kwa kuisaidia serikali kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma iliyosaidia kuongeza tija katika ukuaji wa uchumi wa nchi na utoaji huduma bora kwa wananchi.

James ametoa shukrani hizo jijini Dodoma wakati wa kikao cha mwisho kwa mwaka wa fedha 2018/2019 cha wadau wa maendeleo na serikali kilichojadili maendeleo ya utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Tano (PFMRP-V) ambao utekelezaji wake umeingia mwaka wa pili na unaotarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2021/2022. Programu ya Maboresho na Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Tano, utagharimu Sh. bilioni 152.3 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai mwaka 2017 hadi Juni, 2022, ambapo unatarajia kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya serikali na kudhibiti mianya yote ya matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili cha utekelezaji wake umeonyesha mafanikio makubwa ikiwamo usimikaji wa mifumo zaidi ya saba ya kielektroniki ya kukusanya na kudhibiti mapato ya serikali.

"Mifumo hii ukiwamo mfumo wa GePG umesaidia sana kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya serikali pamoja na kodi, imeongeza udhibiti wa matumizi, misamaha ya kodi na kusaidia upelekaji wa rasilimali fedha kwenye miradi ya kipaumbele ya kitaifa na hatimaye kusaidia usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisema James.

"Wizara ya Fedha na Mipango imejipanga kuendeleza kazi nzuri za program, ili kuendelea kuunga mkono ajenda ya Rais John Magufuli katika kusimika mifumo na maboresho ya uhakika katika kusimamia fedha za umma. Hatua hii itachochea maendeleo ya kiuchumi yanayowagusa Watanzania wote."

Mwenyekiti mwenza wa kundi la washirika wa maendeleo wanaofadhili PFMRP-V, Trine Lunde, alielezea kuridhishwa kwao na namna Tanzania inavyotekeleza na kusimamia programu hiyo ambayo amesema imeleta tija katika usimamizi wa fedha za umma nchini.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (kushoto), akipewa zawadi ya fimbo baada ya kuvishwa vazi aina ya kikoi ikiwa ni ishara ya kumpongeza kwa utendaji kazi wake mzuri katika uhifadhi wa wanyamapori, wakati wa mkutano kati ya wenyeviti wa Muungano wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori nchini (WMAs) na wizara hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: WMU**

# Wananchi wafufua ujenzi shule uliosimama miaka 12

**Na Sabato Kasika**

WAKAZI wa Kijiji cha Mikuyu, Kata ya Nyamulandirira, Musoma Vijijini mkoani Mara, wamefufua ujenzi wa shule yao ya msingi uliosimama takribani miaka 12 kutokana na sababu ambazo ziko juu ya uwezo wao.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mikuyu, Raban Kakengera, amesema ujenzi wa shule hiyo ulisimama mwaka 2007 katika kitongoji cha Mtakuja na sasa umeanza upya ili watoto waanze masomo Januari mwaka ujao.

Aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu jana kuwa wakazi hao wameanza kujenga boma lenye vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu kwa ajili ya shule hiyo itakayoitwa Karusenyi.

"Wamefikia uamuzi huo baada ya kugundua kuwa kwa sababu kuu inayochangia ufaulu mdogo wa watoto wao ni kutembea umbali mrefu kufuata elimu," alisema Kakengera.

Alisema watoto wamekuwa wakitembea umbali wa kilometa kati ya tano hadi nane kwenda katika Shule ya Msingi Mikuyu, ilioko kitongoji cha Miembeni, hivyo sasa wameona kuna haja ya kuendelea kujenga shule yao.

"Wamedhamiria kwamba ifikapo Januari 2020, watoto wa darasa la kwanza waanze masomo, huku wakiendelea na ujenzi wa vyumba vingine zaidi hadi iwe na darasa la saba," alisema.

Alisema, ombi la wakazi wa kitongoji hicho ni kwamba waungwe mkono na wadau wa maendeleo, ili waweze kukamilisha haraka ujenzi huo kwa vile wanahitaji vifaa vya ujenzi ikiwamo saruji na nondo.

"Bahati nzuri Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, ni miongoni mwa wadau hao, ambaye tayari ameahidi kuchangia saruji atakapofanya ziara jimboni hivi karibuni," alisema.

Kakengera alisema ana uhakika na ahadi ya mbunge huyo kwa vile amekuwa akijitolea kwa hali na mali kuhakikisha jimbo lake linakuwa juu katika elimu, kilimo na afya.

## NEC yamwaga ajira za muda

**Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza nafasi za kazi za muda kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Wapigakura.

Kwa mujibu wa tangazo la maombi ya ajira hizo lililosainiwa na Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi, Mabamba Rajabu Moses, Watanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na wasiozidi miaka 45 wametakiwa kuomba.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, sifa zingine za waombaji ni kuwa na elimu ya kidato cha nne na kuendelea na awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.

"Awe na uwezo wa kutambua matatizo ya kompyuta ya hardware na software na kuyatatua," ilisema sehemu ya tangazo hilo na kuongeza kuwa:

"Awe na uwezo wa ku-istall (kuingiza) programu za kompyuta na kutoa msaada wa kuifundi wa Tehama kwa watumiaji. Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai na awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yenye usimamizi mdogo."

## Uhamiaji Sirari walia watumishi

**Na Anthony Gervas,** TARIME

IDARA ya Uhamiaji kituo cha Sirari wilayani Tarime mkoani Mara, inakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa watumishi pamoja na magari ya kufanyia doria.

Mrakibu Mwandamizi wa kituo hicho, Joseph Kasike, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuwapo kwa njia nyingi za panya, zilizobainika kutumiwa na wahamiaji haramu wanaoingia nchini na kuishi bila vibali kinyume cha sheria.

"Idara yetu ya Uhamiaji inakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa watumishi pamoja na magari ya kufanyia doria ambayo hayatoshelezi kutokana na kuwapo kwa njia za panya zaidi ya 50, zinazoingia Tanzania kutoka Kenya," alisema Kasike.

Kasike alisema kutokana na upungufu huo, wa watumishi na magari ya kufanyia doria ambayo kwa sasa yapo mawili katika kituo hicho, hivyo hayawezi kutosheleza mahitaji ya kupambana au kudhibiti wahamiaji haramu kwa kiwango kinachotakiwa wanaoingia nchini kupitia njia hizo.

Alisema changamoto nyingine inayochangia kuwapo kwa wahamiaji haramu nchini ni mwingiliano wa koo za makabila kutoka Tanzania na Kenya, ambazo zipo pande zote mbili, hivyo kuchangia kukumbatiana badala ya kuwafichua wahamiaji hao wanaoingia na kujificha.

Aidha, alisema kuwa idara inahitaji kutoa elimu zaidi kwa wananchi wa mpakani, ili waweze kutoa ushirikiano wa kuwafichua wakiwamo wanaotumia njia za panya kupitisha magendo.

HABARI KIMATAIFA

# Tshisekedi kuzikwa kishujaa DRC

**KINSHASA,** Congo

MWILI wa kiongozi wa zamani wa upinzani, Etienne Tshisekedi, baba mzazi wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, uliwasili jana nchini ikiwa ni miaka miwili baada ya kifo chake.

Tshisekedi alifariki dunia Februari mwaka 2017 mjini Brussels nchini Ubelgiji, akiwa na umri wa miaka 84, lakini mwili wake uliendelea kubaki mjini humo kutokana na kuwapo kwa wasiwasi wa kisiasa kupitia utawala wa Rais wa zamani wa taifa hilo, Joseph Kabila.

Kwa mujibu wa Askofu Gerard Mulumba, baada ya mwili huo kutua uwanja wa ndege, utasafirishwa kuelekea Viwanja vya Mashahidi kwa maombolezo.

**Tayari maandalizi katika uwanja huo ikiwamo ujenzi wa jukwaa umekamilika, maofisa wa polisi wataongoza gwaride la heshima za mwisho.**

"Tayari maandalizi katika uwanja huo ikiwamo ujenzi wa jukwaa umekamilika, maofisa wa polisi wataongoza gwaride la heshima za mwisho," anasema.

Pia amesema takribani marais watano wa Bara la Afrika wamethibitisha kuhudhuria mazishi yake.

"Ni zaidi ya miaka miwili tangu tulipoanza kutumia kila njia kuusafirisha mwili wake," anasema Askofu Mulumba na kuongeza, "Na sasa kwa kuwa hali iko shwari tunashukuru."

Akiwa mwanasiasa wa muda mrefu, Tshisekedi alihudumu katika upinzani kwa miongo kadhaa, lakini hakufanikiwa kuiongoza nchi hiyo.

Alikuwa mkosoaji mkubwa wa aliyekuwa dikteta Mobutu Sese Seko, alianzisha chama cha Union for Democracy and Special Progress UDPS mwaka 1982 baada ya kuachiliwa kutoka jela.

Mwaka 1997, baada ya Mobutu kuondolewa madarakani na kundi lililoongozwa na Laurent Kabila, Tshisekedi alianza kuwa mpinzani wa utawala mpya, msimamo aliokuwa nao hata baada ya mauaji ya Kabila 2001, huku mwanawe Joseph akipanda katika hatamu za uongozi.

Baada ya kushindwa katika uchaguzi wa 2011 uliodaiwa kukumbwa na udanganyifu mkubwa, Tshisekedi alikataa kutambua utawala wa Kabila hadi kifo chake.

Ikiwa imepita miaka miwili baada ya kifo chake, Januari 24, mwaka huu mtoto wake, Felix aliapishwa kuwa Rais mpya wa Congo ikiwa ni miaka 18 ambayo Kabila alikuwa madarakani.

Uchaguzi huo ulikumbwa na madai mengi ya udanganyifu, huku siasa za taifa hilo bado zikitawaliwa na Kabila ambaye alijipatia umaarufu mkubwa akiwa madarakani.

Jumatatu, Rais Tshisekedi alimteua mwanasiasa wa muda mrefu, Sylvestre Ilunga Ilunkamba, kuwa Waziri Mkuu. **BBC**

## Aliyezaliwa na uzito mdogo atoka hospitali

**WASHINGTON,** Marekani

MTOTO Saybie aliyezaliwa akiwa na uzito wa gramu 245 ambaye aliaminiwa kuwa ndiye mtoto mwenye uzito mdogo zaidi wa mwili duniani kuwahi kuzaliwa, ameruhusiwa kuondoka hospitalini nchini Marekani.

Saybie baada ya kuzaliwa mwezi Desemba mwaka jana katika wiki ya 23 ya ujauzito akiwa na uzito sawa na ule wa tofaa, alipelekwa kwenye kituo cha tiba ya dharura hospitali ya Mary Birch mjini San Diego, California ambako madaktari waliwaambia wazazi wake kuwa mtoto huyo ana saa kadhaa tu za kuishi.

Hata hivyo, miezi mitano baadaye ameweza kuruhusiwa kuondoka hospitalini akiwa mwenye gramu 2.5, akiwa mwenye afya tele, kinyume na matarajio. Muuguzi ambaye alimuhudumia Saybie wakati alipokuwa akipigania uhai wake alisema kuwa kuishi kwake na kuruhusiwa kwenda nyumbani ni 'muujiza'.

Taasisi ya usajili ya watoto wenye mwili mdogo zaidi inadhani Saybie ndiye mtoto kijusi mwenye mwili mdogo zaidi ambaye ameweza kunusurika na kifo.

Kwa mujibu wa taasisi ya usajili wa watoto wenye umri mdogo zaidi yenye makao yake katika Chuo Kikuu cha Iowa nchini Marekani, rekodi ya awali ya mtoto aliyezaliwa akiwa na mwili mdogo zaidi, ilikuwa inashikiliwa na msichana kutoka Ujerumani ambaye alizaliwa mwaka 2015 akiwa na gramu 252.

Mtoto mchanga aliyezaliwa akiwa na uzito wa gramu 268 nchini Japan mapema mwaka huu anakisiwa kuwa ndiye mvulana aliyeweza kuishi baada ya kuzaliwa kama kijusi chenye uzito mdogo zaidi duniani.

Mama yake Saybie alijifungua kwa njia ya upasuaji 'C-section' miezi mitatu kabla ya muda wake wa kujifungua haujafika. Ktika video iliyotolewa na hospitali, mama yake alielezea kujifungua mtoto wake kama "siku ya kutisha zaidi katika maisha yake".

"Nilikuwa kila mara ninawaambia: Atanusurika ndiyo nina wiki 23 tu za ujauzito," alisema mama huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe. **BBC**



Waziri Mkuu wa Fiji, Frank Bainimarama, akihudhuria mkutano wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi mjini Nairobi, Kenya, ambapo alipata fursa ya kumtembelea Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta. Wakenya washangazwa na suti yake ya sketi na viatu vya wazi (sandozi). **PICHA: BBC**

## Trump awagawa Wabunge Democrats

**WASHINGTON,** Marekani

WANASIASA watatu wa juu wa chama Democrats wametoa wito wa kuanzishwa mchakato wa kumuondoa madarakani Rais wa Marekani, Donald Trump.

Uamuzi huo umetolewa saa chache baada ya aliyekuwa kiongozi wa timu ya wachunguzi iliyokuwa ikichunguza kama Urusi iliingilia uchaguzi mkuu wa Marekani wa 2016.

Akizungumza juzi kwa mara ya kwanza, Robert Mueller ambaye alipewa jukumu la kuchunguza sakata hilo, amesema uchunguzi walioufanya haukumfutia hatia Rais Trump ya kukiuka sheria.

Kwenye hotuba yake, Mueller alisema suala la kumfungulia mashtaka Rais aliyeko madarakani halikuwa ni suala lililoko mezani kwa wakati ule.

Suala la mchakato wa kumuondoa Trump madarakani limewagawa wabunge wa chama cha Democrats, ambapo baadhi wamejitokeza kuongeza shinikizo kwa Spika wa Bunge, Nancy Pelosi, ambaye hajakubali kuanzisha mchakato huo.

Matamshi ya Mueller sasa yamewaibua wagombea wengine watatu wanaoomba kuchaguliwa na chama chao kuwania urais kwenye uchaguzi mkuu ujao, wakifanya idadi yao kuwa 10 ya wanaotaka mchakato wa kumuondoa Trump uanze.

Rais Trump kwa upande wake ameendelea kusisitiza kutokuwa na hatia akisema sheria zilizopo haziruhusu Rais aliyeko madarakani kushtakiwa na hivyo mjadala wa Mueller umefungwa rasmi. **RFI**

## Netanyahu asalimu amri uchaguzi

**TEL AVIV,** Israel

BUNGE la Israel jana, lilipiga kura kuruhusu kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu mpya baada ya Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, kushindwa kuunda serikali na vyama vingine.

Uamuzi wa Bunge umekuja ikiwa ni mwezi mmoja tu tangu nchi hiyo ifanye uchaguzi wake mkuu, uliooshuhudia Waziri Mkuu Netanyahu na chama chake cha Likud kikishindwa kupata ushindi wa jumla kuwawezesha kuunda serikali.

Hatua hii imekuja pia baada ya muda wa mwisho aliokuwa nao, Netanyahu wa kuunda serikali kupita baada ya majuma kadhaa ya mazungumzo na vyama vingine kugonga mwamba.

Uamuzi wa Netanyahu kukubali kuitisha uchaguzi mkuu mwingine, kumezuia Rais, Reuven Rivlin, kuchagua mtu mwingine kujaribu kuunda serikali, lakini hata hivyo uamuzi wake unazidisha sintofahamu zaidi ya mustakabali wake kisiasa.

Haya yanajiri wakati huu, Netanyahu anapambana kusafisha jina lake kutokana na kashfa za rushwa, ambapo tayari kulikuwa kumeanza mchakato wa chini kwa chini kujaribu kumuondoa madarakani. **RFI**

# Wanafunzi 26 wapewa ujauzito miezi mitatu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KASI ya wanafunzi kuendelea kupewa ujauzito katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, imezidi kuwa kubwa baada ya kubainika kuwa ndani ya miezi mitatu wanafunzi 26 wameacha masomo kutokana na tatizo hilo.

Wanafunzi hao wamepewa ujauzito ndani ya mwaka huu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu katika shule za sekondari 23.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Ustawi wa Jamii wa halmashauri hiyo, Elizabeth Mweyo, kwenye kikao cha wenyeviti wa vitongoji katika Kata ya Usanda kilichoandaliwa na Shirika la Agape kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutokomeza matukio ya ukatili kwa wanawake na watoto.

Alisema tatizo la wanafunzi kuendelea kupewa ujauzito na kuacha masomo katika halmashauri hiyo limeonekana kuwa kama jambo la kawaida kutokana na jamii yenyewe kukubaliana na hali hiyo.

Mweyo alisema kushamiri kwa vitendo hivyo kunatokana na jamii kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati kwa kutomthamini mtoto wa kike na kumwona kama kitega uchumi cha familia.

"Tatizo la mimba za wanafunzi kwenye halmashauri yetu hali inakoelekea ni kubaya sana. Kwa mwaka huu tu ndani ya miezi mitatu, wanafunzi 26 wameshapewa ujauzito na kuacha masomo yao. Ukiwafuatilia wahusika wa mimba hizo huwaoni, jamii ina waficha ili wasikamatwe lengo wapate mali ya mifugo," alisema Mweyo.

"Kwa hali hii nyie wenyeviti wa vitongoji ambao mnaishi na wananchi kwa ukaribu zaidi naombeni tushikamane mlikemee suala hili pamoja na kuwakamata wahusika wa mimba hizi, ili tupate kuwashughulikia kisheria na kuwafungwa jela ndipo tutafanikiwa kulipunguza tatizo hili au kulikomesha kabisa," aliongeza.

Pia aliwataka wazazi kuachana na tabia ya kutomthamini mtoto wa kike bali wawapatie elimu kama wa kiume ili watimize ndoto zao na watakuja kuwasaidia hapo baadaye pamoja na kuwanunulia mifugo mingi ambayo ndiyo imekuwa kizingiti kwa kuharibu maisha yao.

Nao baadhi ya wenyeviti wa vitongoji akiwamo John Matanda wa Manyada, walikiri tatizo la kuficha watuhumiwa wanaohusika kuwapatia mimba wanafunzi lipo kwa madai ya kuogopa lawama ndani ya jamii.

Kutokana na hali hiyo, wazazi huamua binti atolewe mahari ya ng'ombe kuanzia 20 hadi 25, ili aolewe na kesi kuishia hapo.

Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Afya ya Uzazi na Jinsia kutoka Agape, linalotetea haki za wanawake na watoto mkoani Shinyanga, Lucy Maganga, alisema changamoto ambayo wanakabiliana nayo kutokomeza mimba na ndoa za ututoni ni jamii kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati kwa kutomthamini mtoto wa kike.



Balozi wa Finland nchini, Pekka Huka (kulia), akipokea kinyago kutoka kwa Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa Kitengo cha Wanawake (UN Women) nchini, Hodan Addou, wakati wa chakula cha jioni kilichoandaliwa na umoja huo, jijini Dar es Salaam juzi. Balozi Hukka amekuwa akisaidia miradi ya 'Wanawake Wanaweza'. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Walipakodi sasa waitwa kueleza kero

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetoa wito kwa wananchi kutembelea ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) zilizopo katika maeneo yao na kuhudhuria vikao vinavyoitishwa na wakuu wa mikoa na wilaya, ili kuwasilisha maoni na kero zao zinazohusu kodi.

Wito huo ulitolewa Bungeni jana jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, Jaku Hashimu Ayoub, aliyetaka kujua ni lini TRA itakaa na wafanyabiashara kusikiliza vilio vyao kwa kuwa kila mkoa una ofisi za mamlaka hiyo.

Dk. Kijaji alisema TRA ina ofisi katika mikoa yote ya Tanzania pamoja na baadhi ya wilaya zake, na baadhi ya mikoa ina vituo maalum vya huduma za kodi, hususani Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Pia kila mkoa una mwanasheria na ofisa elimu ya kodi kwa ajili ya kutoa elimu, kusikiliza na kutatua kero za walipakodi.

"TRA imeweka utaratibu kwa meneja wa mikoa ya kikodi kukutana na walipakodi kila Alhamisi ili kusikiliza kero zao na kuzitatua, hatua ambayo ina lengo la kujenga imani , kutatua kero na kukuza ridhaa ya ulipaji kodi kwa hiari", alieleza Dk. Kijaji.

Alisema kuwa miongoni mwa kazi za kila siku za TRA ni kusikiliza na kutatua kero za wafanyabiashara ili kuwawezesha kufanya biashara zao bila usumbufu, hivyo hufanya biashara katika ngazi ya wilaya, mikoa na Taifa ili kutoa elimu, na pia hurusha vipindi maalum katika runinga na redio kuhusu elimu ya kodi kwa wananchi na kujibu kero za wafanyabiashara.

Dk. Kijaji alieleza kuwa wenyeviti wa kamati za mapato za mikoa na wilaya ambao ni wakuu wa mikoa na wilaya wamekuwa wakisikiliza kero za walipakodi kwa kushirikiana na TRA na kwamba mamlaka hiyo hubuni na kuanzisha mifumo, vituo na vilabu rafiki vya kikodi ili kujibu vilio vya wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla.

# TPDC kuchimba kisima cha kwanza mafuta 2019/20

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli TANZANIA (TPDC), linatarajia kuchimba kisima cha kwanza cha mafuta nchini, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma hiyo nchini katika mwaka ujao wa fedha.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Kapuulya Musomba, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka 50 ya shirika hilo ambayo yataambatana na maonyesho yatakayofunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa leo, Jiji Dar es Salaam.

Alisema wanataka wachimbe kisima cha kwanza na kwamba visima vingi vilikuwa vikifanywa na kampuni za nje na zingine walifanya kwa kushirikiana nayo.

"Tumeona tufanye sisi kama TPDC. Tumefanya maandalizi, lakini tunaamini tutaweza kuchimba visima vingine mwaka mmoja, miaka miwili na sisi tuwe na kitalu cha kwetu kama TPDC," alisema.

Alisema serikali imeshatenga vitalu ambavyo wanatakiwa kuviendeleza na si waishie Tanzania tu bali wapate nafasi kwenda nchi zingine.

"Kazi nyingine tunayoiona wenzetu walikuwa wanaagiza mafuta, lakini sasa tunataka kufanya biashara ya mafuta katika maana ya TPDC kuagiza mafuta kutoka nje na kuleta hapa nchini," alisema.

Alibainisha kuwa tangu mwaka 2015 wameambiwa na serikali liwe shirika la biashara.

Aidha, alisema shirika hilo linajivunia kufanya mambo mengi ikiwamo ugunduzi wa gesi katika eneo la Songosongo mkoani Lindi na kazi waliyoifanya ni kujenga bomba kubwa la gesi la kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

"Ukamilishaji wa bomba kubwa la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam limetupa msingi mkubwa. Kazi kubwa tuliyo nayo ni kusambaza gesi nchi nzima. Hii ndiyo kazi kubwa tunayoiona kwa miaka 50 ijayo na tumeanza kwa kiasi Dar es Salaam na usanifu unaendelea kwa Tanzania nzima," alisema.

Akizungumzia mafanikio na changamoto, Musomba alisema Juni, 2016 walichukua TPDC likiwa na hasara ya Sh. bilioni 340 na wakaweka mikakati na kupunguza hasara hiyo na kufikia takriban Sh. bilioni 50, mwaka jana.

Alisema mpango wa sasa hivi wanaamini watapata faida ya kutosha kwa kuwa hasara waliyokuwa wanaipata inatosha.

Kadhalika, alisema nusu ya eneo la Tanzania inaweza kupatikana mafuta na gesi na hadi sasa wameshaangalia chini ya theluthi moja.

"Kwa miaka 2010 Mungu ametubariki eneo la baharini tumegundua gesi wenzetu walioweka misingi kuna futi za ujazo karibu trilioni 57.54 na tunategemea kujenga gesi kimiminika ambayo tutauza zaidi ya Tanzania," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836

## MAGARI NA VIPURI


**CRANE FUSO FOR SALE, 1.** Fighter 2002, SAKAI_304, 3 stages, New in TZ, 2. Magnum 1991, TANADO_290, 2 Stages, 3 years in TZ. Dalali Hatakiwi Simu 0692 469 669


NIPASHE
NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**Sultani Ally Mohamed** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo : Cha kidato cha nne chenye index namba S.0671-0129 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2006 katika shule ya Ubungo Islamic High School, na cheti cha Elimu ya Juu chenye namba DSM/BAC/13/12376 kilichotolewa Tanzania Institute of Accountancy mwaka 2017.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: KJN/RB/1800**
**Polisi Taarifa: KJN/RB/2065**

115253802

## KUPOTEA KWA CHETI



**Halima M. Ally** anatangaza kupotelewa na vyeti vya kidato cha nne vifuatavyo: chenye index namba **P0577/0123** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1995 katika shule ya Sekondari Nurulyakin Muslim Seminary na cheti chenye index namba **S.0340/0028** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa lenye mwaka 1994 katika shule ya Sekondari Popatlal.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: UD/RB/1245/2019**

115253902

## KUPOTEA KWA KADI

**Mohamed Ally Luziga** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba T476 DFV aina ya TOYOTA BREVIS, yenye chasis namba JCH100054499.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: KJN/RB/33054/2019**

115254402

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na: 29 YA MWAKA 2019**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ALICE JUSTIN SHOO ..........................MUOMBAJI**

**JUSTINE SHITRAEL SHOO.........................MAREHEMU**

**TAARIFA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya Usimamizi wa Mirathi kwa waombaji/muombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi wa 07 2019.

Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 29 mwezi wa 05 2019

115254102

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**

**SHAURI LA MAOMBI NA 15/2019**
**(asilia shauri la madai Na. 15/2017)**

**MORY TRANSPORT AGENCY..........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **MINZA JOSEPH MWANDU**
2. **YASIN MOHAMED**
3. **ATHMAN**
4. **KURWA.......................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: MINZA JOSEPH MWANDU**
**NA WENZAKE WA MWANZA AU POPOTE MLIPO**

**WITO WA SHAURI**

Mahakama inakufahamisha kwamba wadai hapo juu wamefungua shauri la maombi dhidi yenu, nakala yake inapatikana katika mahakama hii.

shauri la maombi dhidi yenu limepangwa kutajwa mnamo tarehe 05/06/2019 saa 2.30 asubuhi na mnatakiwa kuwepo, au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wenu dhidi ya maombi haya.

zingatia kwamba kutofika kwenu tarehe hiyo shauri litapangwa kusikilizwa bila ya nyie kutaarifiwa tena na maamuzi kutolewa.

imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 22/05/2019.

115256302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER NG'WINZALUBI MBOJE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 403 DDZ TOYOTA NOAH.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KBA/RB/4507/2019.**

115255802

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.35 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late ONESMO ASANI MUHEMBANO of Mkalama Kikuyu South within Dodoma City Council.**
**In the matter of the Application for letters of Administration by LYNDALL ONESMO MUHEMBANO**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 29TH day of MAY, 2019.

THE WILL OF THE SAID DECEASEDIS DEPOSITED AND OPEN FOR INSPECTION OF THE COURT.

DATE ......10....... DAY OF.........5......2019

11525572

**IN THE RESIDENT COURT OF TANZANIA**
**AT TANGA**
**CIVIL CASE NO 17 OF 2018**
**ANTHONY STEPHEN KINGAZI .....................APPLICANT**

**VERSUS**
**BAKARI ALLY @ BAKARI ALFAN, KITOGO @ BAKARI KITOGO..................RESPONDENT**
**TO: BAKARI ALLY @ BAKARI ALFAN, KITOGO @ BAKARI KITOGO**

**NOTICE OF HEARING/MENTION/MEDIATION/PTC**

**TAKE NOTICE** that the above case/appeal will be **MENTION** by the Resident Court of Tanzania, at Tanga on 13th day of June 2019 at 8.30 O'clock in the forenoon/ afternoon.

You must produce on that day all the documents upon which you fated to rely in supporting of your case.

**ALSO TAKE NOTICE** that in default of your nonappearance on that day the case will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my hand and seal of the Court this 20th Day of May 2019.

115255602


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# OBAMA AMPA NENO MESSI NA ARGENTINA



**NEW YORK,** Marekani

ARGENTINA inashindwa kutwaa Kombe la Dunia licha ya kuwa na Lionel Messi kwa sababu hawachezi kama timu, kwa mujibu wa rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama.

miamba hao wa Marekani Kusini wameshinda mara mbili taji la Kombe la Dunia, lakini wameshindwa kuongeza tangu walipotwaa mara ya mwisho mwaka 1986, licha ya kuongozwa na mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Messi.

Argentina ambayo imetinga fainali ya Copa America mara mbili mfululizo ilimaliza nafasi ya mtoano wa 16 bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana na walitinga fainali miaka minne iliyopita nchini Brazil.

Obama, ambaye alikuwa rais wa Marekani kuanzia mwaka 2009 hadi 2017 kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Donald Trump, alizungumza hayo Jumanne wiki hii.

"Hata watu wenye akili kubwa huwa wanafanya kazi na watu wa kawaida ili kuweza kutimiza malengo na kupata maendeleo," alisema Obama jijini Bogota nchini Colombia.

"Kwa Argentina, hata Messi ni mtu wa ajabu, lakini wana matatizo ya kushinda kombe la Dunia."

"Ushauri wangu kwa watu vijana ni kwamba wanatakiwa kuwatambua watu wote ili kufikia mafanikio, ni wachache wanaofanikiwa wakifanya mambo kivyao," aliongeza kusema Obama.

Kauli ya Obama imekuja wakati Messi na Argentina wakijiandaa kushiriki kwenye michuano ya Copa America inayofanyika mwezi ujao huko Brazil.

Argentina imepangwa Kundi B, pamoja na Colombia, Paraguay na wageni Qatar.

# *Lukaku kupunguza mshahara atue Inter Milan*

**MANCHESTER,** England

ROMELU Lukaku yupo tayari kushusha mshahara wake ili akajiunge na Inter Milan ya nchini Italia kwa mujibu wa Sky Sport.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa akiwaniwa na Inter Milan baada ya kuona mambo magumu pale Manchester United.

Maisha ya kucheza soka bila ya kuwapo kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, michuano inayojumuisha mastaa wa maana yanasumbua vichwa vya wachezaji hao.

Msimu ujao, United haitakuwapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, jambo linalomfanya Kocha Ole Gunnar Solskjaer kuwa na wakati mgumu katika kusajili wachezaji wa maana.

Kila mchezaji wa maana anataka akajiunge na timu itakayompa nafasi ya kucheza katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na hilo ndio jambo linalochangia Lukaku kutaka kuondoka hapo United ambayo inahitaji kuwa na pauni milioni 500, ili iwe na nguvu za kuchuana na Manchester City na Liverpool msimu ujao.



# Dias akaribia kutua United



**LONDON,** England

MANCHESTER United imechemsha katika mbio za kumnasa beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly na sasa imehamia kwa mlinzi mahiri wa Benfica na Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Dias ambaye anaweza kupatikana kwa bei nafuu zaidi.

United waliweka mezani dau la pauni milioni 85 kwa ajili ya Koulibaly wiki iliyopita, lakini klabu hiyo ya Italia ililitosa dau hilo huku Real Madrid nao wakiingia katika mbio za kumwania staa huyo wa kimataifa wa Senegal, jambo lililowafanya Manchester United kuachana na suala la kusaka saini ya beki huyo matata kwa sasa.

Kutokana na ushindani huo, United sasa imeelekeza nguvu zake kwa Dias ambaye ni mmoja kati ya mabeki imara wa kati katika soka la Ulaya kwa sasa na kuna uwezekano mkubwa wakampata kwa nusu ya bei ambayo walitazamiwa kutoa kwa Koulibaly.

Kocha wa United Ole Gunnar Solskjaer amekuwa kwenye mpango wa kukiunda upya kikosi chake kwa ajili ya mapambano ya msimu ujao.

# Martinez kumng'oa Valverde Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

KUNA dalili za kibarua cha kocha Ernesto Valverde `kuota nyasi' kufuatia kitendo cha Barcelona kuamua kuwasiliana na Roberto Martinez.

Gazeti la Sport limedai kuwa viongozi wa Barcelona wamezungumza na Martinez, ambaye kwa sasa anainoa Timu ya Taifa ya Ubelgiji.

Viongozi wa Barcelona inasemekana wanataka kuachana na Valverde baada ya kuchukizwa na matokeo ya karibuni ya timu hiyo, licha ya kutwaa ubingwa wa La Liga.

Barcelona ilitolewa katika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Liverpool.

Barcelona ilishinda mchezo wa kwanza mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Nou Camp lakini ilibweteka na kupigwa mabao 4-0 ugenini katika mchezo wa marudiano licha ya Liverpool bila kuwa na mastraika wake tegemeo, Mohamed Salah na Roberto Firmino.

Pia majuzi imelizwa katika fainali ya Copa del Rey baada ya kulala kwa Valencia mabao 2-1.

Uongozi wa Barcelona umepanga kumtimua Valverde na wanataka Martinez achukue nafasi hiyo haraka.

Makocha wengine wanaotakiwa na Barcelona ni pamoja na Unai Emery wa Arsenal na Max Allegri, ambaye aliachana na Juventus hivi karibuni.



# SARRI MAMBO SAFI JUVENTUS



**LONDON,** England

KOCHA, Maurizio Sarri, ambaye ametwaa Kombe la Ligi ya Europa msimu huu akiwa na Chelsea, inasemekana ameshafikia muafaka wa kujiunga na Juventus kwa ajili ya kuinoa timu hiyo katika msimu ujao wa mwaka 2019/20.

Juventus inataka kumchukua Sarri kutoka Chelsea ili kurithi mikoba ya Massimiliano Allegri, ambaye anaondoka mwishoni mwa msimu huu.Sarri amebakiza miaka miwili katika mkataba wake wa kuinoa Chelsea, ambayo haijaweka wazi mustakabali wake.

Chelsea ilimchukua Sarri kutoka Napoli, ambayo ilikuwa inamlipa mshahara wa pauni milioni 5.4 kwa mwaka.

Juventus sasa ipo tayari kumwongezea kiasi cha pauni milioni 1.2 katika mshahara wake wa sasa, ambapo inasemekana Sarri amekubaliana nao.

Viongozi wa Juventus wana kazi ya kukubaliana na Chelsea ili kumalizana.

Hata hivyo, Juventus inatajwa pia kumfuatilia kocha wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino.

Hata hivyo, kuna ugumu wa kumpata Pochettino kwa kuwa klabu yake ya Tottenham Hotspur haitakuwa tayari kumwachia kirahisi kutokana na mafanikio aliyowapa katika siku za hivi karibuni.

# *Ndoto za Frank Lampard zayeyuka*

**LONDON,** England

NDOTO za Frank Lampard kuipandisha timu yake ya Derby County kwenye Ligi Kuu England ziliyeyuka baada ya kufungwa na Aston Villa mabao 2-1 katika mechi ya fainali ya mtoano wa Ligi Daraja la Kwanza England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Wembley juzi.

Lampard, ambaye ni staa wa zamani wa Chelsea, alikuwa anapewa nafasi kubwa ya kuipeleka Derby County na kuzidi kupandisha chati yake kwenye ukocha.

Hata hivyo, mabao ya Aston Villa yaliyopachikwa na Anwar El Ghazi na John McGinn yalizima ndoto za Derby County.

Kocha wa Aston Villa, Dean Smith sasa amejizolea sifa kutokana na kuipandisha timu hiyo, ambayo inaundwa na yosso wengi. Villa sasa inaungana na Sheffield United na Norwich City kupanda daraja na kushiriki Ligi Kuu England msimu ujao.

Kitendo hicho cha Lampard kushindwa kuipandisha Derby kinaweza kumpunguzia sifa ya kuwaniwa na Chelsea, ambayo inasemekana ilikuwa inafuatilia maendeleo yake kwa karibu ili kumpa nafasi ya kuinoa timu hiyo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# HAZARD AAGA RASMI CHELSEA

## Mbelgiji huyo afunguka yuko tayari kukutana na changamoto mpya...

**BAKU,** Azerbaijan

EDEN EHazard amedokeza kuwa amemaliza safari yake na klabu ya Chelsea baada ya kufunga magoli mawili ambayo yalisaidia kuizamisha Arsenal juzi usiku.

**Chelsea iliibuka na ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Arsenal katika mchezo wa fainali ya Kombe la Europa.**

Kwa mujibu BBC Sport mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa akihusishwa na tetesi za kuhamia Real Madrid na amesema kwa sasa "anasubiria klabu hizo (kukubaliana)."

"Nafikiri hii ni kwaheri kutoka kwangu, lakini kwenye mpira hauwezi kujua kitakachotokea."

Kocha wa Chelsea, Maurizio Sarri amesema anaheshimu uamuzi wa Hazard.

"Najua anataka kuondoka na inanipasa niheshimu uamuzi wake," amesema kocha huyo raia wa Italia na kuongeza: "Ni mchezaji mzuri sana. Ilinichukua miezi miwili au mitatu kumwelewa, sasa namwelewa, japo ni mtukutu lakini ni mtu mwema."

Ikiwa mechi hiyo iliyopigwa katika jiji la Baku ndiyo ya mwisho kwa Hazard, basi itahitimisha safari yake ya miaka saba na miamba hiyo ya rangi ya samawati kutoka jiji la London.

Hazard (28), alijiunga na Chelsea kutokea Lille ya Ufaransa kwa dau la pauni milioni 32.

Ameichezea Chelsea mechi 352 na amefunga jumla ya magoli 110.

Akizungumzia mustakabali wake, Hazard amesema: "Tutafikia uamuzi ndani ya siku chache zijazo - malengo yangu ya msingi kwa wakati huu yalikuwa kushinda kombe hili. Labda sasa ni muda wa kufikiria changamoto nyingine.

"Ndoto yangu ilikuwa kucheza Ligi Kuu England na nimefanya hivyo na moja ya klabu kubwa zaidi."

Hazard alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu England msimu wa mwaka 2014/15, akifunga magoli 14 na kusaidia timu yake kunyakuwa ubingwa.

Msimu wa 2016/17 Chelsea pia walinyakuwa ubingwa wa Ligi Kuu England huku Hazard akifunga magoli 16.

Ubingwa wa sasa wa Ligi ya Europa ni wa pili kwa Hazard akiwa na Chelsea baada ya timu hiyo kushinda kombe hilo mwaka 2013.

Kiungo wa zamani wa Chelsea, Cesc Fabregas amekiambia kituo cha runinga cha BT Sport kuwa: "Hazard akiwa na mpira mguuni unategemea kuna kitu kitatokea na wachezaji wote huwa wanapata nguvu mpya. Siwezi kusema kuwa atakuwa ndiye mchezaji bora zaidi katika historia ya klabu ya Chelsea, lakini ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa zaidi kuwahi kumpata."

## ZISIKUPITE

### ATLETICO, CITY VITANI

ATLETICO Madrid imewasilisha ofa ya pauni milioni 71 kwa ajili ya kutaka kumsajili beki wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell (22), lakini itakumbana na ushindani kutoka kwa Manchester City ambao pia wanamhitaji beki huyo. ***(Sun)***

### MADISON ANUKIA SPURS

KIUNGO wa Everton raia wa England, James Maddison ambaye ana umri wa miaka 22 anawindwa na klabu ya Tottenham. ***(Mirror)***

### YOUNG KUMFUATA ROONEY

BEKI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Ashley Young (33), huenda akaungana na mchezaji mwenzake wa zamani, Wayne Rooney katika Ligi Kuu Marekani (MLS) baada ya DC United kuonyesha nia ya kumhitaji. ***(Manchester Evening News)***

### LUKAKU APATA BARAKA

STRAIKA wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku (26), ameelezwa kuwa anaweza kuondoka Old Trafford na kujiunga na Inter Milan ua Italia. ***(Sun)***

### DEMBELE KUMREJESHA NEYMAR

MABOSI wa Paris St-Germain wako katika mazungumzo na Barcelona ili kumtoa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele, kama sehemu ya mchakato wa kufanikisha straika wa Brazil, Neymar (27), kurejea katika klabu yake ya zamani. ***(RAC1 Sport)***

### PEPE AGOMBEWA ULAYA

WINGA wa Lille, Nicolas Pepe (23) ambaye thamani yake ni pauni milioni 70 anatakiwa na Liverpool, wakati Manchester United na Paris St-Germain pia zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo ambaye ni raia wa Ivory Coast. ***(Star)***

### DYBALA ATAKIWA BAYERN

VIGOGO wa Ujerumani, Bayern Munich wamewasilisha ofa ya pauni milioni 80 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### GRACIA ATAJWA ESPANYOL

KOCHA wa Watford Mhispania Javi Gracia yuko katika orodha ya walimu watano ambao wanapewa nafasi ya kurithi mikoba iliyoachwa na Rubi katika kikosi cha Espanyol. ***(Marca - in Spanish)***

### MENDY KUTUA MADRID

BEKI wa kushoto wa Lyon Mfaransa, Ferland Mendy ambaye ana umri wa miaka 23, anajiandaa kujiunga na Real Madrid. ***(AS - in Spanish)***

### DAYOT ATAKIWA ARSENAL

BEKI wa kati wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Vijana ya Ufaransa (U-21), Dayot Upamecano (20), ametajwa kutakiwa na Arsenal.***(ESPN)***

### MORENO, STUANI KUTUA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Valencia na Hispania, Rodrigo Moreno (28) na mshambuliaji wa Girona na Timu ya Taifa ya Uruguay, Cristhian Stuani (32), wametajwa kuwindwa na Barcelona. ***(Marca)***

## HABARI MICHEZO

## Khamis kumaliza makundi Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa nafasi ya Urais katika Uchaguzi Mkuu wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Khamis Abdallah Said, amesema kuwa endapo ataibuka mshindi katika uchaguzi huo, atahakikisha soka la visiwani hapa linapanda kwa sababu anaamini wana wachezaji wenye uwezo kufanikisha malengo hayo yanatimia.

ZFF inatarajia kufanya uchaguzi wake Jumapili na mchakato huo unafanyika baada ya kuifanyia marekebisho katiba yao. Khamisi alisema hayo jana wakati akinadi sera zake na kueleza kwamba ameandaa dira ya soka atakayoifanyia kazi kwa muda wa miaka minne , kipaumbele kikiwa ni katika kuboresha kiwango cha mpira huo kuanzia ngazi ya chini hadi Taifa.

Alisema kuwa katika dira hiyo ya kuzalisha wachezaji wazuri, pia katika utawala wake atahakikisha sheria, kanuni, taratibu na katiba ya shirikisho hilo vinafuatwa ili kuepusha vitendo vya ubabaishaji.

Aliongeza kuwa akichaguliwa kuliongoza shirikisho hilo ataimarisha umoja na upendo kwa familia yote ya michezo kwa kutumia uzoefu wa uongozi alionao huku pia akijiandaa kutenda haki na kumaliza makundi yaliyopo ambayo yanakwamisha maendeleo. Pia alisema ataendelea kuboresha mahusiano na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), CECAFA, CAF na FIFA huku pia akihitaji kuona Zanzibar inashiriki kikamilifu katika kuijenga Timu ya Taifa (Taifa Stars).

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 38 | 29 | 6 | 3 | 77 | 15 | 93 |
| 2. Yanga | 38 | 27 | 5 | 6 | 56 | 27 | 86 |
| 3. Azam | 38 | 21 | 12 | 5 | 54 | 21 | 75 |
| 4. Kinondoni MC | 38 | 13 | 16 | 9 | 40 | 25 | 55 |
| 5. Mtibwa Sugar | 38 | 14 | 8 | 16 | 36 | 34 | 50 |
| 6. Lipuli | 38 | 12 | 13 | 13 | 32 | 40 | 49 |
| 7. Mbeya City | 38 | 13 | 9 | 16 | 38 | 39 | 48 |
| 8. Coastal Union | 38 | 11 | 15 | 12 | 32 | 42 | 48 |
| 9. Ndanda | 38 | 12 | 12 | 14 | 25 | 37 | 48 |
| 10. JKT Tanzania | 38 | 11 | 14 | 13 | 28 | 34 | 47 |
| 11. Alliance | 38 | 12 | 11 | 15 | 33 | 42 | 47 |
| 12. TZ Prisons | 38 | 11 | 13 | 14 | 30 | 31 | 46 |
| 13. Singida United | 38 | 11 | 13 | 14 | 30 | 39 | 46 |
| 14. Biashara United | 38 | 11 | 12 | 15 | 30 | 35 | 45 |
| 15. Ruvu Shooting | 38 | 11 | 12 | 15 | 35 | 43 | 45 |
| 16. Mbao | 38 | 11 | 12 | 15 | 27 | 41 | 45 |
| 17. Mwadui | 38 | 12 | 8 | 18 | 47 | 52 | 44 |
| 18. Kagera Sugar | 38 | 10 | 14 | 14 | 33 | 43 | 44 |
| 19. Stand United | 38 | 12 | 8 | 18 | 38 | 50 | 44 |
| 20. African Lyon | 38 | 4 | 11 | 23 | 23 | 54 | 23 |

# AUSSEMS : HAIKUWA KAZI RAHISI KUTETEA UBINGWA

**Na Somoe Ng'itu**

HAIKUWA kazi rahisi, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji Patrick Aussems ambaye timu yake ilifanikiwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2018/19 wakati ikiwa na mechi mbili mkononi.

**Mabingwa Simba ambao wamemaliza ligi wakiwa na pointi 93, walikabidhiwa kikombe na medali zao za ubingwa mapema wiki hii baada ya kumaliza mchezo wake wa mwisho dhidi ya wenyeji Mtibwa Sugar ambao ulimalizika kwa sare ya bila kufungana.**

Akizungumza na Nipashe jana, Aussems, alisema kuwa kikosi chake kilikuwa na ratiba ngumu sana msimu huu ambayo haikuwa rafiki, lakini anawapongeza wachezaji na viongozi wa Simba ambao walihakikisha wanapambana ili kutimiza malengo yao.

Aussems alisema kuwa walikutana na ushindani na changamoto mbalimbali katika mechi zote lakini hawakukata tamaa kwa sababu walikuwa wanahitaji kutimiza malengo yao ambayo waliyaweka wakati wanaanza msimu huo uliomalizika Mei 28 kwa kushuhudia African Lyon na Stand United zikishuka daraja.

"Haikuwa kazi rahisi kutwaa ubingwa huu, tulikuwa na safari ndefu na yenye changamoto nyingi, nawapongeza wachezaji wangu kwa kazi nzuri waliyofanya, tulikuwa na ratiba ngumu sana, kucheza mechi 15 ndani ya siku 30, ilikuwa ni ratiba inayoumiza, lakini tunafurahi kuona malengo yetu yametimia, " alisema Aussems.

Kocha huyo alisema pia anawapongeza na kuwashukuru mashabiki wa klabu hiyo ya Wekundu wa Msimbazi kutoka mikoa yote ya Tanzania kwa kushirikiana pamoja kuhakikisha wanamaliza msimu kwa mafanikio.

"Nina furaha sana, baada ya kupambana sana na hatimaye sasa tunafurahia ubingwa," aliongeza Mbelgiji huyo.

Naye kipa chaguo la kwanza wa mabingwa hao, Aishi Manula, alisema siri kubwa ya kikosi chao kupata mafanikio ni ushirikiano walioupata kutoka kwa viongozi, benchi la ufundi pamoja na wao wachezaji kuwa wamoja wakati wote.

"Viongozi walijitahidi kutupa kila kitu kinachotakiwa ili kuhamasisha ushindi, tuliishi vizuri, tulishirikiana pamoja na hatukuwa na hali ya kukata tamaa hata pale tulipopitia wakati mgumu," alisema kipa huyo namba moja pia wa Timu ya Tanzania (Taifa Stars).

Manula aliongeza pia anaipongeza safu ya ulinzi ya timu yao kwa kupambana na kuwa makini kuhakikisha wanalinda vema lango lao na hiyo imesababisha Simba kuruhusu mabao machache ya kufungwa.

Kwa kufanikiwa kutetea ubingwa, Simba ambayo imempa mkataba mpya wa mwaka mmoja kocha wake, Aussems, mwakani itaiwakilisha tena Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



Kiungo mpya wa Yanga, Issa Bigirimana (katikati) akionyesha nakala yake ya mkataba wa miaka miwili baada ya kusaini kujiunga na Yanga. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela. **PICHA: MTANDAO**

# *Katwila afunguka wageni wamesaidia Bara*

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kuwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao umemalizika Jumanne wiki hii ulikuwa mgumu, amewataja wachezaji wa kigeni waliosajiliwa na timu mbalimbali za hapa nchini wamesaidia kuongeza ushindani.

Mtibwa Sugar yenyewe ilimaliza msimu ikiwa katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi baada ya kujikusanyia pointi 50.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila, alisema kuwa ushindani ulioonyeshwa katika mechi zote msimu huu umesaidia kuwajenga wachezaji wazawa ambao wengi wameitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Katwila alisema kuwa pia idadi ya mechi walizocheza msimu huu baada ya ligi hiyo kushirikisha timu 20 badala ya 16, umesaidia kutoa nafasi kwa wachezaji wengi zaidi kucheza.

"Kwanza kabisa tunamshukuru Mungu hadi tumemaliza msimu, Ilikuwa ligi ngumu na yenye ushindani kuanzia mwanzo, kwa mfano sisi tulikaa katika nafasi ya nne kwa muda mrefu, lakini baadaye KMC wakafanikiwa kutushusha," alisema Katwila.

Aliongeza kuwa pia klabu zimepambana kucheza mechi zote bila ya mdhamini jambo ambalo halikutarajiwa kama ingewezekana ukilinganisha na mazingira yalivyokuwa na changamoto mbalimbali.

"Haikuwa kazi ndogo, kucheza bila mdhamini na baadhi ya mechi zikiwa karibu karibu, ila ongezeko la timu limesaidia kiufundi wachezaji wameimarika na wengi wamepata nafasi ya kupangwa, mapungufu machache yaliyojitokeza naamini yatafanyiwa kazi na wasimamizi wetu," Katwila aliongeza.

Aliahidi wanakwenda likizo, lakini atakiboresha kikosi chake ili msimu ujao warejee wakiwa na makali zaidi na hatimaye kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA.

Mtibwa Sugar ndio walikuwa mabingwa watetezi wa mashindano ya Kombe la FA ambayo fainali zake zitachezwa kesho kwa kukutanisha Azam FC dhidi ya Lipuli FC kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi.


# Michezo

Ijumaa Mei 31, 2019

Nipashe




Hazard aaga rasmi Chelsea UKURASA 30



Golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, akiruka bila mafanikio kudaka shuti lililopigwa na mshambuliaji wa Arsenal, Alex Iwobi (hayupo pichani), ambalo liliipa timu yake bao pekee katika mechi ya fainali ya Europa iliyochezwa juzi usiku mjini Baku. Chelsea ilishinda mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yasajili mashine hatari

## ●●● Ni kiungo pacha wa Fei-Toto, yaendelea kuibomoa APR...

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA kuhakikisha inarejea kwenye ubora wake katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki katika msimu ujao, Klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam imeendelea kunasa wachezaji nyota, ambapo jana ilikamilisha mchakato wa kumsajili kiungo, Abdulaziz Makame.

**Kiungo huyo ambaye alikuwa akiichezea Mafunzo ya Zanzibar, amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Yanga akiwa mchezaji huru.**

Makame ambaye aliwahi kuichezea Simba kabla ya kurejea kwao Zanzibar, alionyesha kiwango cha juu katika mashindano ya Kombe la Chalenji yaliyofanyika mwaka juzi katika miji ya Machakos na Kisumu akiwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes).

Mchezaji mwingine mpya aliyesajiliwa na Yanga ni pamoja na beki Mghana ambaye aliwahi kufanya majaribio katika kikosi cha Simba, Lamine Moro ambaye naye amesaini mkataba wa miaka miwili.

Simba iliamua kuachana na beki huyo baada ya kutoridhishwa na kiwango chake wakati akiitumikia timu hiyo katika mashindano ya Kombe la SportPesa yaliyofanyika mwaka jana nchini Kenya.

Taarifa zaidi zinasema kuwa Yanga pia imekamilisha mazungumzo ya kumsajili beki wa Lipuli FC na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Ally Sonso ambaye msimu huu ameisaidia klabu yake kutinga hatua ya fainali ya Kombe la FA.

Nyota mwingine ambaye yuko katika rada za Yanga ni beki wa APR, Eric Rutiga, ambaye inaelezwa kuwa atatua nchini kukamilisha mazungumzo mapema wiki ijayo.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema jana kuwa klabu yao itahakikisha inasajili wachezaji wote waliopendekezwa na benchi la ufundi kwa sababu wanataka kushinda mataji mbalimbali.

"Usajili wetu unaoendelea kufanyika unatokana na mapendekezo ya kocha wetu, Mwinyi Zahera, hii ni ahadi ambayo tuliitoa wakati tumeingia madarakani," alisema Mwakalebela.

Usajili wa Makame na Sonso umekamilika siku moja baada ya Yanga kukamilisha mchakato wa kuwanasa washambuliaji wawili kutoka APR ambao ni pamoja na Mnyarwanda Patrick Sibomana, Mrundi Issa Bigirimana na beki Mghana Lamine Moro kutoka Liberty.

# Simba, AS Vita kukutana tena

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba huenda wakakutana tena na wapinzani wao, AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo katika mechi za mashindano ya Kombe la Kagame ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Julai 7 hadi 21 mwaka huu, jijini Kigali, Rwanda.

Simba iliwafunga AS Vita mabao 2-1 na kutinga katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, na baadaye wao waliondolewa na TP Mazembe ya DRC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Nicholas Musonye, alisema kuwa timu nyingine ambazo zimethibitisha kushiriki mashindano ya Kombe la Kagame kama wenyeji ni Motema Pembe ya Congo na Zesco United kutoka Zambia.

Musonye alisema tayari CECAFA imeshapokea barua za kuthibitisha mwaliko waliopewa kutoka katika timu hizo tatu na wanaamini ushiriki wao utaongeza ushindani katika michuano ya mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema pia maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yatakayochezwa kwa muda wa wiki mbili na kushirikisha timu 18 yako katika hatua za mwisho.

"Timu hizi ni kati ya klabu bora hapa barani Afrika na uwepo wao katika mashindano yetu utazisaidia kuzipa maandalizi mazuri klabu zetu ambazo mwakani zinashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Musonye.

Bingwa mtetezi wa mashindano hayo ni Azam FC ya Tanzania Bara.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002